BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 24 Mei, 2012

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

DUA

Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MHE. ENG. YUSSUF HAMAD MASAUNI (K.n.y. MHE. EDWARD N. LOWASSA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Masauni, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na sasa naomba...

Bado sijakuita Mheshimiwa Leticia Nyerere. Waheshimiwa Wabunge naomba sasa nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, sasa ndiyo nakuita rasmi Mheshimiwa Leticia M. Nyerere. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. LETICIA M. NYERERE (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Leticia Nyerere kwa kudumisha huo ushirikiano.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba tuendelee na *agenda* inayofuata.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 263

Tatizo Sugu la Maji Mufindi Kaskazini

MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y. MHE. MAHMOUD H. MGIMWA) aliuliza:-

Tatizo la maji katika Jimbo la Mufindi Kaskazini limekuwa sugu hasa katika Kata za Ihanu, Mdabulo, Ikweha, Ifwagi, Ihalimba, Kibangu na Mapanda:-

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kutatua tatizo hilo sugu?

(b) Je, Waziri husika atakuwa tayari kutembelea maeneo hayo, ili kuona ukubwa wa tatizo la maji linalowakabili wananchi wa maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba lipo tatizo la upatikanaji wa maji ya uhakika katika Jimbo la Mufindi Kaskazini hususan katika Kata za Ihanu, Mdabulo, Ikweha, Ifwagi, Ihalimba, Kibengu na Mapandali. Upatikanaji wa maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ni 61.1% ya mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto hii Serikali inafanya yafuatayo:-

Ujenzi wa Miundombinu ya maji katika vijiji vya Igomaa kwa gharama ya shilingi milioni 422.9 na Ukami kwa gharama ya shilingi milioni 386.3 unaendelea kupitia bajeti ya mwaka 2011/2012, usanifu wa mradi wa maji katika Kijiji cha Ifwagi umefanyika na kubaini kwamba zitahitajika shilingi milioni 183.2 na utahusisha uchimbaji wa visima 10 kwa uhisani wa Shirika la Maendeleo la Ujerumani. Aidha, Halmashauri inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji unaohusisha ujenzi wa visima vitatu vya maji katika Kijiji cha Mapanda na vitatu katika Kijiji cha Kiponda kwa gharama ya sh. 58,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri imefanya upembuzi yakinifu wa mradi wa maji katika Kata ya Ikweha ambao utahusisha Vijiji vya Ikweha, Ugenza, Ukelemi na Uyela. Kwa upande wa Kata ya Ihalimba, wananchi wanapata huduma ya maji kwa teknolojia ya visima vifupi 14 vilivyoko katika Kijiji cha Ihalimba, Visima 13 vilivyoko katika Kijiji cha Nundwe na Visima saba vilivyoko katika Kijii cha Vikula.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, nipo tayari

kuungana naye kutembelea maeneo aliyoyataja kujionea hali halisi ya upatikanaji wa maji kwa kadiri nafasi itakayopatikana.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, je, Serikali ipo tayari kujenga mtandao huu wa maji katika vijiji vyote kwa sababu tatizo la maji limekuwa ni tatizo kubwa sana katika Mkoa wetu wa Iringa?

Pili, kwa kuwa, tatizo hili si Mufindi tu, ni lini sasa tatizo litakwisha kabisa kwa akinamama wale wa Mkoa mzima katika vijiji vyote, katika Majimbo ya Iringa na Ismani? Kwa sababu ndoa za Iringa sasa hivi ni tatizo, akinamama wanaamka asubuhi kutafuta maji. Kwa hiyo, naomba Serikali iseme lini tatizo hilo litakwisha kwa akinamama wa Iringa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, ndoa za akinamama wa Iringa zipo mashakani.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kwa sababu anafuatilia sana shughuli za maendeleo Mkoa wa Iringa na hasa zile zinazowahusu akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la msingi hapa ni kwamba, tunayo programu ya maji ambayo imeanza utekelezaji wake mwaka 2007. Program hii ilianza kwa kuainisha kwanza vijiji 10 kwa Halmashauri na kwa Halmashauri hii ya Mufindi wao waliainisha vijiji 12. Kwa hiyo, vivyo hivyo katika kila Halmashauri kuna vijiji. Kwa hiyo, ninachoweza kumhakikishia ni kwamba, tumeanza utekelezaji na ndiyo maana katika bajeti yetu iliyopita tuliainisha kwamba, kwa mara ya kwanza mwezi wa Tisa tutakuwa tunakamilisha vijiji vitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya Bunge lako Tukufu kutuongezea shilingi bilioni 184.5 tunaongeza vijiji vingine vitano. Kwa hiyo, mwaka kesho kufikia mwezi wa Sita tutakuwa na vijiji 10, lakini tunatambua kwamba vijiji ni vingi.

Kwa hiyo, tunaomba Halmashauri pia ziweke katika mipango yake wakati Serikali inatekeleza hivi vijiji 10 na wao waainishe vingine ambavyo wanaweza wakaingiza kwenye mipango kwani tukitekeleza kwa pamoja tunaweza tukatimiza azma ya kuwapatia wananchi maji mapema na hivyo kunusuru ndoa ambazo zina utata. (*Makofi*)

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa, tatizo la maji lililopo katika Jimbo la Mufindi Kaskazini linafanana kabisa na tatizo la maji lililopo katika Kijiji cha Kichonda, Wilaya ya Liwale. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kukipatia kijiji hiki maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nataka niseme kwamba, nimefika mwenyewe Liwale na kijiji alichokitaja tulikitembelea tukiwa kwenye ziara ya Mheshimiwa Rais na tuliahidi kwamba tutachimba visima. Mpaka sasa wataalam wameshakwenda pale kwa ajili ya kuainisha tathmini ili baadaye tupeleke fedha na baadaye tuchimbe visima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kumhakikishia kwamba, tunalifahamu tatizo la maji la Liwale na kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba, tutatekeleza ili kuona kwamba wananchi wanapata maji vijiji vyote awamu kwa awamu.

Na. 264

Malipo ya Walimu Wilayani Bunda

MHE. ESTER A. BULAYA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawalipa mishahara ya zaidi ya miezi miwili wanayodai Walimu hususani wenye ajira mpya Wilayani Bunda?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Amos Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeboresha mfumo wa kuwahudumia watumishi wapya wakiwemo Walimu wanaoajiriwa kwa kuwalipa mishahara na stahili zao nyingine kwa wakati. Mishahara kwa waajiriwa wote wapya hulipwa baada ya mwajiriwa kujaza fomu za ajira na kuwasilisha taarifa binafsi ikiwemo vyeti vya kitaaluma na kitaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hatua hizo, Halmashauri huwaingiza katika mfumo wa malipo – *Lawson version 9* ambao hupeleka moja kwa moja majina hayo kwa njia ya mtandao wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya kuidhinishwa na kwa maandalizi ya malipo ya mshahara katika mwezi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Walimu wapya, wamekuwa wanakosa mishahara yao kwa sababu ya kuchelewa kuripoti au kushindwa kuwasilisha nyaraka zinazothibitisha sifa zao za kitaaluma na kitaalam. Walimu 14 kati ya 296 wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda walichelewa kuingia katika mfumo wa malipo kwa sababu hizi. Kwa hivi sasa ni Walimu wanne tu wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ambao hawajaingia katika orodha ya malipo ya mishahara kwa mwezi Mei, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wanaokosa mishahara katika miezi ya mwanzo ya ajira hujaza fomu maalum ya madai na baadaye kutumwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi. Baada ya kuidhinishwa hutumwa Hazina kwa ajili ya Malipo. Aidha, Wakurugenzi wa Halmashauri wamekuwa wanasisitizwa kuhakikisha kuwa, wanawahudumia Walimu wote waliopo vituoni na

hawajaingia katika orodha ya malipo ya mishahara ili waweze kujikimu wakati taratibu za kuwaingiza katika orodha ya malipo zinafanyika.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza napenda kuipongeza timu ya Walimu ya Wilaya ya Bunda kwa kuwa mabingwa wa mwaka huu wa michuano ya *Esther Cup*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Moja pia ya malalamiko ya Walimu wa Wilaya ya Bunda ni kwamba, wanapokwenda kujiendeleza wakirudi wanakaa miaka mitatu kwa mujibu wa taratibu ambazo zimewekwa. Mpaka ninavyozungumza Walimu ambao wamekwenda na miaka mitatu imepita hawajapandishwa madaraja. Sasa Serikali inasemaje kuhusu hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ambalo ni tatizo katika Wilaya ya Bunda na maeneo mengine, hivi ninavyozungumza shule nyingi katika Wilaya ya Bunda ina Mwalimu mmoja wa Hisabati na Mwalimu mmoja wa somo la Sayansi. Sasa ni lini Serikali itahakikisha inapeleka Walimu wa kutosha ili vijana wenzangu waweze kufaulu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kushindwa au kuchelewa kupandishwa kwa wakati inategemea na alichokwenda kukisomea, kwa sababu wakati mwingine anaweza kuwa alishapita ukomo na kile alichokwenda kusomea hakiwezi kumwongezea chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, wale ambao wanastahili sasa tumeziimarisha *TSD* na tunahakikisha kwamba wanawezeshwa ili kuweza kukaa vikao vya kisheria na kuweza kuwapandisha madaraja Walimu inavyotakiwa. Kwa hiyo, tunawaomba *TSD* watimize wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuwa na Walimu wachache wa Hisabati, kama nilivyosema katika jibu la msingi, mwaka huu tumepeleka Walimu 296 katika Wilaya ya Bunda, tunachoomba Halmashauri iwapange Walimu kwa uwiano kwa sababu katika maeneo mengi unakuta baadhi ya Walimu wamerundikana katika maeneo ya miji na katika maeneo ya pembezoni kunakuwa na Walimu wachache au Walimu wa masomo fulani. Kwa hiyo, tunachoomba wawapange vizuri ili kuhakikisha kila eneo wanapata Walimu kwa uwiano unaostahili.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la Walimu, mishahara na maslahi limekuwa ni tatizo la kudumu na kila Mbunge analalamika ndani ya Bunge hili. Hivi Serikali, kwa nini hamwoni umuhimu wa kuondoa matatizo ya Walimu kwa mkupuo ili mkatoa hili tatizo la Walimu kulalamika Tanzania nzima kila siku? *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la malalamiko ya watumishi wakiwemo Walimu na watumishi wengine, ukienda kwa masuala ya mishahara, kuchelewa kuingizwa katika *payroll* kama ambavyo swali la msingi lilikuwa linasema, sasa hivi tumeanzisha huo mfumo ambao zamani ulikuwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, lakini sasa hivi tumepeleka katika Halmashauri zote.

Mtumishi akiajiriwa anajaziwa fomu na anaingizwa katika Halmashauri yake pale pale na inakwenda kwa njia ya mtandao Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la mtumishi kuajiriwa akakaa muda mrefu bila kupata mshahara tumetatua kero hiyo kwa zaidi ya asilimia tisini na kitu, kwa sababu kama utakavyoona kati ya Walimu 296 ni Walimu 14 tu ndiyo walikuwa wamechelewa, lakini mpaka sasa hivi

ninavyozungumza, bado Walimu wanne tu. Sababu za wao kuchelewa ni wao wenyewe kuwa na vyeti vyenye mashaka na wengine kwenda kuripoti maeneo tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukija katika upande wa madai yao, kwa kweli kazi inafanyika. Mpaka sasa hivi katika madai ya Walimu zaidi ya 93% yameshalipwa, isipokuwa ni kitu ambacho hata ukilipa yanazaliwa tena na tena. Lakini kimsingi Serikali inajitahidi sana kuondoa kero za watumishi wakiwemo Walimu na watumishi wengine.

Na. 265

Kuunda Kata Mpya Tongwe

MHE. SELEMANI J. ZEDI (K.n.y. MHE. MOSHI S. KAKOSO) aliuliza:-

Kata ya Mpanda Ndogo inayojumuisha Vijiji tisa vilivyotawanyika mbalimbali sana ilipendekezwa igawanywe kupata Kata mpya ya Tongwe, lakini katika uchaguzi uliopita ilikataliwa na Tume ya Taifa kwa kigezo cha kupeleka mikapa isiyotambuliwa na Tume:-

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha Kata mpya ya Tongwe inaundwa na kutangazwa?

(b) Je, Serikali haioni kuchelewesha kutangaza Kata hiyo kunachelewesha pia maendeleo ya wananchi kwenye maeneo hayo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Suleimani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu zote za kuanzisha Kata mpya ya Tongwe tayari zimekamilika ikiwa ni

pamoja na kujadiliwa katika vikao mbalimbali halali kama vile Kamati ya Maendeleo ya Kata (*WDC*), Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya (*DCC*) na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*).

Hata hivyo, Kata mpya ya Tongwe haikufanikiwa kuwa miongoni mwa Kata mpya zilizoanzishwa kwa tangazo la Serikali namba 173 la tarehe 7 Mei, 2010 kutokana na kutokamilisha taratibu za kuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, badala yake Mkoa uliwasilisha maombi ya Kata hiyo Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo ilibaini kwamba Kata hiyo haijaanzishwa kisheria.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kabla ya uchaguzi Mkuu mwaka 2015 inakusudia kuchambua maombi mapya ya Kata na Vijiji, Kata mpya ya Tongwe itajumuishwa na kufanyiwa kazi pamoja na maombi mengine mapya yatakayokuwa yamewasilishwa kabla ya kipindi hicho cha uchaguzi. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI inampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada kubwa na ufuatialiaji kuhusu pendekezo hili ambalo linakusudia kusogeza huduma za jamii karibu na wananchi hasa kwa kuzingatia jiografia ya Mkoa wa Katavi.

MHE. SULEIMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, hata hivyo nina swali la nyongeza. Kwa kuzingatia Sheria ya Uanzishwaji wa Maeneo Mapya ya Utawala kama Kata, Wilaya na kadhalika, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega tumeanzisha mchakato wa kupendekeza Kata mpya na Halmashauri ya Wilaya ya Bukene na Wilaya ya Bukene.

Je, mapendekezo hayo yatakapofika kwenye ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwa yatakuwa yamekidhi vigezo vyote, yamefuata taratibu ya uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala, Serikali itakuwa tayari katika mwaka wa fedha ujao 2014/2015, kuitangaza Halmashauri mpya ya Bukene na

Wilaya mpya ya Bukene kwa kuwa itakuwa imekidhi vigezo vyote na imefuata taratibu na vikao vyote halali vinavyohitajika katika suala hilo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida Kata au Wilaya hata kama zitatimiza vigezo, mwaka halali wa kutangaza ni 2015 wakati tukielekea kwenye uchaguzi, Vijiji ndivyo ambavyo tunategemea kutangaza mwaka 2014. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama vigezo vitakamilika tutangaza hayo maombi yake kwa mujibu wa taratibu na muda ukataporuhusu.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi pia sitofautiani na swali la Mheshimiwa Zedi. Wilaya ya Arumeru imekuwa ni kubwa sana na tayari tuna Halmashauri mbili kwa maana ya Halmashauri ya Meru na Arusha *DC* kwa Mheshimiwa Medeye kwa miaka kadhaa sasa, na tayari tumeshapitia *procedures* zote na tulishapata baraka zote kutoka kwenye vikao vya mashauriano ya Mkoa kwa zaidi ya miaka mitatu ili kwamba, Halmashauri ya Meru iwe Wilaya kamili na ile Halmashauri ya Arusha Vijijini ibaki kuwa Wilaya ya Naboishu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, mwaka halali wa kutangaza ni 2015, je, sasa yuko tayari kufuatilia maombi yetu ili ajue kwamba yamekamilika ama yana kasoro au tatizo lolote ili tuweze kurekebisha ili ifikapo mwaka 2015 na sisi Halmashauri ya Meru tuweze kutangazwa kuwa Wilaya kamili ya Meru?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ofisi yangu inaendelea kupokea maombi yote iwe ni ya Wilaya, Halmashauri, Kata na Vijiji. Tunapopokea tunaangalia vigezo na kufuatilia katika maeneo hayo ili wakati ukifika, basi wanaostahili wapewe kile walichokiomba na wasiostahili waambiwe nini cha kufanya.

Na. 266

Athari za Magugu Maji Ziwa Jipe

MHE. BETTY E. MACHANGU aliuliza:-

Sekta ya Uvuvi katika Mkoa wa Kilimanjaro inakabiliwa na changamoto ya kushamiri kwa magugu maji aina ya *typha SP* katika Ziwa Jipe upande wa Tanzania ambayo asilimia sitini na tano (65%) ya shughuli za uvuvi zimesimama, ikilinganishwa na upande wa Kenya halina magugu:-

(a) Pamoja na taarifa za kuwepo kwa mradi wa *UNDP* wa *Sustainable Land Management* wa 2011 – 2013 ambapo wataalam kutoka Israel wamefanya upembuzi wa awali. Je, utafiti huo unaleta matumaini gani kuhusu kuendelea kuwepo kwa Ziwa Jipe?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kulinusuru Ziwa hilo kutokana na taarifa ya huo utafiti wa awali uliofanywa?

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA) alijibu**:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Ziwa Jipe upande wa Tanzania sehemu kubwa inakabiliwa na changamoto ya kushamiri kwa magugu maji aina ya *Typha* na upande wa Kenya haujaathirika sana na magugu maji. Hali hii inatokana na mipango tofauti ya matumizi ya ardhi yanayoendelea upande wa Kenya na upande wa Tanzania kuzunguka ziwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kenya ziwa hili limezungukwa na hifadhi ya Tsavo Magharibi ambayo hakuna shughuli zozote za kibinadamu zinazoendelea zaidi

ya kuhifadhi wanyamapori. Kwa upande wa Tanzania ziwa limezungukwa na vijiji ambavyo hujishughulisha na kilimo kisicho endelevu. Hali hii husababisha kutiririka kwa tope na virutubisho/mbolea katika ziwa na kuchangia kushamiri kwa magugu maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua tatizo hilo, Serikali kupitia mradi wake wa mpango wa matumizi endelevu ya ardhi ikishirikiana na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)*, ilikuwa na mpango wa kuleta wataalam kutoka Israel ambao watafanya upembuzi wa awali wa jinsi ya kuondoa magugu maji hayo. Hata hivyo, zoezi hilo bado halijafanyika kwa kuwa, mchakato wa Serikali na *UNDP* wa kutekeleza suala hili bado haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kupitia mradi nilioutaja imeendelea kukuza uelewa na kuhamasisha wananchi kupanda miti ya asili katika maeneo yanayozunguka vyanzo vya maji ili kulinda ziwa Jipe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2013/2014, Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga imetenga sh. 86,039,100 kwa ajili ya shughuli za uhifadhi wa ardhi pamoja na upandaji wa miti wenye malengo ya kuotesha miti zaidi ya 45,000 msimu wa mvua za masika.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri amesema kwamba, kaya zinazozunguka Ziwa Jipe zinafanya kilimo ambacho si endelevu, lakini kupanga ni kuchagua, kwa nini Serikali isizipange kaya hizi, ikalinusuru ziwa hili wakaweza kufanya utalii wa majini *aquan tourism* na *spot fishing* kwa ajili ya kulipa Taifa tija zaidi na hata wananchi wa kaya hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kama utekelezaji wa swali langu la nyongeza la kwanza utakuwa unasuasua na kwa sababu uhai wa ziwa hili unatetereka sana kwa

sababu ya magugu maji sugu, je, Serikali sasa iko tayari kulibadilisha eneo hili kuwa *game reserve corridor* likaunganishwa na hifadhi ya Mkomazi na Tsavo ya Kenya kwa ajili ya kuliletea Taifa tija zaidi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wake wa kubadilisha au kuwahamisha wananchi kutoka katika eneo hilo unazingatia zaidi Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 ambayo inatoa nafasi kwa mkoa wenyewe kupitia *RCC* na Wilaya husika kupitia Halmashauri kuweza kujipangia kwa namna gani ardhi au eneo fulani liweze kutumika.

Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Machangu kupitia *RCC* yake kama wanaona hiyo ndiyo njia nzuri zaidi, basi awasiliane na Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii, ili tuweze kuona ni kwa namna gani tunaweza kushirikiana kuhakikisha kwamba, mpango huo unakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwezekano wa kuiunganisha na Mkomazi na Tsavo ambayo iko upande wa Kenya, nirudie tu kusema kwamba, kama *RCC* au Halmashauri itaona jambo hili ni zuri na idadi ya watu walioko pale ni ndogo na wanaweza kuhamishwa, basi tuwasiliane ili tuone ni namna gani tunaweza tukatekeleza.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, kumekuwa na tatizo kubwa kwa Tanzania, kukata miti hovyo na kutumia kama alama za barabara. Je, Mheshimiwa Waziri haoni huu ni uharibifu wa mazingira? Kwa nini isipitishwe sheria ya kuzui kukata miti hovyo na kuitumia kama alama za barabarani?

MWENYEKITI: Hilo ni swali jipya, lakini Mheshimiwa Waziri unahifadhi mazingira.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ukataji wa miti

wa aina yoyote ambao siyo endelevu unaharibu mazingira. Hata ukataji wa miti kwa lengo la kuweka alama barabarani sidhani kama unazingatia sheria kwa sababu sheria inataka uwe na *triangle*. *Triangles* ndizo zinatambuliwa kama alama halali za kumwezesha mtu kuona kwa mbali. Sina uhakika kama miti inawawezesha wananchi kuona kwa mbali. Kwa hiyo, watu hawa hawazingatii sheria na wanazivunja. Tutaendelea kupambana nao kwa jinsi ambavyo sheria inaelekeza.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na swali linalofuata, nimepokea barua sasa hivi kutoka kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, kupitia Ofisi ya Mheshimiwa Spika, ikinitaka niwafahamishe rasmi kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu hatakuwepo leo katika mji wetu wa Dodoma na vilevile ndani ya ukumbi wa Bunge kwa ajili ya kuongoza shughuli za Bunge ndani ya Bunge na hapa Dodoma. Kwa hivyo basi, atakayekaimu nafasi yake ni Mheshimiwa Mathias Chikawe, Waziri wa Katiba na Sheria. (*Makofi*)

Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naomba mtambue kwamba, sasa Kaimu Waziri Mkuu ni Mheshimiwa Mathias Chikawe.

Baada ya tangazo hilo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia ofisi ya Spika. Sasa tunaendelea na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mbunge wa Bukombe.

Na. 267

Ahadi ya Kupeleka Umeme Bukombe

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI aliuliza:-

Serikali iliahidi kupeleka umeme Bukombe tangu mwaka 2000 na ahadi hiyo imerudiwa mara kadhaa mwaka 2005, 2010 na 2011:-

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Bukombe kuhusu utekelezaji wa ahadi hiyo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mbunge wa Bukombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kupeleka umeme makao makuu ya Wilaya ya Bukombe (Ushirombo) upo chini ya miradi inayojulikana kama *Electricity Five (V)*. Fedha za kutekeleza mradi huu zimekwishapatikana kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* na taratibu za kumpata mkandarasi nazo zimekamilika na mkandarasi ni kampuni *Eltel Network ABTE* ya kutoka Sweeden.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yatakayonufaika na mradi huu ni Ushirombo yenyewe pamoja na Vijiji vifuatavyo:- Lunguya, Shilela, Segese, Ikinda, Ushirika, Mlale, Bwelwa (Mbogwe), Nanda, Ituga, Shule ya Msingi Ituga, Bukombe, Lubeho, Shinyanga B, Masumbwe, Mzambarauni, *Cagry Ginnery*, Kagwe, *Nipha Ginnery*, Bintubili "A" Bintubili "B" Nyakafuru, Kakumbi na Lunzewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi utahusisha ujenzi wa njia ya umeme kutoka Kijiji cha Ilogi hadi Ushirombo, ufungaji wa transfoma na kuwaunganisha wateja wa awali wapatao 5,000. Mradi huu utagharimu kiasi cha dola za Marekani milioni 10.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimsihi Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Bukombe na Mbogwe wavute subira, mradi utaanza wakati wowote mwaka huu na kukamilika mapema mwaka ujao.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, tatizo la miradi hii ya umeme huwa haianzi kwa wakati na huwa haikamiliki kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru tu Mheshimiwa Naibu Waziri toka mwaka jana nimekuwa nikifuatilia suala hili na kwa kweli amekuwa na ushirikiano mzuri sana. Mwaka jana aliniambia mradi ungeanza mwezi Oktoba mwaka jana. Sasa hivi ananiambia mradi utaanza wakati wowote mwaka huu. Sasa ni lini hasa mradi utaanza maana wananchi wa Bukombe na Mbogwe wanauliza kuhusu suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, umeme wa *Electricity Five (V)* kutoka Ilogi hadi Lunzewe utapita kwenye maeneo mengi ambayo yana shule za msingi, zahanati na vituo vya afya. Katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema shule ya msingi itakayopata umeme ni ile ya Ituga, je, hizi shule nyingine za msingi na vituo vingine vya huduma za jamii kama vituo vya afya na zahanati havitapata umeme?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli toka mwaka jana tuliahidi tungeweza kuanza mwezi Oktoba, lakini kwa sababu ya mchakato wa kufuata sheria, kutokana na namna tunavyopata fedha zinatoka kwenye taasisi za kifedha nje ya bajeti yetu ya ndani, pengine mchakato huu unakwenda kinyume na taratibu tunazozipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, mwaka huu ni lazima mradi huu utaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ameuliza kwamba, kutoka Ilogi hadi Lunzewe ambapo mradi huu utatekelezwa na zimetajwa baadhi ya sehemu za huduma za jamii kama zahanati au shule za msingi, je, zingine zote zitapitiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, miradi hii ambayo inatekelezwa kwa fedha za ufadhili, wakati mwingine huwa ni kutokana na ile *study* waliyoifanya awali ndivyo utekelezaji wake unavyokuwa. Kwa hiyo, pale ambapo walipitisha *study* yao, wakafika ,ndipo ambapo umeme huu utapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali kupitia Wakala Wa Umeme Vijijini *(REA)*, sisi tutaendelea kutoka pale wanapoishia. Kwa hiyo, hakuna ambapo umeme utapita na wananchi wakauona tu unapita wasiweze kuingiziwa kwenye huduma zao za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwamba, kwenye ile miradi kama ya *MCC*, *Electricity Five (V)* na mingine kama ya *back borne,* kila ambapo umeme utapita tutahakikisha kwamba, kwenye huduma za jamii umeme huu unafikishwa.

MHE. LAIZER M. LEKULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Wizara hii imetupangia majina ya vijiji vingi sana na nawashukuru sana kwa kupanga hayo majina ya vijiji, nadhani karibu 2000 vya Tanzania nzima. Kwa kuwa, vijiji vya Kamonga, Erbaswa, Kitende na Olmorok mpaka Tingatinga vilikuwepo kwenye orodha hiyo. Hii ni bajeti ya saba sasa, hivyo vijiji vikiwa katika orodha, je, mwaka huu tutapata umeme ili tusiendelee kusubiri kama ilivyokuwa kwa miaka tuliyosubiri? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba vijiji hivi vimekuwa kwenye orodha na tumekuwa tukidhamiria kutekeleza na sasa tumefikia hatua ya kutekeleza kweli. Lakini Mheshimiwa Laizer yeye mwenyewe pamoja na wananchi wa Longido ni mashahidi kwamba, siku

za nyuma walizungumzia Wilaya ya Longido kutokuwa na umeme, lakini leo wanao umeme, kwa hiyo, hatua kidogo kidogo za maendeleo zinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mradi wa umeme katika vijiji alivyovitaja vya Kamwanga mpaka Elmorok utatekelezwa katika awamu hii na mwaka huu utaanza kutekelezwa. Ni matumaini yangu makubwa kwamba, kabla ya mwaka 2015 miradi ya umeme katika maeneo haya ya Kamwanga mpaka Elmorok kwa vijiji vyote vile tutatekeleza.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda hauturuhusu, bado tuna maswali mengi kidogo, naomba tuendelea na swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Suleiman Nchambi Suleiman, Mbunge wa Kishapu.

Na. 268

Kuwasaidia Vifaa na Mitaji Wachimbaji Wadogo wa Madini - Kishapu

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN aliuliza:-

Wapo wachimbaji wadogo wa madini katika migodi ya Kata za Songwa, Mwadui, Lohumba, Uchunga na Mondo ambao wanamiliki maeneo hayo kihalali ambao wengi wao hulazimika kuingia maeneo ya wawekezai wakubwa kwa kukosa mitaji na nyenzo za kufanyia kazi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia mitaji na nyenzo za kufanyia kazi wachimbaji hao wadogo wadogo ili waweze kunufaika na rasilimali hizo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Nchambi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua na kuthamini mchango wa wachimbaji wadogo katika kuinua uchumi na pato la Taifa ikiwa ni pamoja na kutoa ajira kwa Watanzania walio wengi hasa waishio vijijini. Inakadiriwa kuwa Watanzania wapatao 1,000,000 wanajishughulisha na kazi hiyo ya uchimbaji.

Kutokana na hali hiyo, kuanzia mwaka 2009/2010, Serikali ilianzisha mpango wa kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uchimbaji mdogo nchini kwa lengo la kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo ili waweze kununua vifaa bora vya uchimbaji na uongezaji thamani katika madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni mbalimbali zilizokwisha kopeshwa fedha kwa ajili ya kuanzisha vituo vya ukopeshaji na ukodishaji wa vifaa vya uchimbaji kwa wachimbaji wadogo ni kama ifuatavyo:-

(i) *STAMICO* ilikopeshwa sh. 200,000,000 kwa ajili ya kuanzisha kituo cha kukodisha vifaa vya uchimbaji madini eneo la Rwamgasa Geita. Wachimbaji wataweza kununua vifaa hivyo kwa utaratibu wa kukopeshwa kisha kulipa kidogo kidogo wanapofanikiwa;

(ii) Kampuni nyingine *Tan Discovery Mineral Consultancy Company Limited* shilingi 180,000,000 (kati ya 200,000,000 walizoomba). Tayari wameshaanzisha kituo cha kukopesha vifaa eneo la Londoni, Singida. Ukodishaji wa vifaa unaendelea;

(iii) Kilimo *G and General Suppliers Limited* shilingi 60,000,000 (Kati ya 200,000,000 walizoomba). Ujenzi wa kituo kwa ajili ya usagaji mawe ili kupata kokoto unaendelea;

(iv) *Gemstyle Co. Limited* sh. 35,000,000 kwa ajili ya uongezaji thamani madini (vito); na

(v) *C.E. Holding (T) Limited* sh. 50,000,000 kwa ajili ya uongezaji thamani madini.

Mikopo hiyo kwa kampuni huendelea kutolewa baada ya kukagua na kuona kuwa fedha zilizotolewa hapo awali zimetumika kwa malengo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wadogo wa maeneo ya Songwa, Mwadui, Lohumo, Uchunga na Mondo wanayo fursa ya kupata mikopo kupitia utaratibu niliouelezea hapo juu ambapo mikopo hiyo itakuwa inapitia benki kwenye dirisha la wachimbaji wadogo. Tunawashauri wachimbaji wa maeneo hayo waone umuhimu wa kuungana ili iwe rahisi kukopesheka kupitia utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tunapenda kueleza kuwa siyo lazima mikopo itolewe na Serikali peke yake, bali inaweza kutolewa kupitia Taasisi zingine za kifedha kama vile benki mbalimbali ilimradi wachimbaji watimize vigezo vinavyotakiwa na Taasisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa wito kwa wachimbaji wote wanaovamia maeneo ya wawekezaji wengine kuacha vitendo hivyo na badala yake waendeleze maeneo wanayomiliki kwa mujibu wa sheria. Uvamizi wa leseni kubwa za utafiti unatishia nchi yetu kukosa miradi mikubwa ya migodi mipya katika siku za usoni.

MHE. SULEIMAN M.N. SULEIMAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu marefu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, Serikali inamiliki asilimia 25 ya hisa za mgodi wa Mwadui na kwa kuwa, inamiliki asilimia 25 ya hisa hizo kwa niaba ya wananchi wakiwemo wananchi wa Jimbo la Kishapu. Je, Serikali ipo tayari kuachia mrabaha wa asilimia mbili kwa wananchi wa Jimbo la Kishapu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa kuwa, mgodi wa almasi wa Mwadui ni mgodi mkongwe ulioanza shughuli zake mapema mwaka 1954 na baadaye mwaka 1963 baada ya kukamilika kwa sheria za nchi yetu. Je, Serikali ipo tayari kutoa

kipaumbele kwa wananchi wanaoishi maeneo ya mgodi wa Mwadui kwa maana ya akinamama na akinababa na vijana wa Jimbo na Wilaya ya Kishapu ili kutoa mfano mzuri kwa wananchi wengine wenye migodi ili kuepuka matatizo makubwa yanayoendelea Mtwara? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia kero za wanachi wake wa Kishapu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niliweke wazi kwamba, mapato rasmi ya Serikali yanatokana na kodi, tozo, misaada pamoja na mikopo. Halmashauri ya Kishapu kama zilivyo Halmashauri zingine nchini kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 inayo haki ya kisheria ya kukusanya kodi mbalimbali ambazo zimeelezwa kwenye sheria ile ikiwemo kodi za Majiji, kodi za Halmashauri na kodi za Mamlaka ya Miji midogo na kodi za Halmashauri za vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo bila kuathiri matakwa ya sheria hiyo hasa kipengele cha (6), (7), (8) mpaka kipengele cha (9) ambacho kinatoa mamlaka hayo, kama nilivyosema Halmashauri lazima imshirikishe Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ili kuweza kuona kama mapato hayo yaliyoainishwa katika Sheria ya Serikali za Mitaa yanaweza kugawanywa ili Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu iweze kupata mapato ambayo imeyazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria hiyo hakuna mtu yeyote anaweza kubadilisha mapato ya Serikali bila kufuata *consultation* na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kweli kwamba Mgodi wa Mwadui ni mgodi wa siku nyingi na wananchi wa eneo hilo wamekuwa wakipata shida nyingi wanaozunguka eneo la mgodi. Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ikiwemo hasa kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji

wadogo kwenye eneo la Magaso ambapo kuna leseni za wachimbaji wadogo, nyingi zimetolewa kupitia vikundi na wachimbaji binafsi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito tu kwa wachimbaji wadogo wa Mwadui na maeneo yanayozunguka mgodi ule kuendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali na sisi Wizara ya Nishati na Madini tutakuwa tayari kutoa ushirikiano wa kutosha ili kuhakikisha mgodi ule unatoa manufaa zaidi kwa wananchi wanaozunguka eneo hilo pamoja na Wilaya ya Kishapu kwa ujumla na hasa kwenye maeneo ya kulipa kodi na tozo mbalimbali zinazostahili katika Wilaya ya Kishapu kwa mujibu wa sheria.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa, ni nia njema ya Serikali kupata mapato na kuendeleza uchumi wa Taifa kupitia migodi hii na kuwawezesha Watanzania kiuchumi hasa wawekezaji wadogo wadogo. Buhemba kuna matatizo kati ya *STAMICO* na wawekezaji wadogo wadogo tunapozungumza sasa na jana hali ilikuwa mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa *STAMICO* wakapigwa na wachimbaji wadogo wadogo wanahitaji kupewa haki yao kwenye machimbo ya Buhemba. Je, Serikali itatatuaje tatizo hili na matatizo ya wawekezaji wengine wote nchini nzima kabla ya hali haijawa mbaya zaidi, kinga ni bora kuliko tiba. Serikali inawaambia nini wana Buhemba na kuwapa haki zao ili tuweze tukawapa uwezo wawekezaji wa ndani zaidi kuliko wa nje? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli jana palitokea matatizo pale Buhemba kwenye leseni inayomilikiwa na *STAMICO* ambapo wachimbaji wadogo waliweza

kupambana na wamiliki wa leseni kisheria ambayo ni *STAMICO* ambayo ni Taasisi ya kimkakati ya Serikali ambayo ilianzishwa kwa makusudi kabisa ya namna gani Serikali itajihusisha na uwekezaji hasa kwenye Seta ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanya jitihada nyingi sana kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo wote kwenye maeneo yote yanayozunguka migodi mikubwa wanapatiwa maeneo ya kufanyia kazi yao ili kutoa fursa pia kwa migodi mikubwa kuweza kufanya shughuli zao uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba Serikali inapata mapato mengi kupitia uwekezaji mkubwa huu wa migodi, lakini pia inaheshimu uwepo wa wachimbaji wadogo kwa sababu inatoa ajira kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa wito kwa Watanzania wote wanaojihusisha na shughuli za madini kufuata Sheria za Madini, anayemiliki leseni anamiliki kisheria. Hivyo, Wizara yangu inaendelea kuongea na migodi mikubwa kwenye maeneo ambayo wanadhani kwamba, uwekezaji mkubwa hautokuwa na faida ili tuyatenge kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo tutaweza kupata maeneo hayo bila misuguano na migogoro. Niwaombe wananchi wa Buhemba wawe wavumilivu, tunapitia kwa makini eneo hilo na kuangalia ni maeneo gani tunaweza kuyatenga kwa ajili yao na kuacha uwekezaji mkubwa uendelee.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Vita Kawawa utanisamehe, majibu yamekuwa marefu sana na kwa kuwa kesho tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini nadhani tutajipanga tu. Naomba tuendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Gosbet Blandes na Mheshimiwa Mwijage kwa niaba yake.

Na. 269

Bodi ya Mazao Mchanganyiko

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE (K.n.y. MHE. GOSBERT B. BLANDES) aliuliza:-

Sheria ya Kuunda Bodi ya Mazao Mchanganyiko ilikwishatungwa na ililenga kuondoa unyonyaji unaofanywa kwa wakulima wetu kuuza mazao yao kwa debe na gunia badala ya kupima mazao yao kwa kilo.

Je, lini Bodi hiyo itaanza kufanya kazi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ilianzishwa kwa Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Namba 19 ya mwaka 2009. Chimbuko la kuanzishwa Bodi hiyo ni kusisimua ushindani katika biashara ya nafaka na mazao mengine na kuwa chombo cha rejea katika biashara ya mazao ya nafaka ili kujenga ushindani ambao unampa mkulima kinga dhidi ya wanunuzi binafsi na walanguzi, ikiwa mazingira ya soko hayatakuwa ya ushindani na manufaa kwa mkulima. Bodi hii itakapoanza kazi kikamilifu itasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao ya nafaka na mazao mengine mchanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kuzinduliwa Bodi hiyo imekuwa kwenye mchakato wa kuandaa miongozo mbalimbali kwa lengo la kuijengea uwezo wake ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kuandaa Kanuni za Sheria, Muundo wa Bodi, Miundo ya Watumishi,

Kanuni za Watumishi na Kanuni za Fedha. Aidha, Bodi imeanza mchakato wa kuandaa Mpango Mkakati yaani *Strategic Plan.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa Bodi hiyo inaanza kufanya kazi, Serikali imeikabidhi baadhi ya mali za zilizokuwa Shirika la Taifa la Usagishaji *(NMC*) ikiwa ni pamoja na kinu cha kusagisha mahindi cha Iringa ambacho kina uwezo wa kusagisha mahindi tani 60 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu hayo. Aidha, Bodi itaanza kutumia kinu cha Iringa kibiashara kwa kushirikiana na *NFRA* kusagisha mahindi. Aidha, Bodi imepanga kutumia mali zingine ilizokabidhiwa kwa kuingia ubia na Sekta Binafsi kupitia utaratibu wa (*PPP*) ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri lilivyoeleza mchakato wa kuunda Bodi umechukua muda mrefu. Kwanza, ningependa kujua nini mikakati ya Serikali katika kuwalinda wananchi ambao wanaendelea kuteseka kupitia njia za ununuzi za *rumbesa* na *balimanyaila*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali imeanza kufikiria na kutekeleza Mpango wa Bodi kama ilivyoainisha kwa kugawa maeneo ya *NMC,* Iringa kwenda kwenye Bodi. Je, nini fikra na matekelezo ya Serikali katika kuainisha ujenzi wa *SILOS* na maghala makubwa katika Mkoa wa Kagera ili tuweze kukusanya nafaka kwa ajili ya hifadhi ya Tanzania na nchi zinazotuzunguka?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Mheshimiwa Gosbert aliuliza swali hili aki-*refer* kwenye zao la maharage kama zao mbadala kwa upande wa Kagera, tulisema wakati huo kwamba katika kuanzisha hii Bodi, hili siyo jambo la mara ya

kwanza hata Bodi ya Mbolea na Bodi zingine zinapoanza zinachukua muda kidogo, huwezi kupitisha sheria leo kesho Bodi ikaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sasa hivi uongozi wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko tayari imeshaundwa na wao wanafanya *structuring* ya Bodi yenyewe ili kuweza kukamilisha utekelezaji wa majukumu yake. Bahati nzuri tayari wamepewa *assets* za kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hawawezi kuanza kazi mpaka wapewe *seed money*. Kwa hiyo, mwaka huu Serikali imepewa bilioni 1.2 kwa ajili ya kuanza *operation* hizo zikiwa ni pamoja na manunuzi. Kwa hiyo, naamini kwamba kwa upande wake hayo matatizo ya rumbesa na balimanyaila yatapungua kwa upande wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Hifadhi ya *NMC* wamepewa watu wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Hili la *SILOS* ndogo ndogo Mikoani tulilizungumza hapa nikijibu swali kama wiki tatu zilizopita. Nilisema kwamba, ipo mikakati kama ya Mikoa nane kupewa *SILOS* ndogo ndogo za kama tani 5,000, 10,000 ili kuwa ni nafasi ya kwanza kuhifadhia chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niwasiliane na Mheshimiwa Mbunge ili nipate uhakika wa kujua kwamba katika ile awamu ya *SILOS* ya kwanza kama Kagera wamo.

Na. 270

Utekelezaji wa Sera ya Fedha ya Mwaka 2011/2012

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED aliuliza:-

Benki Kuu iliuza dhamana na hati fungani za Serikali pamoja na kuuza na kununua fedha za kigeni na kutumia mikataba ya kununua upya dhamana (*Re-purchase*

Agreements) pamoja na madirisha yake yote ya ukwasi (*BOT Liquidity Windows*) ili kutekeleza malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 20011/2012:-

(a) Je, lengo hili limesaidiaje ukuaji wa uchumi nchini?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kilitumika kutekeleza malengo ya sera hii?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji mzuri wa Sera ya Fedha katika mwaka 2011/2012 uliwezesha uwepo wa ukwasi kwa gharama nafuu (*low cost of funds*) na ulipelekea kuwa na utulivu wa uchumi (*economic stability*) ambao ulisaidia kuendelea kukua kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi. Ukuaji wa shughuli za kiuchumi umechangia kukua kwa uchumi wa jumla (*macro economy*) na kufikia asilimia 6.4 kwa mwaka 2011 ikilinganishwa na makadirio ya asilimia 6.0. Aidha, katika kipindi cha robo ya kwanza na ya pili ya mwaka 2012, uchumi uliendelea kukua kwa kasi ya asilimia 7.1 (robo ya kwanza) na asilimia 6.9 (robo ya pili) ikilinganishwa na makadirio ya mwaka ya asilimia 6.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Fedha pia ilisaidia kudhibiti mfumuko wa bei ambao kasi yake imeendelea kupungua tangu mwezi Januari, 2012, baada ya ongezeko kubwa kutokea hapa nchini katika nusu ya pili ya mwaka 2011. Hadi kufikia mwezi Agosti, 2012, mfumuko ulishuka hadi kufikia asilimia 14.9 kutoka asilimia 19.7 mwezi Januari, 2012. Mfumuko huo wa bei ulitokana na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia na bei za vyakula nchini kuwa juu kutokana na hali mbaya ya hewa katika ukanda wa Afrika Mashariki.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu ya Sera ya Fedha, Benki Kuu huingia gharama ambazo hapana budi kulipwa. Hatua zinazotumika kutekeleza sera ya fedha zinajumuisha kununua na au kuuza dhamana na hatifungani za Serikali na kununua na au kuuza fedha za kigeni. Hii inajumuisha riba ambayo hulipwa kwenye dhamana na hatifungani hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama hizi hugharamiwa na Serikali kupitia Benki Kuu. Riba hulipwa kwa wawekezaji kwenye dhamana za Serikali na hatifungani, ikiwa ni pamoja na wawekezaji kwenye mikataba ya kununua upya dhamana. Katika mwaka 2011/12, kiasi cha shilingi bilioni 64.9 kilitumika katika utekelezaji wa malengo ya sera ya fedha.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yanazua maswali mengi, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, hali halisi ya wananchi wa Tanzania bado mbaya. Nataka kujua ni vigezo gani vya kiuhalisi katika wananchi wa kawaida kwa wananchi wetu ambavyo vimetumika hata kusema kwamba uchumi umeweza kuwa *stabilized,* lakini ule mlo wa siku moja bado wananchi wetu wanaendelea kupata tabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa kuwa, matumizi haya ya sera yamesababisha mabenki na Taasisi nyingi za fedha hapa nchini kukimbilia kununua hizi *treasury bond* na vile vile kusababisha riba katika mabenki haya kupanda. Je, ni jitihada gani ambazo Wizara inazichukua ili kuhakikisha kwamba mabenki yanapunguza riba ili wananchi wa kawaida nao waweze kukopa katika mabenki hayo? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hali mbaya ya wananchi pamoja na kuwa viwango vinaonesha kuwa hali ya uchumi imeboreka hii ni kutokana na kuwa viwango vya mfumko wa bei *(inflation)* vimepungua, lakini bado kufuatana na sababu mbalimbali ambazo ni za kimfumo wenyewe hatujaweza kumfikia kila mwananchi kwa maana ya kuwa wote wananufaika moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikwazo bado vingi na changamoto bado nyingi zinahusiana na mambo ya kilimo chetu sio cha kisasa, miundombinu yetu bado haijaboreka, lakini *all in all,* bado wananchi wengi zaidi sasa hivi wananufaika na huu mfumo ambao unaendelea kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na matumizi ya hii sera ya kununua *treasury bonds*. Ni kweli kuwa pamoja na kuwa Benki Kuu inajitahidi sana kuhakikisha kuwa inasimamia mfumo wa vyombo vyetu vya kifedha vinavyokwenda, vyombo vingi vya kifedha mpaka sasa hivi bado vinakuwa na *excess liquidity* kwa sababu bado hatuna taasisi zinazoweza kukopa kwa wingi kwenye Mabenki yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa wakati wowote ule Mabenki yetu yana fedha nyingi zaidi kuliko zile ambazo wanahitaji kwa ajili ya kukopesha na kwa hali hiyo inabidi itafutwe njia gani ya kuweza kwenda kuziwekeza fedha hizi na njia ya moja kwa moja ni ya kwenye *treasury bonds*. Pamoja na hayo Benki Kuu huwa inasimamia kuwa, Benki hizi kwa kufanya hivyo zisiathiri utendaji wao wala kuleta madhara makubwa kwa Taifa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata nilishaomba radhi, sina muda kabisa. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Devota Mkuwa Likokola, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 271

Mafunzo ya Fedha (*Financial Literacy)*

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA aliuliza:-

(a) Je, lengo hilo limesaidiaje ukuaji wa uchumi nchini?

(b) Kama itakuwa tayari; je, itaanza kutoa mafunzo hayo lini, wapi na kwa namna gani?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Devota Mukuwa Likokola, Mbunge Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaweza kulijibu kwa ruhusa yako, naomba nitoe pongezi zangu kubwa sana kwa Mheshimiwa Likokola kwa jinsi ambavyo anafuatilia kwa karibu sana masuala mazima ya *VICOBA* na kuhamasisha mwenendo mzima wa jinsi gani *VICOBA* watanufaika na kuingizwa katika mfumo wa kifedha wa nchi yetu. Kwa kweli anahitaji sifa kubwa sana kwa hilo, nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi katika kujibu swali lake.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo tayari kutoa elimu ya fedha kufuatia taarifa na mapendekezo ya utafiti wa masuala ya elimu ya fedha (*financial literacy and financial education*) kutoka kwa Mshauri Mwelekezi, M/S *Marketwork Africa (Pty) Limited* aliyeteuliwa na Serikali kutoa ushauri juu ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ambayo Serikali imeanza kuyafanyia kazi kabla ya kuanza kutoa elimu ni pamoja na kuandaa Mkakati wa Elimu kuhusu masuala

yanayozungumziwa na kuunda Sekretarieti ya kuratibu na kusimamia mpango wa mafunzo (*Financial Education Secretariat*).

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali imekamilisha hatua ya kwanza ya kuandaa mfumo wa elimu ya fedha na kuuwasilisha Benki Kuu kwa ajili ya kuendelea na hatua za kuandaa Mkakati na kuunda Sekretarieti ya Elimu. Aidha, Benki Kuu imempata Mshauri Mwelekezaji atakayeandaa Mkakati na kuunda Sekretarieti ya Elimu kwa kuzingatia mahitaji *(Training Needs Assessment*) na mafunzo kwa Wawezeshaji (*Training of Trainers*) ambao ndio wahusika wakuu wa kutoa mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mkakati utakaoandaliwa na Mshauri Mwelekezi utaainisha pamoja na mambo mengine mahitaji (rasilimali watu, fedha na vifaa) muda, makundi ya wahusika, mahali na namna mafunzo yatakavyotolewa. Mshauri Mwelekezi ataanza kazi Julai, 2013 kwa mkataba wa mwaka mmoja.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya fedha itaanza kutolewa mara hatua nilizozitaja hapo juu kukamilika, gharama zake kuandaliwa na kuombewa fedha kwenye Bajeti. Kwa sasa Serikali haiwezi kutaja tarehe rasmi ya elimu au mafunzo hayo kuanza kutolewa.

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo Serikali imetoa, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa vile Serikali ina mikakati mizuri ya kutoa elimu ya fedha, ningependa kujua kwa sasa ni nani anasimamia na kutoa elimu ya fedha katika Halmashauri zetu na vijiji vyetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akaliambia Bunge hili na wananchi

kwa ujumla waende wakajifunze katika Halmashauri gani inayofanya vizuri katika kutoa elimu ya fedha kwa wananchi wake? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Devota Likokola Mama wa VICOBA. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kuwa, kwa sasa hivi bado Serikali inatayarisha mitaala pamoja na utaratibu mzima ambao elimu hii itatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Likokola pamoja na Bunge lako pamoja na wananchi kwa ujumla, kuwa hatua zilizofikiwa sasa hivi ni kuwa, watakaoshirikishwa na wadau wakuu watakuwa ni *VICOBA*, taasisi za kifedha zilizoko katika jamii, Halmashauri, Vitengo vile ambavyo vinahusika na masuala ya uwezeshaji na wadau wengine wote ambao wanaojihusisha na masuala ya mikopo na michango ya *SACCOS* ndiyo yatakayohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sasa hivi hakuna Halmashauri yoyote rasmi ambayo tunaweza tukasema inaweza ikaenda kutumiwa kama mfano, japo kuna taasisi nyingi zisizokuwa za Kiserikali, kuna Idara za Kiserikali zinazosimamia masuala ya umaskini ambazo huwa zinatoa semina mbalimbali kuhusiana na *Economic literacy*. Idara ya Forodha, Idara ya Kodi pia huwa inatoa elimu kufuatana na mahitaji yao na ya shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia niongezee tu, suala zima la elimu ya kifedha sasa hivi linataka kufanywa kuwa ni mtaala utakaoanzia tangu mashuleni na ndiyo maana taasisi hii iliyoundwa inataka kuangalia jinsi gani tangu shuleni watoto watafundishwa masuala ya *economic literacy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile hii itahakikisha kuwa, watumiaji wa huduma za kifedha

wanalindwa kutokana na mbinu za kibiashara za wanaotoa huduma hizi za kifedha kama mabenki na wengineo. Kwa hiyo, hili ndio ambalo naweza kumwahidi sasa hivi Mheshimiwa Likokola.

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, hatuna muda na nilishawaomba radhi. Tunaendelea na swali linalofuata na tumebakiza maswali mawili tuyamalize, tuingie kwenye Wizara yetu ambayo ni ya siku moja tu. Swali linalofuata linakwenda kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na litaulizwa na Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, Mbunge wa Meatu.

Na. 272

Ukamilishaji wa Gereza Meatu

MHE. MESHACK J. OPULUKWA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha Gereza la Meatu ili lianze kutumika badala ya kuendelea kutumia Gereza la Maswa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mbunge wa Meatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza kupitia Bajeti yake inajitahidi kuboresha hali ya Magereza kwa awamu kwa kuyafanyia ukarabati, kujenga Magereza mapya na kukamilisha Magereza ambayo ujenzi wake haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Meatu ni miongoni mwa Magereza ambayo ujenzi wake bado unaendelea. Kwa sasa ujenzi wa bweni moja lenye uwezo wa kuchukua wafungwa 100 pamoja na mfumo wa majitaka vimekamilika.

Lengo ni kuendelea na ujenzi wa mabweni mengine pamoja na miundombinu kama vile Ngome ya Gereza, Vyoo vya nje ya Mabweni (*Day Toilets*), Jiko, Messi ya kulia chakula na Jengo la Ofisi ya Utawala kulingana na hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukamilishaji wa Gereza la Meatu utategemea wingi wa fedha unaopatikana.

MHE. MESHACK J. OPULULWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Meatu hakuna gereza na mahabusu au watuhumiwa wengi hupelekwa kwenye gereza la Maswa na kwa kuwa inawachukua muda mrefu sana kufikishwa Mahakamani kwa ajili ya kusikilizwa mashauri yao.

Nataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri, je, anaweza akakubaliana na mimi kwamba, sasa Wizara yake ishirikiane na Wizara ya Katiba na Sheria ili kuwe na utaratibu sasa wa Mahakama kuwa inahama angalau mara moja kwa mwezi inakwenda Maswa inasikiliza yale mashauri kuweza kupunguza mlundikano wa kesi ambazo mahabusu wako kule gerezani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa hili gereza lilianza kutumika, sasa bado ni kiasi kidogo tu cha fedha ni kama sh. 60,000,000 ili kuweza kukamilisha ule uzio ambao ndio kikwazo kikubwa cha gereza hili kuanza kutumika. Je, Wizara iko tayari sasa kuangalia kwenye vifungu vyake vya fedha ili angalau kuweza kupata ile fedha sh. 60,000,00 ili iweze kupatikana kwa ajili ya kukamilisha gereza hili?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kushirikiana na Wizara ya Sheria ili pengine tutazame uwezekano wa kuhamisha vikao vya Mahakama kuja kufanyika Meatu. Hili ni suala ambalo linawezekana sana kwa sababu Wizara ya Katiba na Sheria ni mdau katika jukwaa la haki jinai. Ni wenzetu na nina hakika hili tunaweza tukalizungumza kama hakuna vikwazo *technically,* basi litafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, sh. 60,000,000. Ukweli ni kwamba, bajeti ya Wizara hii mmeshaipitisha na kwa bahati mbaya sh. 60,000,000 za gereza la Meatu hazipo. Tuna sh. 74,000,000 ya shughuli kama hizi kwa nchi nzima. Sina hakika Meatu tunaweza tukaisaidia kiasi gani, lakini tutaendelea kuhakikisha kwamba, fedha zinapatikana na zikipatikana tu Meatu na Magereza yaliyobaki yatakamilika *Inshallah*.

MWENYEKITI: Swali la mwisho kwa siku ya leo Waheshimiwa Wabunge linakwenda kwa Wizara hiyo hiyo na linaulizwa na Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi.

Na. 273

Kituo cha Polisi Itigi Kupatiwa Gari

MHE. JOHN P. LWANJI aliuliza:-

Kumekuwepo na ahadi ya muda mrefu ya kukipatia Kituo cha Polisi cha Mjini Itigi gari la doria:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya magari na vitendea kazi kwa ujumla kwa Jeshi la Polisi ni makubwa ukilinganisha na uwezo wa kifedha na bajeti ambayo ilikuwa inatolewa. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikilitatua tatizo hili kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Jeshi la Polisi lilipata magari 270 ambayo yaligawanywa katika Wilaya zote za Kipolisi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua ahadi iliyotolewa na kukipatia kituo cha Polisi cha Mjini Itigi gari la doria. Kwa hivi sasa Jeshi la Polisi Mkoa wa Singida limefanya juhudi za kukarabati gari lililopo Mkoani hapo ili liweze kutumika kituoni hapo wakati jitihada za kutafuta magari mapya kukabiliana na upungufu uliopo nchi nzima zikiendelea.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kwa kuwa shabaha na sababu ya kuomba gari kituo hicho ilikuwa ni kukabiliana na wimbi la matukio ya ujambazi katika barabara ya kutoka Itigi kwenda Tabora na pia kutoka Itigi kwenda Rungwa mpaka Chunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza, mwanzoni mwa mwaka huu tumepokea gari kituo cha Itigi, lakini gari lile limekuja likiwa bovu na hilo gari inasemekana limekarabatiwa kwa sh. 3,000,000/= wakati fundi wa kawaida akiliangalia na kulikagua anasema zinahitajika si chini ya sh. 20,000,000/=. Je, Wizara iko tayari kutoa hizo fedha kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa hilo gari ili liweze kufanya kazi? Au lah, tupate gari lingine kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kutoka Itigi kwenda Mitundu ni takribani kilomita 60, kuna kituo kingine cha Polisi. Lakini kituo hicho hakina usafiri, hakina gari, ni juzi tu tulipata pikipiki moja, lakini kazi kubwa inayotakiwa katika eneo hilo ambalo kuna mapori makubwa ni doria ili kukabiliana na majambazi hayo. Je, Wizara iko tayari kutoa gari kwa kituo hicho?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi kabisa.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze kwa sababu nimemwona amelifuatilia sana suala hili, si hapa tu lakini hata ofisini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, gari limeshatengwa kwa ajili ya kituo cha Polisi na suala la ukarabati ni suala la kazi ya Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, kama itagharimu sh. 3,000,000 au 5,000,000 tayari Polisi imeshaamua kulitengeneza ili litumike kwa kituo hicho. Kwa hiyo, tutajitahidi kuhakikisha kwamba, gari hilo linatembea na linafanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa sababu hili gari tumeahidi kulitengeneza, pikipiki itakuwa ni ziada, lakini gari hili litapatikana. Naomba niwajulishe Wajumbe kwamba, tuna jitihada kubwa sana ambazo zinatia matumaini kwamba, si wakati mrefu tutaweza kupata magari mengi kwa nchi nzima. Kwa hiyo, tusubiri, uvumilivu ni mgumu, lakini mzuri na tutafanikiwa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge matangazo yafuatayo yameletwa kwenye meza ya Spika.

Tangazo la kwanza Mheshimiwa Idd Azzan anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kesho tarehe 25 Jumamosi kutakuwa na mazoezi ya viungo kwa wanamichezo wote yatakayoambatana na muziki. Mazoezi hayo yataanza saa 12.00 asubuhi katika uwanja wa Jamhuri Dodoma.

Hivyo Wabunge wote mnatakiwa kuhudhuria mazoezi hayo maalum kabisa yatakayokuwa yakiongozwa na muziki. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge haya ni mazoezi ya aina yake kabisa, nafikiri labda tujitahidi kuwepo tuone inakuwaje.

Mheshimiwa Mama Anna Margareth Abdallah, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake wa Tanzania *(TWPG)* ameniomba niwatangazie Wabunge Wanawake

wote kuwa leo tarehe 24 saa 7.15 mchana kutakuwa na semina itakayofanyika ukumbi wa Pius Msekwa. Ni Wabunge Wanawake tu wanachama wa *(TWPG)*.

WABUNGE FULANI: Mnatubagua!

MWENYEKITI: Hatubagui, nadhani ndio utaratibu. Tunawahamasisha na Wabunge Wanaume waanzishe chama chao.

Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa James Lembeli Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuwa, tarehe 24 saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo kitakachofanyika katika Ukumbi Na. 231, Jengo la Utawala. Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo mhudhurie bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na yeye ameniomba niwatangazie Wabunge wote Wajumbe wa Kamati hiyo, kuwa leo tarehe 24, saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kitakachofanyika katika ukumbi Na. 133, ghorofa ya kwanza, Jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho, linatoka kwa Mheshimiwa Said Nkumba, Mwenyekiti wa Klabu ya Kulenga Shabaha. Mheshimiwa Nkumba anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe waliojiorodhesha kwenda kulenga shabaha, kuwa zoezi hilo litafanyika siku ya Jumapili tarehe 26 kuanzia saa 4.00 asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge waliojiorodhesha kwa zoezi hili wanatakiwa kufika Ofisi ya Bunge saa 3.30 asubuhi usafiri utakuwepo kwa ajili ya kuwapeleka Makutupora. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, nadhani zoezi hilo pia ni muhimu basi Mheshimiwa Said Nkumba anawaalika kushiriki zoezi hilo Makutupora siku ya Jumapili.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tunaendelea na ratiba.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), kuhusu jambo ambalo limetokea mapema leo na mapema jana. Leo tumekabidhiwa orodha ya shughuli za Bunge ambayo inaonesha hoja ya leo, ni Hoja ya Serikali ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kipindi cha maswali na wakati majibu yanatolewa kuna kauli ambayo ilitoka kwamba, Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini inaendelea kesho. Sasa jana wakati suala hili la kujadili Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini inaahirishwa hakuna hoja yoyote ambayo imetolewa na Serikali kwa mujibu wa Kanuni ya 66(1) ambayo inasema kwamba, kama mjadala wa hoja iliyoko mezani inabidi uahirishwe, lazima kutolewe hoja ambayo itaeleza mjadala unaahirishwa mpaka wakati gani na pia ikieleza sababu za kuahirishwa kwa mjadala huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mwongozo wako ili Serikali sasa itakiwe kufuata Kanuni, kutoa hoja ya kuahirisha mjadala mpaka hiyo siku iliyopangwa. Nitoe tahadhari tu kwamba, hiyo siku Serikali itakapotoa hoja hiyo ituhakikishie Wabunge kwamba, muda utakaotengwa kujadili Wizara hii utakuwa wa kutosha kwa sababu tayari kuna mambo mengi yanaendelea nyuma ya pazia yanayohitaji muda wa kutosha ikiwemo mauaji ya wananchi wa Mtwara ambayo yanaendelea hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika unawahisha shughuli za Bunge kabla ya wakati. Shughuli zozote kama ulivyosema zitafuata Kanuni na kwa kuwa wewe umesema umesikia, lakini si kwamba ndiyo taarifa rasmi ya meza; kwa hiyo, uwe mpole subiri utaratibu utatengenezwa.

Kwa hiyo, kwa utaratibu wa Kikanuni pia na wewe usiwahishe shughuli kabla ya wakati. Kwa hiyo, wakati utakapofika hayo yote unayoyasema ya Kikanuni ili yaweze kutekelezwa, yatafanyiwa utekelezaji kwa sababu vikao vyote na ratiba ya Bunge inapangwa kwa taratibu. Kwa hiyo, wewe subiri, taratibu zote zinatengenezwa, Kanuni zitafuatwa na mambo yote yatakwenda kwa kuzingatia. Usiwahishe shughuli za kikanuni kabla ya wakati wake. Katibu tuendelee.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014 – Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasoma hotuba yangu nataka kueleza tu kwamba pamoja na hotuba yenyewe kutakuwa na viambatanisho vitatu. Hotuba kwa lugha ya Kingereza kwa muhtasari, mkakati wa mawasiliano kwa lugha ya Kiingereza na jariba. Vitu hivi vinne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, sikutaka kuliweka hili kwenye hotuba kwa sababu ya mahusiano yetu na nchi jirani. Katika toleo moja la gazeti la *Sunday Nation,* mchora katuni alionesha picha ya Bunge hili kukiwa na chupa za ulevi, kukiwa na watu wamevaa hovyohovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali na kwa niaba ya Bunge hili, nasema kwamba, kitendo hiki kilikuwa si cha kijirani mwema wala si urafiki, ni kitendo cha kihuni, kinaweza kuchochea maelewano mabaya. Kwa hiyo, tunalaani kwa nguvu zote jitihada zozote za watu ambao wanajaribu kukashfu Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mara nyingine Bunge letu linakuwa na mjadala mkali, lakini kulinganisha sisi

Wabunge na ulevi na nguo nusu uchi na kadhalika, hata kama ni namna ya tu mchoro na kujaribu kuchekesha, hii haikubaliki kabisa. Tunaipenda nchi yetu, tunalipenda Bunge letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa iliyowasilishwa hapa Bungeni, kuhusu Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Edward Ngoyayi Lowassa, kwa kupokea, kujadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2013/2014. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu imezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Jumuiya ya Afrika Mashariki imekumbwa na simanzi kubwa kufuatia vifo vya Mheshimiwa Eriya Kategaya, aliyekuwa Naibu wa Kwanza wa Waziri Mkuu na Waziri wa Afrika Mashariki wa Jamhuri ya Uganda pamoja na Bwana David S. Nalo, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afrika Mashariki nchini Kenya. Tunawapa pole wafiwa na tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Uchaguzi Mkuu wenye mafanikio tunaipongeza Serikali na wananchi wa Kenya kwa kukamilisha zoezi hilo kwa uwazi, demokrasia na amani. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Uhuru Kenyatta kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Nne wa Jamhuri ya Kenya na Mheshimiwa William Ruto kuwa Naibu Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niwasaidie hasa waandishi wa habari wanaandika Makamu wa Rais, wao hawana Makamu wa Rais wana Naibu Rais *(Deputy President)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti,vile vile, nampongeza Mheshimiwa Phyllis Chipkosgey Kandie kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Afrika Mashariki kutoka Kenya. Ni matumaini yangu kuwa kama ilivyokuwa kwa Waziri aliyemtangulia, Mheshimiwa Kandie ataendeleza ushirikiano mzuri katika kazi za mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maandalizi ya hotuba hii, Wizara imezingatia maudhui ya Hotuba kwa mwaka 2013/2014 aliyoitoa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Bunge lako Tukufu. Aidha, Hotuba yangu imezingatia Taarifa ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2012, iliyotolewa na Mheshimiwa Stephen Masatu Wassira, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu. Hotuba zao nzuri zimeweka mwelekeo wa shughuli za Serikali na Dira ya Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nautambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Abdulla J. Saadalla, Naibu Waziri; Dkt. Stergomena L. Tax, Katibu Mkuu; Ndugu Uledi A. Mussa, Naibu Katibu Mkuu; Wakuu wa Idara na Vitengo; pamoja na Watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaonipa. Nawapongeza sana kwa kuitikia kwa vitendo wito wangu wa kazi kwa viwango, kasi, uadilifu na uzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha Hotuba hii kwa umakini na ndani ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa malengo na mipango ya mwaka 2012/2013. Malengo na

Mipango ya mwaka 2012/2013. Katika mwaka 2012/2013, Wizara ilipanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake;

(ii) Kukamilisha mchakato wa Serikali kuidhinisha Sera ya Taifa ya Mtangamano ili ianze kutekelezwa;

(iii) Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Wizara 2010/11 – 2012/13;

(iv) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja;

(v) Kutoa Elimu kwa Umma ili kuwawezesha wadau mbalimbali kuzifahamu na kuzitumia fursa zitokanazo na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(vi) Kukamilisha zoezi la kuwianisha Sheria, Kanuni na Taratibu ili Sheria za Taifa ziendane na matakwa ya Itifaki ya Soko la Pamoja;

(vii) Kuratibu na kuongoza ushiriki wa Tanzania katika majadiliano ya ushirikiano katika Utatu wa *COMESA-EAC-SADC*;

(viii) Kuratibu na kuongoza ushiriki wa Tanzania katika majadiliano ya kuandaa Itifaki ya Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki;

(ix) Kuratibu na kuongoza ushiriki wa Tanzania katika majadiliano ya kuandaa mfumo wa utekelezaji wa Himaya Moja ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(x) Kushiriki na kuongoza ushiriki wa Tanzania katika kuhakiki utayari wa Jamhuri ya Sudan Kusini kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(xi) Kuratibu utekelezaji wa Mitandao ya Uendelezaji wa Miundombinu ya Kiuchumi ya Jumuiya (Barabara, Reli, Bandari, Viwanja vya Ndege, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Mpango wa Uzalishaji na Usambazaji Nishati);

(xii) Kuratibu utekelezaji wa Programu za Kisekta, katika sekta za uzalishaji na huduma za jamii;

(xiii) Kuratibu maandalizi ya Itifaki na sheria mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Itifaki ya Amani na Usalama; Itifaki ya Utawala Bora; Itifaki ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Itifaki ya Ulinzi;

(xiv) Kukamilisha maandalizi ya Mkataba wa Mfuko wa Maendeleo wa Afrika Mashariki *(East African Development Fund)*; Mfumo wa Sheria wa Vituo vya Pamoja Mipakani; Sheria ya Kuwianisha na Kudhibiti Uzito wa Magari na Itifaki na Sheria ya Viwango;

(xv) Kuratibu utekelezaji wa Sera na Mikakati mbalimbali ya Jumuiya ikiwa ni pamoja na Sera ya Uendelezaji Viwanda, Sera ya Usalama wa Chakula na Mpango-Kazi wa Kupambana na Mabadiliko ya Tabianchi, Mpango wa Kuondoa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha;

(xvi) Kufanya chambuzi ili kuandaa msimamo unaozingatia maoni ya wananchi katika kuandaa Modeli na Mfumo wa Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki;

(xvii) Kujenga uwezo wa Wizara kiutendaji ili kuwa Kitovu cha Mawazo *(Think Tank)* katika masuala ya mtangamano na kufanya tathmini na chambuzi za kina kwa kushirikisha wadau kutoka sekta mbalimbali ili kuwezesha kujenga hoja na misimamo yenye kuzingatia maslahi ya Taifa na Jumuiya katika majadiliano ya hatua mbalimbali za mtangamano; na

(xviii) Kuhakikisha mchango wa Tanzania katika Jumuiya, unalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika mwaka 2012/2013 ulizingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Malengo ya Milenia; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA II); Mpango wa Utekelezaji wa Kilimo Kwanza; Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016) na Mpango Mkakati wa Wizara (2010/2011 – 2012/2013).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara imezingatia Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake; Maagizo ya Viongozi Wakuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; Maagizo ya Baraza la Mawaziri la Jumuiya na Mkakati wa Nne wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 2011/2012 -2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Wizara ilitengewa jumla ya Sh. 16,643,667,000. Kati ya fedha hizo, Sh. 1,378,292,000 ni kwa ajili ya Mishahara na kiasi cha Sh. 15,265,375,000 ni Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, mchango wa Tanzania katika Jumuiya ulikuwa Sh. 8,841,573,000 na sh. 6,423,802,000 kwa matumizi mengine ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara iliongezewa kiasi cha sh. 2,000,000,000 ili kuziba upungufu wa mchango katika Jumuiya. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2013, Wizara ilikwishapokea kiasi cha Sh. 16,755,885,800 ikiwa ni sawa na asilimia tisini (90%) ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa malengo na mipango, Sera na Mikakati, Sera ya Taifa ya Mtangamano; ili kukamilisha Sera inayozingatia mahitaji mtambuka ya mtangamano, Serikali iliunda Timu ya Wataalam inayojumuisha Wizara za Kisekta chini ya uratibu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa lengo la kupitia rasimu iliyoandaliwa na kuikamilisha ili ianze kusambazwa katika mwaka ujao wa fedha, 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango Mkakati wa Wizara; Wizara imekamilisha mapitio ya Mpango Mkakati wake wa pili unaoishia mwaka 2012/2013. Aidha, Wizara imekamilisha kuandaa Mpango Mkakati wa Tatu kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 – 2017/2018. Pamoja na Dira na Dhima ya Wizara, Mpango Mkakati huu unabainisha Malengo ya kimkakati ya Wizara kwa kipindi cha miaka mitano (2013/2014 – 2017/2018) na Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Soko la Pamoja; Mkakati wa Taifa wa Utekelezaji wa Soko la Pamoja unatarajiwa hivi karibuni kuidhinishwa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji. Mkakati huo unaogusa sekta nyingi utatekelezwa kwa kushirikiana na Wizara husika za Kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara; Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara ulizinduliwa rasmi mwezi Februari, 2013. Mkakati huu unalenga kutoa mwongozo wa utoaji Elimu kwa Umma kuhusu mtangamano wa Afrika Mashariki kwa makundi mbalimbali na pia kama nyenzo ya kupata mrejesho kutoka kwa wadau. Mkakati umeainisha njia mbalimbali za kutoa Elimu kwa Umma, ikiwa ni pamoja na mikutano ya ndani na hadhara, semina, vipindi vya luninga na redio, vipeperushi pamoja na machapisho, magazeti, na ujumbe mfupi wa simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Takwimu za Hali ya Hewa ya Jumuiya; katika kuhakikisha kuwa Nchi Wanachama zinakuwa na takwimu sahihi za Hali ya Hewa, katika mwaka 2012/2013, Wizara ilishiriki na kuratibu maandalizi ya Sera ya Takwimu za Hali ya Hewa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sera hii iliidhinishwa na Baraza la Mawaziri la Jumuiya mwezi Agosti, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera hii inatoa mwongozo wa namna ya kukusanya, kuchambua, kusambaza, kuhifadhi na kubadilishana takwimu za hali ya hewa miongoni mwa Nchi Wanachama. Hatua hii itaimarisha utabiri wa hali ya

hewa katika Kanda hii na pia kutumika kama nyenzo katika mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Matumizi ya Maji katika Ziwa Victoria; Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki, katika Mkutano wake wa 26 uliofanyika mwezi Novemba, 2012, lilipitisha Sera Mpya ya Matumizi ya Maji katika Ziwa Victoria *(New Water Release and Abstraction Policy for Lake Victoria)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Sera hii ni kutoa mwongozo wa matumizi endelevu ya rasilimali ya maji ya Ziwa Victoria kwa Nchi Wanachama. Tunatarajia kuwa utekelezaji wa Sera hii utapunguza kasi ya kushuka kwa kina cha maji katika Ziwa Victoria na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa hatua za matangamano; Ibara ya 5(2) ya Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki imeainisha hatua nne za Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hatua hizo ni: Umoja wa Forodha; ikifuatiwa na Soko la Pamoja; kisha Umoja wa Fedha na hatimaye Shirikisho la Kisiasa. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja na majadiliano ya Umoja wa Fedha na Shirikisho la Kisiasa.

Mhesh
imiwa Mwenyekiti, Umoja wa Forodha; Kifungu cha 49(c) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, kinaitaka Serikali kujenga mifumo imara ya viwanda, biashara na masoko yenye kuendeleza na kukuza mauzo ya nje ikiwemo Soko la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Umoja wa Forodha umeendelea kuwa na mafanikio katika kukuza biashara ya mauzo ya bidhaa miongoni mwa Nchi Wanachama na hivyo kuongeza ajira, kuongeza uwekezaji na kukuza sekta za uzalishaji nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kubainisha hoja hii, Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, wakati akihutubia Bunge la Afrika Mashariki, tarehe 27 Novemba 2012 alieleza na nanukuu:

"The Customs Union has had a positive impact on economies of Partner States contrary to the original fears that it could be otherwise" Yaani, Umoja wa Forodha umekuwa na matokeo chanya katika uchumi wa Nchi Wanachama tofauti na hofu zilizokuwepo hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo na manunuzi ya Tanzania katika Soko la Jumuiya; thamani ya mauzo ya Tanzania katika soko la Jumuiya imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Katika kipindi cha mwaka 2011 mauzo yaliongezeka hadi kufikia Dola za Marekani milioni 409, kutoka Dola za Kimarekani milioni 394.30 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 3.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, takwimu za awali za mwaka 2012, zinaonesha kuwa mauzo ya Tanzania katika Jumuiya yameongezeka na kufikia Dola za Kimarekani milioni 613.30, sawa na ongezeko la asilimia 49.95. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa mauzo ya mazao ya kilimo na mbolea katika Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Kenya imeendelea kuwa soko kuu la bidhaa za Tanzania ikiwa inachukua asilimia 57.02 ya mauzo yote ya bidhaa za Tanzania ndani ya Jumuiya. Bidhaa za Tanzania zilizouzwa nchini Kenya kwa wingi ni pamoja na vyandarua, bidhaa za plastiki, chai, transfoma, karatasi na bidhaa za karatasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa nyingine zilizouzwa katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni mbolea, saruji, nafaka, matunda, chuma, samaki, ngano, sukari na nguo.

Grafu Na. 1 hapa chini inaonesha mwenendo wa mauzo ya Nchi Wanachama.



Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011 jumla ya biashara ya bidhaa miongoni mwa Nchi Wanachama iliongezeka hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 4,486 toka Dola za Kimarekani milioni 3,732 mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za awali za mwaka 2012, biashara ya bidhaa miongoni mwa Nchi Wanachama iliongezeka na kufikia Dola za Kimarekani milioni 5,472.90 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 4,486 mwaka 2011. Ongezeko hili ni asilimia 22 ikilinganishwa na asilimia 20.49 mwaka 2011.

Grafu Na. 2 hapa chini inaonesha biashara ya bidhaa baina ya Nchi Wanachama.



Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Kenya imeendelea kuongoza katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuwa na mgao mkubwa zaidi wa soko *(market share)* ikifuatiwa na Tanzania, Uganda, Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za awali, mgao wa soko la Tanzania katika Jumuiya umeendelea kuongeza kutoka asilimia 18 mwaka 2010 na kufikia asilimia 24 mwaka 2012.

Tufe Namba 1 hapa chini linaonesha mgao wa Soko miongoni mwa Nchi Wanachama katika mwaka 2012.



Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011, thamani ya manunuzi ya bidhaa kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ilipanda kwa asilimia 27.78, kutoka Dola za Kimarekani milioni 295.9 mwaka 2010 hadi kufikia Dola millioni 378.1 mwaka 2011. Takwimu za awali za mwaka 2012 zinaonesha manunuzi yamepanda na kufikia Dola za Kimarekani milioni 678.60, ikiwa ni ongezeko la asilimia 79.48 ikilinganishwa na mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili la manunuzi limechangiwa na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa kutoka Uganda. Bidhaa zilizoagizwa kutoka Uganda ni pamoja na vifaa vya umeme, viatu, karatasi, mafuta ya kula na sabuni.

Mshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeendelea kununua bidhaa nyingi kutoka Kenya ikilinganishwa na nchi nyingine

za Jumuiya. Kwa mwaka 2012, bidhaa kutoka Kenya zinachukua wastani wa asilimia 83.15 ya thamani ya manunuzi yote ya Tanzania kutoka ndani ya Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa zilizoagizwa kutoka Kenya ni pamoja na madawa ya binadamu na yamifugo, chuma na bidhaa za chuma, mafuta, magari ya mizigo na matela ya mizigo.

Grafu Na. 3 hapa chini inaonesha manunuzi baina ya Nchi Wanachama.



Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwekezaji; utekelezaji wa Umoja wa Forodha umeendelea kuchangia katika jitihada za Serikali za kuvutia na kukuza uwekezaji. Idadi na thamani

ya miradi inayowekezwa Tanzania na wawekezaji kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012, miradi mipya 27 iliwekezwa ikiwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 100.3. Katika mwaka 2012, sekta zilizoongoza nchini katika uwekezaji kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni ujenzi, utalii, usafirishaji na usindikaji viwandani. Hali hii inaonesha kuwa sekta za viwanda na ujenzi zinaendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha kutokana na utekelezaji wa Umoja wa Forodha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la uwekezaji baina ya Nchi Wanachama, limesababisha ajira kuongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2012, ajira mpya zilikuwa 1,774. Sekta zilizoongoza katika kukuza ajira ni pamoja na uzalishaji viwandani, ujenzi, usafirishaji, biashara ya huduma na utalii.

Mchanganuo kamili ni kama inavyoonekana katika Tufe Na. 2.



Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni za Uasili wa Bidhaa. Katika mwaka 2012/2013, Nchi Wanachama ziliendelea kufanya mapitio na kuandaa rasimu ya marekebisho ya Kanuni za Uasili wa Bidhaa za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho hayo ni kufanya Kanuni za Uasilia wa Bidhaa ziendane na mabadiliko ya kiuchumi na kiteknolojia na hivyo kurahisisha uendeshaji wa biashara ya bidhaa miongoni mwa Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho yaliyofanyika, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kuondoka kwenye mfumo wa sheria ya uasili wa bidhaa wenye vigezo vya jumla kwa bidhaa zote na kwenda kwenye mfumo wa sheria wenye vigezo mahsusi kwa kila bidhaa *(product specific criteria)* kutegemeana na hatua ya usindikaji iliyofikiwa katika bidhaa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko haya yamezingatia uwezo wa kiuchumi na kiteknolojia wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuweza kufikia vigezo vinavyopendekezwa. Lengo likiwa ni kuhimiza matumizi ya malighafi ya ndani na kuhamasisha ukuzaji wa teknolojia. Zoezi hili linaendelea na linatarajiwa kukamilika katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa mabadiliko yanayopendekezwa katika kanuni za utambuzi wa uasili wa bidhaa ni makubwa, Nchi Wanachama zinaendelea kutoa elimu kwa wadau wa sekta ya umma na binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la zoezi hili ni kuhakikisha kunakuwepo na uelewa wa pamoja baina ya watendaji na watumiaji wa vigezo hivyo kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Himaya Moja ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wizara kwa kushirikiana na Nchi Wanachama zimeendelea kuandaa Taratibu za Uendeshaji wa Mfumo wa Himaya Moja ya Forodha ulioidhinishwa na Wakuu wa Nchi Wanachama. Mfumo huo unatoa fursa kwa kila nchi kukusanya ushuru wa bidhaa zinazotua *(Destination Model).* Aidha, kwa bidhaa zinazopitia nchi moja kwenda nchi nyingine *(transit goods*), ukaguzi na ukusanyaji wa mapato utafanyika katika kituo cha kwanza bidhaa zinapoingia katika Jumuiya na mapato kuwasilishwa kwa nchi husika baada ya kuthibitishwa kuwa bidhaa zimevuka mpaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kutekeleza mfumo huu, nchi Wanachama zimebainisha Mihimili Mitatu ya Himaya Moja ya Forodha. Mihimili hiyo ni: Mzunguko Huru wa Bidhaa, Usimamizi wa Mapato na Mfumo wa Kisheria na Kiutawala. Nchi Wanachama zinaendelea kujadiliana ili kukamilisha taratibu za uendeshaji za mfumo huu unaozingatia mihimili hii. Inatarajiwa kuwa Mfumo huo utakamilika kufikia mwezi Novemba, 2013. Kukamilika kwa mfumo huo kutaimarisha utekelezaji wa Umoja wa Forodha na kuweka msingi imara wa utekelezaji wa Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vikwazo Visivyo vya Kiforodha. Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika utekelezaji wa Mpango Maalum wa Kikanda wa kushughulikia Vikwazo Visivyo vya Kiforodha. Katika mwaka 2012/2013, kati ya vikwazo 35 vilivyobainishwa, 30 viliweza kuondolewa. Miongoni mwa vikwazo vilivyoondolewa ni pamoja na ushuru wa kuegesha magari ya mizigo, ushuru wa mazao katika maua na mbogamboga na ushuru wa kupitisha mizigo. Aidha, changamoto ya biashara ya magendo ya Karafuu kutoka Zanzibar imeondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na jitihada za Jumuiya za kuondoa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha, katika mwaka 2012/2013, vikwazo vipya vimejitokeza. Vikwazo hivyo ni pamoja na kutofautiana kwa

viwango vya uzito wa magari vinavyoruhusiwa katika nchi Wanachama, Dhamana ya Fedha Taslimu *(Cash Bond),* Kodi ya asilimia 75 kwa mchele wa Kenya uingiapo Uganda, Sheria ngumu kwa biashara ya chakula na dawa, Mamlaka za Mapato kudai nyaraka halisi wakati wa kutoa mizigo bandarini, kuzuiwa kwa matunda kutoka Burundi kuingia Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Pamoja. Katika kipindi cha 2012/2013, Wizara imeendelea kuongoza na kuratibu Kamati za Kitaifa na Kikanda za Kusimamia na Kufuatilia Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja. Utaratibu huu unaziwezesha nchi Wanachama kufuatilia na kutoa taarifa za utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa katika Itifaki ya Soko la Pamoja na kutatua changamoto za utekelezaji. Kwa jumla utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja unakwenda taratibu kutokana na kuchelewa kukamilika kwa zoezi la kurekebisha sheria za ndani za Nchi Wanachama ili ziendane na matakwa ya Itifaki. Hali hii imesababisha Nchi Wanachama kutoweza kuzitumia fursa za Soko la Pamoja ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kubainisha Sheria zinazohitaji kufanyiwa marekebisho. Hatua zilizofikiwa ni kama ifuatavyo:-

(a) Sheria ya Makampuni (Sura 212) iliyopendekeza kuanzisha *Limited Liability Single Shareholder,* utekelezaji umefanyika kupitia Sheria ya Marekebisho ya Biashara Na. 3 ya 2012;

(b) Sheria ya Uhamiaji Na. 7/1995 na Kanuni zake za mwaka 1997 ambapo Idara ya Uhamiaji imebainisha vipengele vinavyohitaji marekebisho. Aidha, mchakato wa kutunga Sheria mpya ya Uhamiaji unaendelea na utakamilika baada ya kupata maoni kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; na

(c) Marekebisho ya Kanuni za Fedha za Kigeni ya

mwaka 1998, Kanuni ya Dhamana za Fedha za Kigeni ya mwaka 2003, Waraka wa Fedha za Kigeni wa mwaka 1998 na Mabadiliko ya Sheria ya Mitaji na Dhamana kwa Wawekezaji wa Kimataifa ya mwaka 2003 yapo katika hatua za mwisho. Inatarajiwa mabadiliko ya Sheria hizi za fedha na mitaji yatatangazwa kupitia Gazeti la Serikali katika kipindi cha mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kikosi Kazi kinaendelea kuzipitia sheria zinazosimamia biashara ya huduma ili kuhakikisha kuwa sheria za Tanzania hazikinzani na Itifaki ya Soko la Pamoja katika eneo hili. Katika mwaka 2012/2013, Sheria zilizopitiwa ni zile zinazosimamia Wahandisi, Wakunga na Wauguzi. Mapendekezo ya Kikosi Kazi yatawasilishwa kwenye Wizara husika ili ziweze kuendelea na mchakato wa kuandaa Miswada ya marekebisho ya sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Fedha. Katika kipindi cha 2012/2013, Wizara imeendelea kuratibu na kuongoza ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika majadiliano ya Itifaki ya Uanzishwaji wa Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Majadiliano yapo katika hatua za mwisho, ambapo pamoja na kupitia vipengele vyote vya rasimu ya Itifaki, Nchi Wanachama zimeandaa Rasimu ya Mpangokazi wa kuelekea katika Umoja wa Fedha. Kwa mujibu wa Mpangokazi huo, masuala ya msingi yatakamilika katika kipindi cha miaka kumi baada ya kukamilika kwa Itifaki. Mpango huo unalenga kuhakikisha kuwa misingi ya kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Fedha inakamilika kabla ya kuanza utekelezaji wa Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya msingi yaliyoainishwa katika Mpangokazi huo ni pamoja na kukamilisha hatua za awali za mtangamano za Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja; na kuwianisha sera na sheria mbalimbali ili kufikia vigezo vya muunganiko wa uchumi mpana wa Nchi Wanachama na kuanzisha Taasisi muhimu za kusimamia utekelezaji wa Umoja wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi wanachama zimekubaliana kuwa vigezo vya muunganiko wa uchumi mpana *(Macro - Economic Convergence)* vitumike kupima utayari wa Nchi Wanachama kujiunga na Umoja wa Fedha na kufuatilia mwenendo wa utekelezaji wake. Vigezo vinavyopendekezwa ni:-

(a) Kiwango cha juu cha mfumuko wa bei kisichozidi asilimia nane (8%);

(b) Kiwango cha juu cha nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada kisichozidi asilimia tatu (3%) ya Pato la Taifa;

(c) Kiwango cha juu cha deni la Taifa kisichozidi asilimia 50 ya Pato la Taifa; na

(d) Akiba ya fedha za kigeni ya kutoshelezea mahitaji ya miezi minne na nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatarajiwa kuwa majadiliano yatakamilika ifikapo mwezi Agosti, 2013 na Itifaki kutiwa sahihi mwezi Novemba, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirikisho la Kisiasa. Katika hotuba yangu ya mwaka 2012/2013, nilijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya waliiagiza Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuandaa mapendekezo ya Muundo na Modeli ya Mfumo wa Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki; Mpangokazi wa Kutekeleza Mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa ya Wataalam ya kutatua kero, hofu na changamoto za kuanzisha Shirikisho la Kisiasa; na Mpangokazi wa Uanzishaji na Uimarishaji wa Taasisi muhimu katika utekelezaji wa hatua za awali za mtangamano, hususan Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja na Umoja wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wao wa 14 uliofanyika mwezi Novemba 2012, Ngurutodo, Arusha, Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama walipokea rasimu ya

mapendekezo ya Muundo na Modeli ya Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki iliyoandaliwa na Sekretarieti ya Jumuiya na kuagiza kuwa Rasimu hiyo iwasilishwe kwa Nchi Wanachama kwa ajili ya kuitolea maoni. Zoezi la kukusanya maoni linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na wadau kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, itaendelea kufanya uchambuzi wa Wasimu ya Mapendekezo ya Muundo na Modeli ya Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Wadau hao ni pamoja na Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wanasiasa, Makundi Maalum ya Kijamii, wataalam na wananchi kwa jumla. Zoezi hili litaiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuandaa maoni na msimamo wa kitaifa kuhusu suala hili la Shirikisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano na Kanda nyingine za Kiuchumi. Utatu wa Jumuiya za *COMESA-EAC-SADC*. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuratibu, kushiriki na kuongoza majadiliano ya Utatu *COMESA - EAC –SADC,* ikiwemo majadiliano ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara. Nchi Wanachama zimefikia muafaka kuhusu misingi itakayoongoza majadiliano ya Eneo Huru la Biashara. Misingi hiyo ni:-

(a) Kufungua Soko la bidhaa kwa asilimia 100, isipokuwa bidhaa zilizozuiliwa au zenye utaratibu maalum katika mikataba ya kikanda na kimataifa;

(b) Kufungua soko la bidhaa kwa asilimia 60 hadi 85 katika mwaka wa kwanza baada ya mkataba wa eneo huru la biashara kupata nguvu ya kisheria; na

(c) Kufungua kiasi kilichosalia katika kipindi cha miaka mitano hadi minane ili kukamilisha ratiba ya ufunguaji wa soko la bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Nchi Wanachama zinaendelea na uchambuzi wa Kitaifa na

Kikanda kuhusu taratibu na maeneo yatakayofunguliwa katika majadiliano hayo ya Utatu yanayotarajiwa kuanza rasmi mwezi Juni, 2013 na kukamilika ifikapo mwezi Aprili, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi baina ya Jumuia ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya ambapo kumekuwa na mafanikio. Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya zimeweza kufikia muafaka katika maeneo kadhaa ikiwa ni pamoja na eneo la ushirikiano wa kiuchumi na maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili, pande zote mbili zimekubaliana kuwa Umoja wa Ulaya utatoa fedha zitakazochangia kuziba pengo katika kutekeleza miradi inayolenga kutatua changamoto za uendelezaji wa miundombinu ya kiuchumi, usafirishaji, na huduma za masoko. Utekelezaji wa miradi hii utaziwezesha Nchi Wanachama kujenga na kuimarisha uwezo na hivyo kuziwezesha Nchi Wanachama kuzitumia na kunufaika na fursa za kimasoko zitokanazo na ubia huu. Miradi husika imeainishwa kwenye Jedwali la Miradi ya Maendeleo ya ushirikiano huu ambalo litakuwa sehemu ya Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Ulaya. Miradi hiyo inalenga kuzisaidia Nchi za Jumuiya kukabiliana na changamoto za kiuzalishaji na usambazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha uwajibikaji kwa pande zote mbili na kurahisha utekelezaji, imekubalika kuwa kuwepo kipengele katika mkataba, kinachozitaka Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuingiza vipaumbele vilivyoainishwa katika Jedwali la Miradi ya Maendeleo ya *EPA* katika mikakati na mipango ya Kikanda na Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano wa Sekta ya Uzalishaji. Kilimo na Usalama wa Chakula. Wizara, kwa

kushirikiana na Wizara za Kisekta, imekamilisha maandalizi ya Sera ya Mifugo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lengo la Sera hii ni kutoa mwongozo wa uendelezaji wa sekta ya mifugo unaozingatia matumizi bora na endelevu ya ardhi na mazingira. Sera hii itaanza kutumika rasmi baada ya kuridhiwa na Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maliasili na Mazingira; katika mwaka 2012/2013, Wizara iliratibu na kushiriki katika majadiliano ya kuandaa mfumo wa uendeshaji wa Mfuko wa Jumuiya wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya Tabianchi. Mfumo wa uendeshaji wa mfuko huo unaainisha Mfumo wa Kitaasisi na Usimamizi. Majadiliano yanatarajiwa kukamilika katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii na wanyamapori; katika mwaka 2012/2013, zoezi la kupanga hoteli katika madaraja kwa Mkoa wa Manyara limekamilika. Zoezi hili litaendelea katika Mkoa wa Arusha mwaka 2013/2014. Inatarajiwa kwamba zoezi la kutoa viwango hivi litaboresha utoaji huduma za hoteli na utalii na hivyo kuchangia katika kukuza sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa miundombinu ya kiuchumi. Ujenzi na uimarishaji wa miundombinu ya uchukuzi hususan, bandari; mitandao ya reli; viwanja vya ndege; na usafiri wa majini, anga na barabara; ni miongoni mwa vipaumbele vya Tanzania katika Jumuiya. Uendelezaji huu wa miundombinu utaiwezesha Tanzania kutumia nafasi yake ya kijiografia na kunufaika. Katika kutekeleza azma hii, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Miradi ya Kitaifa iliyoainishwa katika Mipango ya Kikanda ya Uendelezaji wa Miundombinu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao wa barabara. Katika mwaka 2012/2013, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeendelea kutekeleza mradi ulioidhinishwa katika Mtandao wa Barabara katika Jumuiya *(The East African Road Network Project).* Mtandao huo unajumuisha barabara

za kitaifa zenye umuhimu wa kikanda ambazo zinaunganisha nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao wa reli. Katika Hotuba yangu ya mwaka 2012/2013 nilizungumzia kuhusu kuanza kwa usanifu wa kina wa uendelezaji wa reli ya Isaka - Kigali/Keza hadi Musongati ili kuiunganisha Tanzania na Nchi za Rwanda na Burundi kwa reli. Upembuzi wa kina wa mtandao huo wa reli umekamilika na hatua inayofuata ni usanifu na ujenzi. Reli hii ni miongoni mwa reli zilizopo katika Mpango Kabambe wa Reli wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Kipaumbele iliyoidhinishwa na Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama. Katika jitihada za kuimarisha miundombinu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, mwezi Novemba, 2012, Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya Mkutano wa Pili wa Kazi *(Retreat)* wa Viongozi Wakuu wa Jumuiya kuhusu Uendelezaji wa Miundombinu katika Jumuiya huko Nairobi Kenya. Katika Mkutano huo, Viongozi Wakuu waliidhinisha miradi ya vipaumbele ya uendelezaji wa miundombinu yenye sura ya kikanda. Miundombinu hiyo ni pamoja na reli, bandari, nishati na barabara wezeshi. Kwa upande wa Tanzania, Miradi ya kipaumbele iliyoidhinishwa ni ifuatayo:-

(a) Miradi ya Uendelezaji Reli.

(i) Ukarabati na ujenzi wa reli ya kati (Dar es Salaam-Tabora-Mwanza-Kigoma) kwa kiwango cha *standard gauge* inayounganisha Tanzania na nchi za Rwanda na Burundi;

(ii) Ukarabati wa reli ya Voi-Taveta-Holili-Moshi-Arusha inayounganisha Tanzania na Kenya; Ujenzi na ukarabati wa reli ya Tanga – Arusha – Musoma; na

(iii) Uendelezaji wa reli ya Mtwara – Mbambabay.

(b) Miradi ya Uendelezaji Bandari.

(i) Kuongeza kina cha gati Namba 1-7 katika bandari ya Dar es Salaam;

(ii) Ujenzi wa gati mpya Namba 13-14 katika bandari hiyo; ujenzi wa bandari ya Maruhubi - Zanzibar, ujenzi wa Chelezo *(Dry Dock Construction)* na Kivuko *(Roll on Roll Off – RORO)* kati ya bandari za Dar es Salaam, Zanzibar, Pemba, Tanga na Mombasa; na

(iii) Matengenezo katika Bandari za Maziwa Makuu ya Victoria na Tanganyika.

(c) Miradi ya Uendelezaji Barabara.

(i) Ujenzi wa barabara za Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma zinazounganisha Tanzania na nchi za Burundi na Rwanda;

(ii) Ujenzi wa barabara za Nyanguge - Musoma – Sirari zinayounganisha Tanzania na nchi za Kenya na Uganda;

(iii) Barabara za Tanzania zitakazopunguza msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam ambazo ni Banana-Tangi Bovu; na

(iv) Upanuzi wa barabara ya Morogoro.

(d) Miradi ya Uendelezaji Nishati.

(i) Uzalishaji na usambazaji wa umeme katika maporomoko ya mto Rusumo utakaozinufaisha Nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi;

(ii) Uzalishaji wa umeme katika eneo la Murongo/ Kigagati wenye Megawati 16;

(iii) Nsongezi wenye Megawati 34.

(e) Miradi ya Kuzalisha Umeme.

(i) Uzalishaji wa Megawati 240 kutoka katika mradi wa Kinyerezi II na megawati 300 kutoka katika mradi wa Kinyerezi III; na

(ii) Uzalishaji wa umeme wa makaa ya mawe wa Kiwira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viongozi Wakuu wa Jumuiya wameziagiza Nchi Wanachama na Baraza la Mawaziri la Jumuiya kuhuisha miradi ya vipaumbele iliyoidhinishwa katika mipango na mikakati ya kitaifa na kikanda ili kuwezesha miradi hiyo kutekelezwa. Uendelezaji wa miundombinu hii utaiwezesha Tanzania na Nchi Wanachama kuzitumia fursa zitokanazo na mtangamano hususan, Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja. Aidha, kwa kuzingatia kuwa Tanzania inapakana na nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo baadhi yake hazina bandari, uendelezaji wa miundombinu hii utaiwezesha Tanzania kunufaika kikamilifu na jiografia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kuwa sekta husika zitazingatia na kutoa kipaumbele kwa miradi hiyo katika Mipango na Mikakati yao ili kuwezesha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Usafiri wa Anga. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika maandalizi ya taratibu za matumizi ya Mfumo Rahisi wa Mawasiliano ya Anga unaotumia mfumo wa Kimataifa wa Mawasiliano ya *Satellite (Global Navigation Satellite System - GNSS).* Mfumo huu unatarajiwa kutumika katika viwanja vya kimataifa na vya kitaifa katika Nchi Wanachama ili kurahisha mawasiliano ya anga. Maandalizi ya mfumo huu yanatarajiwa kukamilishwa katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano kuhusu

uandaaji wa Mfumo wa Kikanda wa Kusimamia Uchunguzi wa Ajali za Ndege yaliendelea katika mwaka 2012/2013. Lengo la kuanzisha Mfumo huu ni kuinua kiwango, uwezo wa kitaaluma na uzoefu kwa wachunguzi wa ajali za ndege. Kuanzishwa kwa Mfumo huu ni utekelezaji wa matakwa ya Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (*International Civil Aviation Organisation - ICAO)* linalozitaka Mamlaka za Usafiri wa Anga kuzingatia uimarishaji wa huduma za uokozi na uchunguzi wa ajali za ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika majadiliano baina ya Nchi Wanachama ya kuanzisha Mfumo wa Mawasiliano ujulikanao kama *Automatic Dependent Surveillance – Broadcast.* Lengo la mfumo huu ni kuziwezesha Nchi Wanachama kushabihiana katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na kuwa na uwezo wa kuona na kusimamia eneo kubwa la anga. Mfumo huu unatarajiwa kukamilishwa mwezi Januari, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Nishati. Katika mwaka 2012/2013, kazi ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuunganisha Gridi za Tanzania na Kenya kutokea Singida (Tanzania) hadi Isinya (Kenya) kupitia Arusha na Namanga ikiwa ni sehemu ya Mradi wa njia Kuu ya Umeme ya Zambia, Tanzania na Kenya ilikamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuzalisha Umeme Katika Miji ya Murongo/Kikagati. Katika mwaka 2012/2013, Wizara iliendelea kuratibu majadiliano ya Mikataba mbalimbali itakayowezesha utekelezaji wa Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Murongo/Kikagati unaotarajiwa kuzalisha Megawati 16. Mikataba hiyo ni pamoja na Mkataba wa Makubaliano *(Bilateral Agreement)* kati ya Tanzania na Uganda wa uzalishaji wa umeme huo, Mkataba wa mgawanyo na uuzaji wa umeme *(Power Sharing and Selling Agreement - PSSA),* pamoja na Mkataba wa kununua umeme *(Power Purchase Agreement* - PPA). Mikataba hii ni muhimu katika utekelezaji wa mradi huu na inatarajiwa kukamilishwa katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kongamano la Sita na Maonesho ya Petroli ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mwaka 2012/13, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Sekta ya Nishati iliratibu na kushiriki katika Kongamano la Sita na Maonesho ya Petroli ya Jumuiya ya Afrika Mashariki lililofanyika mwezi Februari, 2013, jijini Arusha. Kongamano hilo liliwashirikisha wadau zaidi ya 900 wa Sekta ya Utafutaji na Uvunaji wa Madini, Gesi Asilia na Mafuta kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwingineko duniani. Kongamano liliwezesha Nchi Wanachama kutangaza fursa za uwekezaji katika Nchi za Afrika Mashariki kwenye sekta hizo muhimu kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mawasiliano. Katika mwaka 2012/2013, Nchi Wanachama zilikamilisha Itifaki ya Ushirikiano katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(EAC Protocol for Cooperation on ICT Networks).* Itifaki hiyo iliidhinishwa na Viongozi Wakuu wa Jumuiya mwezi Novemba, 2012. Itifaki hiyo itaimarisha ushirikiano katika maendeleo ya Teknohama baina ya Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwianishaji wa Uzito wa Magari Katika Barabara. Katika mwaka 2012/2013, Nchi Wanachama zimekamilisha maandalizi ya Muswada wa Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Udhibiti wa Uzito wa Magari. Muswada huu unalenga kutunga sheria itakayowezesha kuwianisha uzito wa magari kwa lengo la kulinda barabara na kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha na hivyo kupunguza gharama za kufanya biashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Muswada huu unaendelea kujadiliwa katika Bunge la Afrika Mashariki na unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha wa 2013/14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuratibu ujenzi wa Vituo vya Utoaji Huduma kwa Pamoja Mipakani (*One Stop Border Posts - OSBPs).* Ujenzi wa vituo hivi unalenga kurahisisha utoaji huduma za kiforodha, uhamiaji, udhibiti wa ubora, viwango, usalama wa bidhaa na usalama kwa jumla katika mipaka.

Aidha, Vituo hivi vitawezesha taratibu zote za uvukaji wa mipaka kutolewa katika upande mmoja wa Nchi Mwanachama zinazopakana na hivyo kupunguza urasimu wa kuvuka mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Vituo vya Holili/Taveta, Sirari/Isebania, Mutukula/Mutukula na Horohoro/Lunga Lunga upo katika hatua za mwisho. Aidha, Kituo cha Holili/Taveta kitaanza kutumika mwezi Juni, 2013. Ujenzi wa Vituo vya Rusumo/Rusumo, Kabanga/Kobero na Namanga/Namanga unatarajiwa kukamilishwa katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Aprili, 2013 Bunge la Afrika Mashariki lilipitisha Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Uanzishaji na Uendeshaji wa Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani. Sheria hii itawezesha vituo vya Pamoja vya Mipakani kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makao Makuu ya Jumuiya. Katika mwaka 2012/2013, ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Jumuiya ulikamilika na lilizinduliwa na Wakuu wa Nchi tarehe 28 Novemba, 2012. Aidha, Serikali ya Tanzania imekamilisha ujenzi na matengenezo ya barabara yenye urefu wa mita 300 ya kuingia katika Makao Makuu hayo. Nawashukuru kwa dhati Viongozi na Watendaji wote waliosimamia na kutoa msukumo uliowezesha kukamilisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu. Hatua hii ya kukamilika kwa jengo la Makao Makuu imeijengea heshima Tanzania na Jumuiya kwa jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta za Huduma za Jamii. Sekta za Elimu, Utamaduni na Michezo, Afya na Sayansi. Uwianishaji wa Mifumo ya Elimu na Mitaala katika Jumuiya. Wizara iliratibu na kushiriki katika maandalizi ya Mpango wa Utekelezaji wa Kuwianisha Mifumo ya Elimu na Mitaala. Aidha, Baraza la Mawaziri la Jumuiya limeidhinisha maandalizi ya Mikakati saba inayolenga kuhuisha mifumo na mitaala ya elimu katika Nchi Wanachama katika ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari, ualimu, elimu ya wenye mahitaji

maalum, watu wazima na ufundi. Timu ya wataalam kutoka Nchi Wanachama inaendelea na maandalizi ya Mikakati hiyo pamoja na mitihani na kalenda ya mihula ya masomo inatarajiwa kukamilishwa katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaratibu na kushiriki katika majadiliano ya Kutunga Sheria Mpya ya Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki *(Inter - University Council of East Africa - IUCEA).* Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuratibu Uwianishaji wa Mifumo ya Elimu ikiwa ni pamoja na mitihani na kalenda ya mihula ya masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Elimu Zilizobobea. Nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Taasisi nne, kati ya tano za Tanzania, zilizodahiliwa zilikidhi vigezo na hivyo kustahili kuwa Taasisi Zilizobobea. Taasisi hizo ni: **-**

(a) Taasisi ya Mafunzo ya Ubaharia (DMI). *(Makofi)*

(b) Taasisi ya Sanaa Bagamoyo (TASUBA). *(Makofi)*

(c) Chuo Kikuu cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi (MUCCoBs). *(Makofi)*

(d) Chuo cha Wanyamapori - Mweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Nchi Wanachama zimekubaliana kuwa kwa kuanzia kila Nchi iteue Taasisi moja miongoni mwa Taasisi zilizokidhi vigezo itakayowezeshwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Tanzania iliiteua Taasisi ya Sanaa Bagamoyo (TASUBA). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kufanya udahili wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitivo cha Sayansi za Baharini – Zanzibar unaendelea hususan katika kujiandaa ili kukidhi vigezo vya taasisi ya elimu iliyobobea. Chuo hiki ni miongoni mwa Taasisi zitakazofanyiwa ukaguzi katika awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2013/2014, Wizara itaendelea kuratibu mchakato wa kuiwezesha TASUBA kupata rasilimali kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ilivyoamuliwa na Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashindano ya Insha ya Jumuiya. Katika mwaka 2012/2013, Wizara iliendelea kuratibu na kukamilisha Shindano la Uandishi wa Insha la Jumuiya linaloshirikisha wanafunzi wa Shule za Sekondari katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mashindano haya yanalenga kuwapa wanafunzi uelewa wa masuala mbalimbali kuhusu Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mada ya Insha kwa mwaka 2012 ilikuwa 'Jadili Nafasi ya Elimu katika Kuimarisha Mtangamano wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki'. Washindi wa mwaka 2012 walikabidhiwa zawadi zao katika Mkutano wa 14 wa Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama uliofanyika mwezi Novemba, 2012 Nairobi, Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kijana Joel Anderson Mwaigomole, mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Mzumbe Mkoani Morogoro, iliyopo Mkoani Morogoro, alishinda nafasi ya pili kati ya nafasi tano za washindi wa Jumuiya katika shindano hilo. Naomba kutumia nafasi hii kumpongeza kijana huyu Wazazi na Walimu wake kwa kuliletea Taifa sifa kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2013, Mada inayoshindaniwa ni 'Maendeleo ya Miundombinu Yataboreshaje Maendeleo ya Kiuchumi ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki'. Natoa wito kwa wanafunzi na shule zote kushiriki kwa wingi kwenye shindano hili kwani pamoja na zawadi inayotolewa kwa mshindi, hii ni fursa ya kuufahamu mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kujiendeleza kitaaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki. Kama mnavyofahamu kuwa Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (*East African Kiswahili Commission*), yapo Zanzibar na katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuratibu zoezi la kuanzishwa kwa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ambayo Makao Makuu yake yatakuwa Zanzibar. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeshatoa jengo kwa ajili ya kuanzisha ofisi ya Kamisheni hiyo. Vilevile, zoezi la kufanya tathmini ya mahitaji ya rasilimali watu na fedha za uanzishwaji wa Kamisheni hiyo limekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, majadiliano ya Mkataba wa Uenyeji wa Kamisheni *(Headquarters' Agreement)* kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yatafanyika. Majadiliano hayo yanalenga kukamilisha upatikanaji wa rasilimali za uanzishwaji wa Kamisheni hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tamasha la Sanaa na Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Sanaa na Utamaduni imeratibu na kushiriki katika Tamasha la Kwanza la Sanaa na Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki lijulikanalo kama 'Jumuiya ya Afrika Mashariki Utamaduni *Festival' (JAMAFEST)* lililofanyika mwezi Februari, 2013, mjini Kigali, Rwanda. Tamasha hilo, pamoja na mambo mengine, lililenga kuwakutanisha Wadau wa Sekta ya Sanaa na Utamaduni kutoka Nchi Wanachama ili kuenzi tamaduni mbalimbali zilizopo katika nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Tamasha hili, Watanzania waliweza kujitangaza, kujenga mahusiano na ushirikiano na watu mbalimbali kutoka katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, washiriki walipata fursa ya kuuza kazi zao za kitamaduni na sanaa kama vile nguo, vitabu vya kiswahili, urembo na vinyago.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Hifadhi ya

Mazingira. Mradi wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika utekelezaji wa Mradi wa Jumuiya wa Utunzaji wa Mazingira na Matumizi Endelevu ya Ziwa Victoria *(Lake Victoria Environmental Programme - LVEMP II)* wenye miradi inayotekelezwa katika ngazi ya kanda na ngazi za kitaifa. Katika ngazi ya Taifa mradi una maeneo makuu kumi na moja yanayotekelezwa katika ngazi ya Wilaya. Katika maeneo hayo, miradi midogo 113 imeibuliwa na wananchi wenyewe na kupitishwa na Mradi. Miradi hii inalenga katika utunzaji wa mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria na vyanzo vya mito na maji. Aidha, Miradi hii itahusu udhibiti wa magugu maji, umwagaji na uachiaji wa majitaka na uhamasishaji wa matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Utunzaji wa Mazingira na Afya katika Bonde la Mto Mara. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeratibu na kushiriki katika utekelezaji wa Mradi wa Utunzaji wa Mazingira na Afya wa Jumuiya katika Bonde la Mto Mara. Katika kipindi hiki, Mradi umetoa mafunzo kwa wataalam kutoka Nchi za Kenya na Tanzania kuhusu upimaji wa athari kwa mazingira *(Strategic Environmental Impact Assessment).* Aidha, Mradi huu umetoa Mafunzo ya udhibiti wa taka ngumu kwa wafanyakazi wa hoteli za kitalii zilizopo Serengeti, Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/13, Wizara iliendelea kuratibu utekelezaji wa agizo la Baraza la Kisekta la Mawaziri kuwa tarehe 15 Septemba ya kila mwaka iwe ni ya Maadhimisho ya Siku ya Mara (Mara Day) katika eneo la Bonde la Mto Mara lilipo mpakani mwa Kenya na Tanzania. Lengo la maadhimisho hayo ni kuhamasisha uboreshaji na usimamizi wa rasilimali na Bioanuai za Bonde hilo. Maadhimisho hayo kwa mwaka 2012/2013 yalifanyika Narok nchini Kenya ambapo kaulimbiu ya Maadhimisho hayo ilikuwa ni "Mara – Uhai Wetu". Maadhimisho hayo yalifanyika kwa njia ya kutoa elimu kwa jamii, kutembelea miradi mbalimbali ya mazingira na maonesho ya bidhaa mbalimbali. Kwa mwaka 2013/2014, maadhimisho haya yamepangwa kufanyika Mugumu, Wilayani Serengeti,

Tanzania. Aidha, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuratibu na kushiriki katika Maadhimisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Utunzaji na Usimamizi wa Pamoja wa Maliasili na Rasilimali za Ziwa Chala, Jipe na Mto Umba. Katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta imeendelea kuratibu maandalizi ya Programu ya Utunzaji na Usimamizi wa Pamoja wa Maliasili na rasilimali za ziwa Chala na Jipe na Mto Umba iliyopo mpakani mwa Tanzania na Kenya. Aidha, Hati ya Makubaliano kwa ajili ya Usimamizi wa pamoja wa Mazingira na Maliasili ya Ziwa Chala na Jipe na Ikolojia ya Mto Umba ilisainiwa na Serikali za Tanzania na Kenya mwezi Februari, 2013. Hati hii inalenga kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizi mbili katika uhifadhi wa mazingira katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Afya. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Programu na Miradi katika Sekta ya Afya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye maeneo yafuatayo:-

(a) Kuwianisha sera, sheria na taratibu za usajili wa madawa ya msingi kwa binadamu kwa kuzingatia viwango vya ubora kwenye Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lengo ni kuboresha upatikanaji wa dawa kwa urahisi kwa kuzingatia viwango vya ubora unaokubalika;

(b) Kuimarisha Maabara za Afya kwenye Nchi Wanachama ili kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza na yanayoambukiza;

(c) Kuendelea kujenga uwezo wa utoaji huduma kwa taasisi za kiraia zinazoshughulikia masuala ya afya ya watoto na vijana kwa kupitia mafunzo ya namna ya kutoa huduma, namna ya kupata ufadhili wa miradi na programu mbalimbali kwa kushirikiana na Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Mafunzo haya yanatolewa kwa makundi mbalimbali ya jamii kama Waelimisha Rika Vinara, *Champions* wa makundi ya vijana na wawakilishi wa makundi ya vijana;

(d) Mafunzo kuhusu udhibiti wa magonjwa ya maambukizi kwa binadamu na wanyama kutokana na mwingiliano uliopo mipakani yameendelea kutolewa kwa wananchi kwenye Nchi Wanachama katika maeneo ya Rusumo, Namanga, Kabanga na Kobero. Mafunzo haya yamekuwa yakifanyika kwa nyakati tofauti, na mara ya mwisho yamefanyika mwezi Septemba, 2012;

(e) Mradi wa kudhibiti sumu kuvu (*Aflatoxin*) na Kuimarisha Lishe *(EAC Aflatoxin Control and Improved Nutrition)* unaolenga kuelimisha jamii juu ya tatizo la Sumu kuvu inayopatikana kwenye mazao ya vyakula; kuimarisha udhibiti wa Sumu kuvu kupitia hatua mbalimbali za biashara ya mazao pamoja na kudhibiti sumu katika mazao yakiwa shambani kwenye Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mradi huo ulizinduliwa mwezi Oktoba, 2012, wakati wa kikao cha 8 cha Baraza la Mawaziri la Afya la Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

(f) Mpango wa *Open Health Initiative (OHI)* ambao ni jitihada za Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kuhakikisha kuwa Malengo ya Maendeleo ya Milenia 4 & 5 ambayo yanalenga kuboresha afya ya mama na mtoto kwenye Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yanatekelezwa. Mpango huu unafadhiliwa na *NORAD* kupitia *The Clinton Health Access Initiatives*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara itaendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu masuala ya Afya ikiwa ni pamoja na kuwianisha sera, sheria na taratibu za usajili wa madawa ya msingi kwa binadamu kwa kuzingatia viwango, kuimarisha Maabara za Afya kwenye Nchi Wanachama, kujenga uwezo wa utoaji huduma kwa taasisi za kiraia zinazoshughulikia masuala ya watoto, udhibiti wa magonjwa ya maambukizi kwa binadamu na wanyama mipakani, kudhibiti sumu kuvu, kuimarisha lishe na Mpango wa *Open Health Initiative (OHI).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Jinsia na Maendeleo

ya Jamii. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau iliratibu na kushiriki katika Kongamano la Haki ya Mtoto lililofanyika mwezi Septemba, 2012, Mjini Bujumbura, Burundi. Kongamano hilo lilijadili masuala mbalimbali ikiwemo hali ya Haki za Mtoto katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo ilipendekezwa kuanzishwa kwa Sera ya Haki ya Mtoto katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano Katika Siasa, Ulinzi na Usalama. Mkakati wa Kikanda wa Kusimamia Amani na Usalama; Nchi Wanachama zinaendelea kutekeleza Mkakati wa Kikanda wa ushirikiano katika Amani na Usalama uliosainiwa na Nchi Wanachama mwaka 2006. Katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea na kuratibu na kushiriki katika zoezi la kupitia upya Mkakati huu, kwa lengo la kutathmini utekelezaji wake ili uendane na mahitaji ya sasa. Mapitio hayo yanatarajiwa kukamilika katika mwaka 2013/14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama wa Jumuiya zimekubaliana kuwa na operesheni za pamoja za mara kwa mara kwa lengo la kukabiliana na uhalifu katika maeneo mbalimbali ikiwemo wizi wa magari, mifugo na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Aidha, Nchi Wanachama zimekubaliana kuangalia uwezekano wa kushirikiana na Nchi nyingine majirani katika kukabiliana na changamoto mpya zinazojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki ya Amani na Usalama. Ili kuimarisha hali ya usalama katika Jumuiya, mwaka 2012/2013, Nchi Wanachama zimeendelea na majadiliano ya kutunga Itifaki ya Amani na Usalama. Itifaki hii iliidhinishwa na Viongozi Wakuu wa Jumuiya katika Mkutano wao wa 14 uliofanyika mwezi Novemba, 2012 na kutiwa saini na Nchi Wanachama mwezi Februari, 2013 Jijini Dar es Salaam. Kwa sasa Nchi Wanachama zinaendelea na taratibu za kuridhia Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwianishaji wa Shughuli za

Kipolisi. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuratibu zoezi la kuandaa miongozo itakayosimamia uwianishaji na uendeshaji wa shughuli za kipolisi katika Jumuiya. Aidha, katika mwaka 2012/2013, Nchi Wanachama zimeiteua Uganda kuwa mwenyeji wa Kituo cha Kanda cha Rufaa cha Maabara ya Utambuzi wa Vielelezo *(Regional Referral Forensic Centre).* Kujengwa kwa kituo hicho kutapunguza gharama ambazo Nchi Wanachama zinaingia katika kupeleka sampuli nje ya Jumuiya kwa ajili ya vipimo ambavyo haviwezi kufanyika katika nchi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kupambana na Madawa Haramu ya Kulevya. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika vikao vya Jumuiya vya Wakuu wa Taasisi za kupambana na madawa haramu ya kulevya. Lengo la vikao hivi, pamoja na mambo mengine, ni kubadilishana taarifa na kujenga uelewa wa pamoja wa kudhibiti uhalifu huo ambao ni hatari kwa Nchi Wanachama. Aidha, Nchi Wanachama zinaendelea na zoezi la kupitia sheria za Nchi zao kwa lengo la kuhuisha sheria hizo ili zitoe adhabu zinazoshabihiana katika Nchi Wanachama. Zoezi hili litaendelea katika mwaka 2013/14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapambano Dhidi ya Uharamia. Katika mwaka 2012/2013, Nchi Wanachama ziliendelea kufanya maandalizi ya Mkakati wa kupambana na uharamia katika Bahari ya Hindi. Lengo la Mkakati huu ni kuwezesha Nchi Wanachama kukabiliana na uharamia kwenye Bahari ya Hindi. Mkakati huu unatarajwa kukamilika katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mazoezi ya Pamoja ya Kijeshi. Katika kuimarisha ushirikiano miongoni mwa Majeshi ya Nchi Wanachama katika mwaka 2012/2013, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika zoezi la kijeshi la pamoja lijulikanalo kama 'Ushirikiano Imara 2012' lililofanyika mwezi Oktoba, 2012 nchini, Rwanda. Zoezi hili lililenga kujenga na kuimarisha mfumo na uelewa wa pamoja wa utendaji katika operesheni za kijeshi kama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapambano Dhidi ya Ugaidi. Katika mwaka 2012/2013, Nchi Wanachama zimeendelea na maandalizi ya mikakati ya kukabiliana na ugaidi, ikiwa ni pamoja na Rasimu ya Hati ya Makubaliano *(MoU)* itakayosimamia ushirikiano katika mapambano dhidi ya ugaidi. Mikakati hii ni muhimu katika kuimarisha ushirikiano katika kupambana na ugaidi ndani ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara iliendelea kuratibu utekelezaji wa mradi wa kudhibiti kusambaa kwa silaha haramu ndogo ndogo na za kati. Mradi huu ambao umetekelezwa kwa kipindi cha miaka sita ulifungwa rasmi mwezi Februari, 2013. Katika sherehe za ufungaji, Nchi Wanachama ziliadhimisha kwa kufanya zoezi la kuteketeza silaha haramu zipatazo 3,100 lililofanyika jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano Katika Siasa. Ibara ya 123 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya inabainisha kuwa Nchi Wanachama zitashirikiana katika masuala ya siasa. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara imeratibu na kushiriki katika majadiliano ya kuandaa Itifaki mbalimbali za Jumuiya katika eneo la Siasa. Itifaki hizo ni pamoja na Itifaki ya Kinga na Hadhi ya Kidiplomasia; Itifaki ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa; na Itifaki ya Utawala Bora. Majadiliano kuhusu Itifaki hizi yanatarajiwa kukamilishwa katika mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchaguzi Mkuu Nchini Kenya. Tarehe 4 Machi, 2013, jirani zetu Jamhuri ya Kenya ilifanya Uchaguzi Mkuu chini ya Katiba Mpya. Jumuiya ya Afrika Mashariki ilituma Timu ya Waangalizi 40 kutoka katika Nchi Wanachama katika uchaguzi huo. Mheshimiwa Abdulrahman Kinana, Spika wa Kwanza wa Bunge la Afrika Mashariki, aliongoza Timu ya Waangalizi kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zoezi hili, Jumuiya ilifanya uangalizi wa Uchaguzi kwa kutumia Vigezo vya

Tathmini ya Uchaguzi vilivyoandaliwa na kuidhinishwa na Jumuiya katika mwaka 2012/2013. Hii ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Jumuiya kutumia vigezo hivyo. Hatua hii ni uthibitisho wa ukomavu wa Jumuiya katika kuzingatia misingi ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchaguzi huo, Mheshimiwa Uhuru Kenyatta kutoka Muungano wa Jubilee, alichaguliwa kuwa Rais wa Nchi hiyo. Nachukua nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa wananchi wa Jamhuri ya Kenya kwa kufanya uchaguzi ulio huru, haki na kwa amani. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta na Mheshimiwa William Ruto kwa kuchaguliwa kuongoza Taifa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu kwa Umma. Vipindi vya Redio na Luninga. Katika mwaka 2012/2013, Wizara iliandaa vipindi vya luninga na redio. Vipindi vya luninga vilirushwa kupitia vituo vya *TBC1, StarTV* na *SIBUKA*. Aidha, kwa upande wa radio vipindi hivi vilirushwa kwenye stesheni za *TBC, SIBUKA FM* na *Radio Free Africa*. Wizara itaendelea kuandaa na kurusha vipindi vya aina hii katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa taarifa kwa umma kuhusu Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne, Wizara iliandaa kipindi cha luninga ambacho kilitoa taarifa kuhusu Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne katika Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika kipindi cha kuanzia mwaka 2006 hadi 2012. Kipindi hicho kilirushwa hewani na vituo vya luninga vya *TBC 1, ITV* na *Star TV* mwezi Januari, 2013. Aidha, nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kipindi cha Wizara kiliibuka kidedea kwa kipindi chake kuwa kipindi bora. Naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kukitangaza kipindi cha Wizara yangu kuwa kipindi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu ya mwaka jana niliahidi Bunge lako Tukufu kuhusu kukamilisha

mkakati wa mawasiliano wa Wizara yangu, kutoa mwongozo wa utoaji elimu kwa umma. Nashukuru kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imekamilisha Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara na kuuzindua rasmi mwezi Februari, 2013 na leo tumeugawa kwa Wabunge wote. Mkakati umebainisha njia mbalimbali zitakazotumika katika kutoa elimu kwa umma ikiwa ni pamoja na mikutano, warsha, semina, vipindi vya redio na luninga, machapisho, vipeperushi, magazeti na ujumbe mfupi wa simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushiriki Katika Maonesho mbalimbali. Katika mwaka 2012/2013, Wizara ilishiriki katika Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Dodoma mwezi Agosti, 2012. Katika Maonesho hayo, Wizara ilitoa Elimu inayohamasisha uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma zenye kukidhi ubora na viwango ili kumudu ushindani katika soko kubwa la Afrika Mashariki, na kuzitambua na kuzitumia fursa za uwekezaji na ajira zitokanazo na Soko la Pamoja la Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara, kwa kushirikiana na wadau, iliratibu ushiriki wa wajasiriamali wa Tanzania katika Maonesho ya 13 ya Juakali/ Nguvukazi yaliyofanyika Nchini Burundi mwezi Desemba, 2012. Maonesho haya hufanyika kila mwaka kwa mzunguko katika Nchi Wanachama yakiwa na lengo la kukuza ajira, biashara pamoja na kuwapatia Wajasiriamali fursa za kuonesha bidhaa zao. Katika maonesho hayo, jumla ya wajasiriamali 87 kutoka Tanzania walishiriki. Bidhaa walizoonesha na kuuza ni nguo za batiki, vikoi, sanaa za mikono, bidhaa za ngozi, uhunzi na madawa ya tiba asili. Natoa wito kwa Watanzania wengi zaidi kutumia fursa hii kujifunza, na kuendelea kujenga uwezo wao wa kiushindaji kwa kuimarisha zaidi ubora wa bidhaa zao ili kutumia fursa zilizopo katika Soko la Jumuiya. Aidha, natoa wito kwa wajasiriamali kuwa wabunifu zaidi na kutengeneza bidhaa mpya mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utoaji Elimu kwa Pamoja Mipakani. Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika zoezi la Utoaji wa Elimu kwa Umma kwa Pamoja Mipakani kwa

kushirikiana na Nchi Wanachama. Zoezi hili linalenga kutoa elimu kuhusu masuala ya mtangamano kwa wafanyabiashara na wananchi mipakani pamoja na kupokea mrejesho, hususan kuhusu changamoto zinazowakabili wafanyabiashara, wasafiri, wasafirishaji, na jamii za mipakani na kuweka mikakati ya pamoja ya kutatua changamoto hizo. Aidha, mikutano hii inaimarisha na kuboresha mahusiano na ujirani mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013 elimu ilitolewa katika mpaka wa Holili/Taveta na Hororo/ Lungalunga kwa upande wa mpaka wa Tanzania na Kenya. Katika zoezi hilo, Nchi hizi mbili ziliazimia pamoja na mambo mengine kuanzisha masoko ya mipakani, kuunda kamati za pamoja za ujirani mwema na kutoa huduma katika vituo vya mipakani kwa saa 24 kwa pande zote mbili za mpaka, utekelezaji unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto za mipakani zinazosababishwa na uelewa mdogo kuhusu masuala ya mtangamano wa Afrika Mashariki, katika mwaka 2012/2013, Wizara ilifanya ziara katika mipaka ya Mutukula, Murongo na Kabanga Mkoani Kagera; Namanga Mkoani Arusha, Holili Mkoani Kilimanjaro na Sirari Mkoani Mara. Lengo la ziara hizi lilikuwa ni kutoa ufafanuzi wa sheria, sera, kanuni na taratibu zilizopo katika Jumuiya zinazorahisisha biashara na uwekezaji baina ya Nchi Wanachama. Mafunzo ya aina hii yataendela kutolewa katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchango katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha imeendelea kutekeleza maagizo ya Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama kuhusu kulipa kwa wakati michango ya Nchi kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mwaka 2012/2013, Mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa shilingi 11,320,230,400 ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2013 Tanzania ilikwisha wasilisha shilingi 10,841,573,000 ikiwa ni sawa na asilimia 95%. Wizara inaendelea kufuatilia ili

kupata kiasi kilichosalia na kuhakikisha Tanzania inaendelea kulipa mchango wake wote kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushiriki wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika uendelezaji wa mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ushirikiano huu umeendelea kwa kufanya chambuzi na tafiti mbalimbali kwa pamoja na kuandaa misimamo ya Taifa kwa pamoja; kufanya maandalizi kwa pamoja kupitia vikao na vikosi kazi mbalimbali vya kitaifa na kikanda; na kushiriki katika vikao mbalimbali vya Jumuiya. Ushirikiano huo umewezesha maslahi ya pande zote mbili za Muungano kuendelea kuzingatiwa katika shughuli na pia katika maamuzi mbalimbali yanayofikiwa kikanda. Vile vile, pande hizi mbili zinashirikiana katika maandalizi ya sera, mikataba, miradi na Itifaki mbalimbali za Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya Zanzibar. Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Maruhubi ni miongoni mwa miradi ya kipaumbele katika sekta ya Bandari iliyopitishwa na Viongozi Wakuu wa Jumuiya mwezi Novemba, 2012 katika Mkutano wao wa Pili wa Kazi wa kujadili uendelezaji wa miundombinu katika Jumuiya uliofanyika Nairobi, Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya Ujenzi wa Chelezo (*Dry dock construction*) na Kivuko (*Roll on Roll Off – RORO*) kati ya Bandari za Zanzibar, Dar es Salaam na Mombasa ni miongoni mwa miradi ya vipaumbele vya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyopo kwenye Mkakati wa Uchukuzi iliyowasilishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Ushirikiano wa Utatu wa *COMESA-EAC-SADC* ili kutafutiwa wafadhili. Miradi hii pia imeidhinishwa na Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama kama miradi ya kipaumbele katika sekta ya miundombinu na Wizara imejadiliana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kina kuhusu miradi hii.

Mheshimiwa Spika, Kufungua Ofisi ya Masuala ya Afrika Mashariki Zanzibar. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara ilikamilisha taratibu za kupata Ofisi Zanzibar

itakayotumika kuratibu masuala ya Mtangamano wa Afrika Mashariki. Aidha, upatikanaji wa vitendea kazi na watumishi kwa ajili ya uendeshaji wa Ofisi hiyo umekamilika na ofisi hiyo imeanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya Jamhuri za Sudan Kusini na Somalia kujiunga na Jumuiya. Katika mwaka 2012/2013, Nchi Wanachama zilifanya uhakiki wa ombi la Jamhuri ya Sudan Kusini kujiunga na Jumuiya kwa mujibu wa Ibara ya 3(b) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Taarifa ya Uhakiki iliwasilishwa katika Mkutano wa 14 wa Wakuu wa Nchi Wanachama uliofanyika mwezi Novemba, 2012. Baada ya kupitia taarifa ya uhakiki, Wakuu wa Nchi waliliagiza Baraza la Mawaziri kuanza majadiliano na Jamhuri ya Sudan Kusini ili kuiwezesha kujiunga na Jumuiya. Majadiliano hayo yataendelea katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Jamhuri ya Somalia iliwasilisha maombi ya kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2011. Wakuu wa Nchi Wanachama katika Mkutano wa 14 uliofanyika mwezi Novemba, 2012, waliliagiza Baraza la Mawaziri wa Jumuiya kufanya uhakiki wa endapo Nchi hiyo inakidhi vigezo vya kujiunga na Jumuiya kulingana na Ibara ya 3(3) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Zoezi hili linatarajiwa kufanyika katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Afrika Mashariki. Katika mwaka 2012/2013, Nchi Wanachama zilikamilisha taratibu za uanzishwaji wa Ofisi Ndogo ya Msajili wa Mashauri ya Mahakama ya Afrika Mashariki katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa upande wa Tanzania, Ofisi hii ipo katika jengo la Mahakama ya Rufaa, Dar es Salaam na ilizinduliwa mwezi Septemba, 2012. Uanzishwaji wa ofisi hizi unalenga kusogeza na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kimahakama na kwa gharama nafuu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Afrika

Mashariki katika kipindi cha mwaka 2012/2013 imepokea malalamiko mapya 14 na kutolea maamuzi malalamiko 22.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la Afrika Mashariki. Katika mwaka 2012/2013, Bunge la Afrika Mashariki lilifanya vikao vinne ambavyo vilijadili na kupitisha Miswada mitatu (3) ya sheria za Jumuiya, kupitisha maazimio tisa (9) pamoja na kupokea taarifa mbalimbali za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala na Maendeleo ya Rasilimali Watu. Kuimarisha uwezo wa Wizara kiutendaji. Katika mwaka 2012/2013, Wizara ilipewa kibali na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma cha ajira mpya ya Watumishi 18 katika kada mbalimbali. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inaendelea kukamilisha taratibu za kuajiri watumishi hao. Aidha, Wizara ilipandisha vyeo watumishi saba (7) baada ya kukidhi vigezo vya miundo yao ya utumishi na utendaji mzuri wa kazi kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma. Utendaji kazi wao ulipimwa kwa kutumia Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi (MWAMTUKA).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara iliwathibitisha katika vyeo Watumishi 23 na watumishi wawili walithibitishwa katika madaraka. Watumishi hao walithibitishwa baada ya kukamilisha kipindi cha matazamio na kuthibitisha kuyamudu majukumu yao mapya ya vyeo walivyopandishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo kwa watumishi. Latika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara iliendelea kutekeleza Mpango wake wa Mafunzo wa Miaka Mitatu (2011/12-2013/14) kwa kuandaa na kutekeleza Mpango wa Utekelezaji wa Mwaka Mmoja (2012/2013). Lengo la Mpango huu ni kuwajengea watumishi uwezo na ujuzi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Hadi kufikia mwezi Machi, 2013 jumla ya watumishi 56 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi. Kati

ya watumishi hao, watumishi 11 wanahudhuria mafunzo ya muda mrefu na 45 ya muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadili ya utumishi wa umma. Katika kuhakikisha kuwa Watumishi wa Wizara wanatekeleza majukumu yao kwa uadilifu na kuzingatia maadili ya utumishi wa umma, katika mwaka 2012/2013 Wizara ilitoa mafunzo kwa watumishi mia moja na saba (107) kuhusu Maadili na Mapambano dhidi ya Rushwa katika Utumishi wa Umma. Lengo la mafunzo hayo ni kuhamasisha watumishi kuepuka vitendo na mienendo inayochochea ukiukwaji wa Maadili ya Utumishi wa Umma ikiwemo kutoa na kupokea rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI. Wizara imeendelea na mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI. Katika mwaka 2012/2013, Wizara iliandaa mafunzo ya uhamasishaji kwa watumishi wa Wizara yaliyofanyika mwezi Machi, 2013. Lengo la mafunzo hayo ni kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI, kuondoa unyanyapaa kwa watumishi wanaoishi na VVU/UKIMWI, kuhamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari pamoja na kuwahudumia wanaoishi na VVU/UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikishwaji wa watumishi. Wizara imeendelea kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa watumishi wanashirikishwa katika maamuzi. Wizara imeendelea kuzingatia utaratibu wa kuwa na vikao vya watumishi katika ngazi mbalimbali. Vikao hivyo ni pamoja na vikao vya Menejimenti, vikao vya Idara na Vitengo, vikao Elekezi, Baraza la Wafanyakazi na mikutano ya watumishi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa Wizara katika michezo ya SHIMIWI. Katika kuimarisha afya za watumishi na pia kuimarisha ushirikiano na mshikamano miongoni mwa Watumishi wa Umma, Wizara ilishiriki katika mashindano ya SHIMIWI ya mwaka 2012/2013 yaliyofanyika mwezi Septemba, 2012 Mkoani Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa mapato na matumizi. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi wa Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma, Sheria ya Ununuzi ya Umma na Miongozo ya Serikali. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kufanya vikao vya kila robo mwaka vya Kamati ya Udhibiti wa Mapato na Matumizi na kuwasilisha Taarifa za vikao hivi kwa wakati kwa Waziri Mkuu kama ulivyo utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba kutumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ilipata Hati Safi ya Ukaguzi wa Hesabu kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya Mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005, Wizara iliandaa na kutekeleza Mpango wa Ununuzi kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto na hatua zilizochukuliwa. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika mwaka wa fedha 2012/2013, bado zipo changamoto ambazo Wizara inakabiliana nazo. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(a) Kasi ndogo ya urekebishwaji wa Sheria za ndani ili kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja. Itifaki ya Soko la Pamoja inatoa fursa mbalimbali ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na uhuru wa biashara ya bidhaa na biashara ya huduma; uhuru wa kupata ajira katika Nchi wanachama; uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kuwekeza mitaji katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya; na uhuru wa kuanzisha na kuendesha shughuli za biashara na uchumi katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya. Hata hivyo, ili manufaa yaliyopo katika Itifaki hiyo yapatikane, Nchi Wanachama zinatakiwa kufanyia marekebisho ya sheria husika za ndani. Kumekuwepo na kasi ndogo ya kufanya marekebisho ya sheria za Tanzania ambazo ni muhimu katika

kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja. Wizara, kwa kushirikiana na Wadau, imeendelea kufanya mapitio ya sheria za ndani na kutoa mapendekezo ya maeneo ya kufanyiwa marekebisho. Natoa wito kwa sekta husika kuongeza kasi ya mapitio ya sheria husika ili kuliwezesha Taifa kunufaika na Soko la Pamoja la Afrika Mashariki;

(b) Ushiriki mdogo wa Wadau katika utekelezaji wa Mtangamano wa Afrika Mashariki. Maeneo ya ushirikiano katika mtangamano wa Afrika Mashariki yanagusa Sekta mbalimbali hapa nchini, hivyo kuhitaji ushiriki wa sekta husika katika majadiliano na uzingatiaji wa makubaliano katika mipango ya Sekta kwa ajili ya utekelezaji. Natoa wito kwa Wadau kutoa uzito stahiki katika uendelezaji wa Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(c) Kama nilivyobainisha katika hotuba yangu, suala ya Vikwazo Visivyo vya Kiforodha *(Non Tariff Barriers – NTB)* limeendelea kuwepo na hivyo kutoziwesha Nchi Wanachama kunufaika kikamilifu na utekelezaji wa Umoja wa Forodha. Naendelea kutoa wito kwa wadau wote kuongeza kasi ya uondoaji wa vikwazo hivi ili kuwezesha Watanzania kunufaika na fursa za kibiashara zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki;

(d) Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu mtangamano na hivyo kuwafanya Watanzania kutozitumia kikamilifu fursa zitokanazo na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wizara inaendelea kutekeleza Mkakati na Mpango wa kutoa Elimu kwa Umma ili kuwawezesha Watanzania kunufaika na mtangamano wa Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na kushirikiana na Wadau ili kuwezesha uhuishaji wa masuala ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mipango ya Halmashauri. Aidha, kutokana na semina ambazo Wizara imekuwa ikifanya kwa Waheshimiwa Wabunge, Wizara inawaomba Waheshimiwa Wabunge wanapokwenda kwa wapiga kura wao waendelee kutoa elimu kwa umma juu ya Mtangamano kwani suala hili sio la Wizara pekee bali ni la Taifa kwa jumla. Kupanuka kwa haraka kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki

kusikoendana na raslimali (fedha na rasilimaliwatu) zilizopo. Ili kukabiliana na changamoto hii, Wizara imeendelea kuwasiliana na Wadau husika ambapo changamoto ya upungufu wa raslimali watu inaendelea kufanyiwa kazi;

(e) Baadhi ya Nchi Wanachama kutaka kuingia katika hatua za mtangamano za juu, ambazo wakati muafaka haujafikiwa. Tanzania imeendelea kusisitiza umuhimu wa kuendeleza mtangamano hatua kwa hatua kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 5(2) ya Mkataba ili kujenga misingi imara ya Jumuiya na kuwezesha wananchi kunufaika na mtangamano na kuwa na maisha bora. Natoa wito kwa wadau kusimamia umuhimu wa kuweka msingi imara wa uendelezaji mtangamano ulio endelevu na ambao umejikita katika kuzingatia taratibu zilizowekwa na kuwashirikisha wananchi katika utekelezaji wa mtangamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto nilizoainisha, katika mwaka 2012/2013 tumeweza kupata mafanikio makubwa na ya kujivunia katika ushiriki wetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Naamini kabisa tukiongeza juhudi zaidi na umakini tunaweza kupata mafanikio zaidi. Katika kuhimiza uchangamkiaji wa fursa za soko la Jumuiya, Mheshimiwa Rais, alitutanabaisha wakati wa Kongamano la Uwekezaji lililofanyika Jijini Dar es Salaam mwaka 2011 kama ifuatavyo, na naomba kunukuu:-

"We could do better and aiming to do that should be our guiding motto. It should inform our vision and actions"

Hii ni Kauli Mbiu muhimu kwa sekta zote zinazohusika na utekelezaji wa mtangamano wa Afrika Mashariki hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na wadau mbalimbali itaendelea kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2013/2014. Shughuli zitakazopewa kipaumbele katika mwaka wa fedha 2013/2014 ni pamoja na:-

(a) Kuratibu, kushiriki na kuongoza vikao vya kisheria vya Jumuiya, ikiwemo Mikutano ya Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama, Mikutano ya Baraza la Mawaziri, Mabaraza ya Mawaziri ya Kisekta na kusimamia uendelezaji wa mtangamano unaozingatia maslahi ya Taifa na Jumuiya;

(b) Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Programu na Miradi ya Jumuiya, ikiwa ni pamoja na miradi ya uendelezaji wa miundombinu barabara, reli, bandari, nishati iliyoidhinishwa na Wakuu wa Nchi kama miradi ya kipaumbele katika Jumuiya;

(c) Kuratibu, kushiriki na kuongoza majadiliano ya uanzishwaji wa Umoja wa Fedha wa Jumuiya;

(d) Kuratibu, kushiriki na kuongoza majadiliano ya uanzishwaji wa Himaya Moja ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(e) Kuratibu na kushiriki katika vikao vya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge la Afrika Mashariki;

(f) Kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara na Mpango wa Utoaji Elimu kwa Umma;

(g) Kuratibu, kushiriki na kusimamia majadiliano ya uanzishwaji wa Utatu wa *SADC-EAC-COMESA*, pamoja na majadiliano ya Ubia wa Kiuchumi baina ya Jumuiya na Umoja wa Ulaya (*Economic Partnership Agreement - EPA*);

(h) Kuratibu utekelezaji wa Mipango ya Jumuiya ya Uendelezaji Viwanda, Mifugo na Uvuvi na Mpango Kazi wa Uzalishaji wa Chakula katika Jumuiya;

(i) Kuimarisha na kuendeleza Kituo cha Habari cha Wizara;

(j) Kufanya chambuzi, tafiti na tathmini mbalimbali kuhusu uendelezaji wa mtangamano wa Jumuiya

ya Afrika Mashariki, na kuandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali ya uendelezaji mtangamano inayozingatia maslahi ya Taifa katika Jumuiya;

(k) Kukamilisha Mpango wa Ushirikiano baina ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika masuala ya uhuishaji na utekelezaji wa Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mipango ya TAMISEMI;

(l) Kukamilisha ukusanyaji wa maoni ya wadau na maandalizi ya msimamo wa Tanzania kuhusu Mpangokazi wa kutekeleza Mapendekezo ya Kukabiliana na Hofu, Kero na Changamoto za Uanzishwaji wa Shirikisho la Kisiasa la Jumuiya ya Afrika Mashariki; na kuhusu Modeli ya Mfumo wa Shirikisho la Kisiasa; na

(m) Kuendelea kuimarisha uwezo wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wizara na kwa niaba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, napenda kuwashukuru kwa dhati Washirika wa Maendeleo wanaoshirikiana nasi katika kutekeleza Programu na Miradi mbalimbali katika Wizara na katika Jumuiya hususan, Serikali za Marekani, Uingereza, Ufaransa, Kanada, Norway, Sweden, Ubelgiji, Denmark, Finland, Japani na Ujeruman; Mashirika na Taasisi za Kimataifa za Jumuiya ya Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Japani ya Maendeleo ya Kimataifa, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japani, Benki ya Dunia, *GIZ, Rockefeller Foundation, The Investment Climate Facility for Africa (ICF), AWEPA, African Capacity Building Facility (ACBF), DFID, TradeMark East Africa (TMEA), na International Planned Parenthood Federation Africa Region (IPPFAR)* na Kilimo Trust.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha za Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ili Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2013/2014, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 20,470,107,000 kwa ajili

ya matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2013/2014. Kati ya fedha hizo, shilingi 19,000,000,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC),* na shilingi 1,470,107,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi *(PE).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii tumejumuisha viambatanisho mbalimbali ambavyo nimekwishavionyesha. Naomba viambatanisho hivyo vichukuliwe kuwa ni vielelezo vya hoja hii. Aidha, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anwani ya www.meac.go.tz. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi, kwa jinsi ambavyo wewe pamoja na wenzio wanaokalia Kiti hiki, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti mnavyoshughulikia shughuli za Bunge na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono na idadi ya waungaji mkono naona imetimia sana leo mpaka Mheshimiwa Vita Kawawa ameunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati atakayekuja kutoa maoni ya Kamati. Toka asubuhi naona Mwenyekiti wa Kamati leo amekasimu madaraka yake kwa Mheshimiwa Masauni aiwakilishe Kamati hiyo kwa asilimia mia moja. Mheshimiwa Masauni, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge kuhusiana na hoja iliyoko mbele yetu.

MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA KUHUSU WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2012/2013; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2012/2013; na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni moja ya Majukumu ya Kamati hii, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 2(3), Toleo la Mwaka 2013. Ili kutekeleza jukumu hili, Kamati ilikutana tarehe 28 Machi, 2013 na kupokea Taarifa ya Wizara kuhusu Utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1). Kamati ilipaswa kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2012/2013, lakini kwa kuwa kama ilivyo ada, Wizara hii haikuwa na Bajeti ya miradi hiyo, hakuna ziara iliyotekelezwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mipango ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Katika kufuatilia utekelezaji wa Mipango ya Bajeti ya Wizara hii, Kamati ilifuatilia Mambo Makuu manne yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kama yalivyotolewa Bungeni tarehe 3 Agosti, 2012.

(ii) Makusanyo ya Mapato ya Serikali kama ilivyolengwa na kuidhinishwa na Bunge;

(iii) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; na

(iv) Utekelezaji wa majukumu na malengo ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya mapato. Ingawa Wizara hii haikuwa na lengo la kukusanya Mapato ya Serikali, katika utekelezaji wa Majukumu yake kwa kuzingatia Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, Wizara ilikusanya kiasi cha Sh 533,200/= kutokana na mishahara iliyorejeshwa. Kiasi hicho ni sehemu ya kiasi kilichoidhinishwa kwa ajili ya kulipa mishahara ambacho ni Sh.1,024,993,520/=. Katika uchambuzi, kiasi hicho cha mshahara uliorejeshwa ni sawa na asilimia 0.03. Kamati ilibaini kuwa pamoja na kuwa si jambo la kawaida mishahara iliyokasimiwa kurejeshwa, hali hiyo ilitokea kutokana na sababu za taratibu za kiutumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maoni na ushauri**.** Ili kuhakikisha kuwa Serikali inafanyia kazi ushauri unaotolewa Bungeni, Kamati ilipokea maelezo ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa mMwaka wa fedha 2012/2013. Katika kipindi hicho ushauri uliotolewa ulihusu mambo kumi kuhusiana na dhima, wajibu na majukumu ya Wizara hii. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa sehemu kubwa ya ushauri wa Kamati bado inafanyiwa kazi na sehemu nyingine imetekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa ushauri uliotekelezwa ni kuhusu Itifaki ya Ushirikiano katika Masuala ya Ulinzi. Kamati iliishauri Serikali kuongeza umakini katika jambo hili. Taarifa ya Waziri ilionesha kuwa ushauri huu ulizingatiwa kwa kuongeza tahadhari katika ushirikiano wa kiulinzi ili kuepuka kuingia katika migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa ushauri ambao haukutekelezwa, unahusu kuanzishwa kwa Kitengo cha Utafiti katika Wizara hii. Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati haionyeshi namna Serikali ilivyofanyia kazi kikamilifu suala la kuanzisha kitengo muhimu cha utafiti katika Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kwa kuwa ni mwaka wa tatu sasa ushauri kama huu unatolewa, Kamati inaitaka

Serikali kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu maoni yake juu ya umuhimu wa Kitengo hiki na kisha kubainisha ni lini Kitengo hicho kitakuwa tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** mfano mwingine ni ushauri kuhusiana na lugha ya Kiswahili kama bidhaa katika nchi nyingine za Jumuiya. Wizara ilishauriwa kushirikiana na wadau wengine wa lugha hii ili kujipanga na kuuza Kiswahili kama bidhaa katika nchi nyingine za Jumuiya. Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati ilionesha kuwa Wizara imeweza kutetea na kuiwezesha Tanzania kuwa Mwenyeji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki, ambayo Makao Makuu yake yatakuwa Zanzibar. Aidha, Kamati ilijulishwa kuwa Serikali inaendelea na mchakato wa kuiwezesha kuingia mkataba na nchi nyingine Wanachama ili kuwawezesha Walimu wa Lugha ya Kiswahili kupata ajira katika nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Ili kufuatilia kiasi cha fedha zilizotolewa na Hazina na kulinganisha na kiasi cha fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa majukumu ya Wizara hii, ni muhimu kufuatilia Taarifa ya upatikanaji wa fedha. Maelezo ya Wizara yalionesha kuwa hadi kufikia tarahe 28 Februari, 2013, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Sh.15,878,527,320/=. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 95 ya kiasi cha fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo, Kamati ilijulishwa kuwa wakati wa utekelezaji lilijitokeza pengo la mchango, kiasi cha Sh.2, 000,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa wakati wa mapitio ya bajeti kwa nusu Mwaka *(mid-year review)* Wizara iliongezewa Sh. 2,000,000,000/= nje ya kiasi cha Sh.16.643.667,000/= kilichoidhinishwa na Bunge. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 12 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kwa sababu hiyo, baada ya mapitio ya nusu ya mwaka, Wizara ikatengewa jumla ya Sh.18,643,667,000/=. Kati ya fedha hizo, Sh.10, 641,573,000/= ni kwa ajili ya mchango katika Jumuiya kiasi ambacho ni sawa na asilimia 57 ya fedha iliyotengwa kwenye bajeti ya Wizara**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi unaonesha

kuwa pesa zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za Wizara pamoja na mishahara ni Sh. 8,002,094,000/= sawa na asilimia 43. Kwa kuwa katika ya fedha hizo, Sh. 1,024,993,520/- ilikuwa ni bajeti ya mishahara ya watumishi, kiasi halisi cha uratibu na uendeshaji wa shughuli za Wizara hii kilikuwa ni Sh. 4,011,960,800/- tu sawa na asilimia 22 ya bajeti yote kwa Wizara hii. Kwa takwimu hizo, ni dhahiri kuwa ni kiasi kidogo cha bajeti ndicho kilichotengwa kwa ajili ya uratibu wa shughuli za Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si jambo jema kugharamia uanachama kwa kiasi kikubwa wakati bajeti halisi ya kuratibu shughuli hizo ni kidogo. Hali hii inaonesha uwezekano wa hatari ya kugharamia uanachama kiasi kikubwa bila kuwa na bajeti ya kutosha kufuatilia na kuratibu namna bora ya kunufaika na uanachama huo. Kamati ina maoni kuwa ni vema Serikali ikatafakari suala hili na kurekebisha ipasavyo dosari zote za kibajeti na mipango.

Mheshimiwa Mweyekiti, utekelezaji wa malengo ya bajeti. Ili kuhusisha kiasi cha fedha iliyotengwa na kupokelewa kwa ajili ya malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Kamati ilipokea maelezo kuhusu shughuli zilizotekelezwa. Shughuli hizo ziliainishwa katika maeneo kumi ya malengo. Miongoni mwa maeneo hayo ni Sera na Mikakati ya Taifa na Kanda, Utekelezaji wa Hatua za Mtangamano, Miradi na Programu ya Miundombinu ya Kicuhumi na Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Wizara kuhusu Sera na Mikakati ya Taifa na ya Kanda yalisababisha Kamati itake kujua kuhusu utekelezaji wa lengo la kukamilisha mchakato wa Serikali kuidhinisha Sera ya Taifa ya mtangamano. Aidha, Kamati ilipenda kufahamu hatua iliyofikiwa katika mpango wa kuridhia mkakati wa Kitaifa wa utekelezaji wa soko la pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Wizara ilionesha kuwa hadi sasa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Mtangamano wa Afrika Mashariki haijakamilika. Kuhusu Mkakati wa Kitaifa wa

Utekelezaji wa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, maelezo ya Waziri yalionesha kuwa Serikali imeiagiza Wizara hii kufanya mashauriano zaidi na sekta nyingine zinazohusika na kwamba kwa sasa, Wizara inaendelea kufanya mashauriano na Sekta hizo. Lengo ni kuwezesha sekta husika kujumuisha shughuli zilizoainishwa kwenye mkakati katika Mpango na Bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo hilo lilikuwa zuri na ndio maana Bunge lilipoidhinisha Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa fedha 2012/2013, halikushauri kufutwa kwa lengo hili. Hata hivyo kutokana na Taarifa ya Wizara, Kamati imebaini mambo makuu mawili:-

(i) Pamoja na umuhimu mkubwa wa kuwa na Sera ya Taifa ya Mtangamano wa Afrika Mashariki, bado hadi sasa mchakato wa Serikali kuidhinisha Sera hiyo haujakamilika. Ni maoni ya Kamati kuwa si vema kuwa Mwanachama wa Jambo ambalo kama Taifa hatujajipanga na kuliwekea mwongozo. Aidha, ni jambo la hatari kwa maslahi ya nchi yetu kuratibu shughuli za Mtangamano huu bila kuwa na Sera ya Taifa.

(ii) Maagizo ya Serikali kwa Wizara hii kuhusu Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki yanaonesha kuwa, Wizara haikufanya mashauriano kiasi cha kutosha na kushirikisha Sekta nyingine zinazohusika na Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Athari yake ni kutoidhinishwa kwa Mkakati huo. Kamati ina maoni kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kila Wizara na Idara kutimiza wajibu wake ipasavyo bila kusubiri kukumbushwa na kuelekezwa kwa msisitizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine wa eneo la utekelezaji lililotolewa Taarifa, ni kuhusu Hatua za Mtangamano. Katika eneo hili, moja ya mambo yaliyoelezwa ni kuhusu soko la pamoja na umoja wa Fedha *(Monetary Union).* Maelezo ya Waziri yalibainisha kuwa zoezi la Kurekebisha Sheria zilizoainishwa na Kikosi Kazi cha Mapitio ya Sheria halipewi uzito unaostahili na sekta husika. Jambo

hili, kwa maoni ya Kamati linahitaji umakini wa hali ya juu na kasi ya utekelezaji wake izingatie tija inayotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kutokana na uelewa mdogo wa Watanzania kuhusu fursa zilizopo katika Soko la Pamoja, Kamati imebaini kuwa kazi iliyofanywa na Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2012/2013, ilikuwa kidogo katika eneo hili ikilinganishwa na ilivyopaswa kuwa. Bado kuna kazi kubwa ya kuwaelimisha Watanzania juu ya fursa zilizopo kwa makubaliano kuhusu Soko la Pamoja, ili hatua hiyo, iwe na manufaa kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara ililenga kukamilisha zoezi la kuoanisha Sheria, Kanuni na Taratibu ili ziendane na matakwa ya Itifaki ya Soko la Pamoja. Hata hivyo, maelezo yaliyotolewa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, hayaoneshi kufanyika kwa shughuli hiyo. Zaidi ya hivyo, Mheshimiwa Waziri aliieleza Kamati kuwa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania ikiwemo zinashindwa kutumia fursa za Soko la Pamoja ipasavyo. Kwa taarifa hiyo, ni dhahiri hali hii ni ya mashaka kuhusu mafanikio ya Soko la Pamoja na jinsi Tanzania inavyoweza kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Shughuli za Bunge la Afrika Mashariki, Kamati ilijulishwa kuwa kwa kipindi cha mwaka 2012/2013, Bunge la Afrika Mashariki ililifanya Vikao vitatu vilivyojadili Miswada sita (6) na kupitisha Maazimio tisa (9). Mojawapo ya Miswada hiyo ni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(The East African Community Customs Management (Amendment) No.2)* wa Mwaka 2012. Muswada huu uliopitishwa mwezi Desemba, 2012, unalenga kuongeza kipindi cha miaka mitatu kuanzia Desemba 2012 hadi 31 Desemba, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii ya Bunge la Afrika Mashariki inathibitisha kuwa, hadi sasa suala la Forodha ya Afrika Mashariki halijakaa sawa. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali inapaswa kuendelea kujipanga vema na kuzingatia ipasavyo maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Kamati ilielezwa jumla ya shughuli kumi na tano zitakazopewa kipaumbele na Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Nyingi kati ya hizo, ni shughuli za kawaida za Wizara zinazotekelezwa kila mwaka wa fedha. Kati ya shughuli hizo, ipo shughuli ya kufanya uchambuzi, utafiti na tathmini mbalimbali kuhusu utekelezaji wa Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, shughuli hii ingefanyika vizuri zaidi kwa kuwa na Kitengo au Idara inayohusika na Utafiti. Kamati ilibaini kuwa muundo wa Wizara unahitaji kuwekwa vizuri zaidi ili tafiti muhimu na uchambuzi makini ufanyike ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli nyingine inayopangwa ni kuandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali kuhusu utekelezaji wa Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jambo hili ni muhimu kwa Taifa letu kuweza kunufaika katika mtangamano huu. Hata hivyo, taarifa haikuainisha aina wala mifano ya mikakati iliyowekwa badala yake lengo hilo linatajwa kwa ujumla. Kwa mantiki hiyo, Bunge litapaswa kufuatilia kwa karibu zaidi utekelezaji wa mikakati inayopangwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya matumizi, ili kutekeleza shughuli zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kamati ilielezwa kuwa Wizara hii inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tsh. 20,476,051,000/=. Kiasi hiki ni ongezeko la Sh.3,832,384,000/= ikilinganishwa na fedha iliyoidhinishwa na Bunge tarehe 3 Agosti, 2012. Uchambuzi ulionesha kuwa katika Kifungu 1003, Kasma 270200 (*Current Grant to International Organisation)* kuna kiasi cha Sh.12,452,253,440/= ambacho ni asilimia 61 ya Bajeti ya Wizara, kinaombwa kwa ajili ya michango ya Jumuiya. Maombi hayo yakilinganishwa na mwaka wa fedha 2012/2013 yameongezeka kwa Sh.1,810,680,440/- sawa na ongezeko la asilimia 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijulishwa kuwa Matumizi Mengineyo *(Other Charges)* ikiwemo fedha kwa ajili

ya kulipia michango ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, yanaombewa jumla ya Sh. 19,000,000,000/=. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kiasi hiki ni tofauti na mwaka 2012/2013 ambapo zilizoombwa Sh.14,853,533,800/-. Kamati ilipochambua makadirio hayo ilibaini kuwa ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa kiasi cha michango ya Jumuiya kutoka Sh.8,841,573,000/- zilizoidhinishwa na Bunge mwaka wa fedha 2012/2013 hadi Sh.12,452,253,440/- zinazoombwa mwaka wa fedha 2013/2014. Hili ni ongezeko la asilimia 41 katika michango ya Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati michango inaongezeka kwa asilimia 41, jumla ya makadirio ya matumizi kwa Wizara hii imeongezeka kutoka Sh.16,643,667,000/- kwa mwaka wa fedha 2012/2013 hadi Sh.20,470,051,000/- kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Hilo ni ongezeko la asilimia 23 katika Bajeti ya Wizara hii. Tofauti hiyo ya ongezeko katika michango ya Jumuiya na bajeti ya Wizara inaonesha kuwa gharama za uanachama wetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki imeongezeka bila kuzingatiwa ipasavyo katika mipango ya kunufaika na uanachama wetu katika Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri. Umuhimu na faida za Mtangamano wa Afrika Mashariki si jambo la kupuuzwa kwa namna yoyote. Hata hivyo, ni vema tukumbuke kuwa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, zinatofautiana kutokana na Muundo, Jiografia na Historia ya Mfumo wa Siasa, Uchumi na Utawala. Jambo hili halifuti umuhimu wa Mtangamano wa Afrika Mashariki. Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliwahi kusema kwenye kitabu chake cha *"Freedom and Unity".* Nanukuu:-

"We have to accept our differencies and accommodate them. There is no other way". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri isiyo rasmi, tunaweza kusema kuwa inabidi tuzikubali tofauti zetu na

twendenazo kama zilivyo, hakuna njia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo na kwa kuzingtia umuhimu wa mtangamano wa Afrika Mashariki Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Kasi ya kushughulikia Sera ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki iongezwe ili kuwezesha wadau muhimu nchini kuzingatia mambo ya msingi.

(ii) Mawasiliano na uhusiana baina ya Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika yanapaswa kuboreshwa.

(iii) Ili kuiwezesha nchi yetu kunufaika na mtangamo wa Afrika Mashariki, Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji kwa kila hatua ni jambo la kupewa uzito unaofaa. Serikali ihakikishe kuwa inaandaa mkakati husika kabla ya kuanza kutekeleza hatua yoyote ya Mtangamano. Kwa mfano, utekelezaji wa hatua ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki ungekuwa na tija zaidi kama mkakati husika ungeandaliwa mapema. Aidha, Wizara ihakikishe inawahusisha wadau muhimu katika hatua hii kadiri inavyowezekana.

(iv) Elimu kwa Umma itolewe kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kuzifahamu vema fursa zilizopo katika Soko la Pamoja.

(v) Serikali itumie uwezo walionao Watanzania kuwawezesha kupata ajira katika nchi nyingine wanachama. Aidha, kasi ya kuingia mkataba na nchi hizo kwa madhumuni hayo iongezwe. *(Makofi)*

(vi) Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, Sura ya Tanzania wawezeshwe kupata Taarifa mbalimbali za tafiti na uchambuzi kuhusu masuala ya ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

(vii) Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni jambo lenye

manufaa kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hata hivyo, muundo wa Wizara inayohusika usipowekwa vizuri itakuwa vigumu kuvuna fursa zilizopo. Kamati inashauri kuwa muundo wa Wizara hii uboreshwe na kuongeza Idara ya Utafiti.

(viii) Pamoja na Maoni na ushauri kuhusu umuhimu wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ni vema nchi Wanachama zifanye kazi ya ziada mbali na kuimarisha ushirikiano huo. Ni ukweli ulio wazi kuwa na ushirikiano si muarubaini wa matatizo ya watu wa Afrika Mashariki. Jambo lingine muhimu ni pamoja na juhudi za ndani ya kila nchi kuboresha maisha ya watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na ushauri huo, Kamati inatambua kuwa Bunge la Ulaya lilipitisha Azimio la Kusogeza mbele tarehe ya mwisho kwa nchi za *ACP* kusaini makubaliano ya *EPA* kutoka tarehe 1 Januari, 2014 hadi tarehe 2 Januari, 2016. Kamati inashauri kuwa pamoja na mabadiliko yoyote ya kubadilisha tarehe ya mwisho ya kusaini makubaliano hayo, bado kuna umuhimu mkubwa kwa nchi za Afrika Mashariki kuingia kwenye makubaliano kwa pamoja na si nchi moja moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Kwa kuhitimisha, naomba tena kukushukuru wewe binafsi kunipatia nafasi hii adhimu ili niwasilishe taarifa pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Ushirikiano wao wakati wa kupitia, Kujadili na Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Kwa kuthamini michango yao naomba kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mheshimiwa *Engineer*

Yussuf Hamad Masauni, Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Muhammad Ibrahimu Sanya, Mheshimiwa John Magale Shibuda na Mheshimiwa Anastazia James Wambura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Makatibu wa Kamati, Athuman Hussein, Ramadhani Issa na Nesta Kawamala kwa kufanikisha Taarifa hii kwa wakati. Nawashukuru pia watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Dokta Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuijadili pamoja na kuyakubali Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Fungu 97, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Masauni kwa mchango wako kwa niaba ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa nitamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kuhusu hoja iliyoko mbele yetu na ninamwona Mheshimiwa Raya, kwa hiyo, Mheshimiwa Raya, sasa unayo nafasi.

MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA AFRIKA MASHARIKI): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kutokana na muda, naomba Hotuba yangu ichukuliwe kama ilivyo katika kitabu ambacho kimewasilishwa Mezani kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika Mashariki imeundwa na Ibara ya 2(1) ya Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki kufuatia makubaliano ya wakuu wa nchi

wanachama wa Jumuiya hiyo ambazo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi. Aidha Ibara ya 8(3)(a) ya Mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki imezipa mamlaka nchi wanachama kuanzisha Wizara mahsusi, itakayoshughulikia masuala ya Afrika Mashariki. Kwa mujibu wa Ibara hiyo, Tanzania, ilianzisha Wizara ya Afrika Mashariki ambayo majukumu yake ni pamoja utekelezaji wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mikataba Midogo *(Protocols),* Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na Mazungumzo ya uundwaji wa Shirikisho la kisiasa la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mategemeo ya Watanzania kwamba Wizara hii ya Afrika Mashariki italitendea haki taifa hili, kwa kuwashirikisha wananchi kwenye kila hatua na kwa kusimamia kwa dhati na kikamilifu michakato yote ya mtangamano wa Afrika Mashariki, kwa maslahi ya nchi yetu, ili kuhakikisha kwamba Tanzania inanufaika vilivyo na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani kipindi hiki itajielekeza kwenye mambo machache ambayo tunaamini yakizingatiwa, Jumuiya ya Afrika Mashariki itakuwa imara na nchi zote wanachama watafurahia matunda ya Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya mafao ya Wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika 1977. Madai ya mafao ya wazee wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki sasa ni aibu kwa Taifa. Wastaafu hawa wameyumbishwa kiasi cha kutosha, wamepuuzwa kiasi cha kutosha, wamedhalilishwa kiasi cha kutosha na wameonewa kiasi cha kutosha na Serikali hii ya CCM inayojiita sikivu. Hakika laana ya wastaafu hawa wanaodhulumiwa haki yao waziwazi namna hii itaendelea kulitafuna Taifa hili kwa kwa miaka mingi ijayo kama Serikali haitawatendea haki wazee hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Jumuiya hiyo kuvunjika ghafla tarehe 30 Juni, 1977 ulizuka mgogoro wa

mgawanyo wa mali na madeni yake. Ili kuumaliza mgogoro huo, Umoja wa Mataifa uliiteua Benki ya Dunia kusuluhisha mgogoro huo. Benki ya Dunia ilimteua mtaalamu wake, Mwanadiplomasia, Dokta Umbricht (sasa marehemu) ambaye alifanikisha kuwanzishwa kwa Mkataba wa Kimataifa uliojulikana kama *"East African Community Mediation Agreement 1984"* kuhusu mgawanyo wa mali na madeni ya Jumuiya yakiwemo mafao ya wafanyakazi wa Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa tulizo nazo, kazi kubwa aliyofanya Msuluhishi huyu, Dokta Umbritch ilikuwa ni kuzigawanya fedha za pensheni na *provident funds* za Jumuiya kwa nchi tatu wanachama yaani Kenya, Uganda na Tanzania kulingana na idadi ya raia wake katika Jumuiya, kwa madhumuni ya kuwalipa mafao raia wake. Katika mgawo huo, Tanzania ilikabidhiwa paundi za Uingereza milioni 14 kwa ajili ya kulipa mafao ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili na wananchi wote fedha hizo zilitumika kufanyia nini kama walengwa hawakulipwa mafao yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za Kenya na Uganda tayari zilishawalipa wastaafu wa Afrika ya Mashariki stahili zao na hali huko ni shwari, lakini kwa Tanzania jambo hili limegubikwa na wingu zito la ufisadi kwa kuwa fedha ya kuwalipa wastaafu hao ilishatolewa. Kwa nini wastaafu hao hawakulipwa na wale waliolipwa, walipewa cheki za shilingi 10 na shilingi 130 za Kitanzania jambo ambalo ni aibu na fedheha kwa Serikali hii ya CCM inayojiita sikivu kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali hii ya CCM inayojiita sikivu, kutoa tamko leo, mbele ya Bunge hili kuhusu mafao ya wastaafu hao ili wajue moja, kama wanalipwa au hawalipwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali haitatoa tamko leo, kuhusu unyanyasaji wanaofanyiwa wastaafu wa

Afrika Mashariki, basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni italazimika kuleta Hoja Binafsi Bungeni kwa hatua za Kibunge kuhusu mafao ya wastaafu wa iliyokuwa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sarafu ya Pamoja. Katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Kambi Rasmi ya Upinzani ilinukuu sehemu ya hotuba ya Rais Jakaya Kikwete aliyoitoa wakati wa uzinduzi wa Bunge la Kumi tarehe 18 Novemba, 2010 kwamba mchakato wa kuanzisha Umoja wa Sarafu ulikuwa ukiendelea kwa kasi na kwamba ulikuwa unategemewa kukamilika mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuhoji hatua iliyofikiwa katika kuanzisha Umoja wa Sarafu kwa mwaka ule wa 2012/2013, Kambi Rasmi ya Upinzani vilevile iliitaka Serikali kulieleza Bunge kama ilikuwa imefanya utafiti wa kina juu ya suala hilo kwa kuwa tayari kulikuwa na mvutano katika nchi za Jumuiya ya Ulaya kuhusu kujiunga na umoja huo au kutojiunga nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro uliopo katika *"Euro Zone"* ni kwamba; pamoja na kuwa na sarafu moja ya "*Euro"* bado kuna nchi wanachama ambao wanaendelea kutumia sarafu yao, lakini pia kuna nchi nyingine zinaonekana kuwa mzigo katika umoja huo wa Euro kama ilivyo Ugiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 28 Aprili 2013, wakuu wa nchi za Afrika Mashariki, akiwemo Rais Kikwete walikutana Arusha na kuagiza pamoja na mambo mengine, kusainiwa kwa mkataba wa Sarafu ya Pamoja kabla ya mwezi Novemba 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaihoji Serikali kwa mara nyingine tena, hivi imefanya utafiti wa kina na kujiridhisha kwamba Umoja huu wa Sarafu hautakumbwa na dhoruba kama ilivyotokea kwa Umoja wa Sarafu wa nchi za Jumuiya ya Ulaya *(Eurozone)?* Pili, kwa kuwa

shilingi ya Tanzania imekuwa ikishuka thamani dhidi ya shilingi ya Kenya na Faranga ya Rwanda na kwa kuwa kuna tofauti kubwa za hali ya uchumi baina ya nchi wanachama huku Tanzania ikiwa nyuma ukilinganisha na nchi nyingine za Jumuiya: Je, kuna mkakati gani wa kuimarisha hali ya uchumi wetu ili tusiburuzwe katika Shirikisho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haipingi kuwa na Umoja wa Sarafu *(Monetary Union)*, lakini inataka kama Taifa, tuwe na maandalizi ya kutosha na tukidhi vigezo ili tusiwe mzigo au watumwa katika Umoja huo. Hii ni kwa sababu kila nchi mwanachama inataka kutumia fursa za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuimarisha uchumi wake wa ndani na kwa maana hiyo kama hatutakuwa na maandalizi ya kutosha, tutaishia kuwa soko la bidhaa za wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa angalizo kwa Serikali, isiharakishe kusaini mkataba wa Sarafu ya Pamoja. Serikali iweke nguvu zaidi katika kujenga uchumi wa ndani.

Serikali ikipuuzia ushauri huu, kuna kila dalili kwamba Tanzania itakuwa nyenzo ya kujenga uchumi wa nchi nyingine wanachama na yenyewe ikibaki kama mzalishaji wa malighafi ya kulisha viwanda vya wenzetu na kuwa soko la bidhaa zao kama ilivyokuwa enzi za ukoloni. Jambo hili likitokea ni kwamba matumaini ya Kauli Mbiu ya Serikali ya Tanzania ya "Maisha bora kwa kila Mtanzania" itakuwa imezikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wa Afrika Mashariki. Katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii mwaka 2012/2013, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilishtushwa sana na maamuzi mazito yanayofanywa, sheria mbalimbali zilizotungwa na maridhiano na mikataba mbalimbali inayofanywa na Bunge la Afrika Mashariki bila Bunge letu kuwa na taarifa yoyote. Miongoni mwa mikataba iliyoridhiwa na Bunge la Afrika Mashariki na sheria mbalimbali zilizotungwa bila Bunge letu kuwa na taarifa rasmi ni kama ifuatavyo:-

(i) Jumuiya ilisaini mkataba na Jumuiya ya wafanyabiashara wa Uturuki chini ya umoja unaojulikana kama *"Africa-Turkey Partinership"* mkataba ambao ulitegemewa kuingiza zaidi ya dola za kimarekani 350 bilioni kutokana na biashara mbalimbali.

(ii) Uandaaji wa Sheria ya Kuthibiti Uhalifu wa Kimtandao *"Cyber Laws".*

(iii) Uandaaji wa Itifaki ya Pamoja kuhusiana na kuwa na Kituo Kimoja cha Utalii *"Single Tourist Destination Protocol"* na uwepo wa Hati ya Kusafiria na Visa Moja ya Utalii *"Single Tourist Visas"* kwa nchi wanachama wa Jumuiya.

(iv) Kuandaa mfumo mmoja wa mitaala ya elimu ili kuweza kukidhi haja ya Soko la Pamoja la ajira la Jumuiya.

(v) Kusainiwa makubaliano ya pamoja *(MoU)* juu ya ushirikiano wa masuala ya kiulinzi.

(vi) Kuanzishwa kwa Umoja wa Wafanyabiashara wa Samaki Ukanda wa Ziwa Viktoria *"The Lake Victoria Fisheries Organization" (LVFO)* ambacho ni chombo chenye mamlaka juu ya usimamizi wa shughuli zote za uvuvi katika Ziwa Viktoria.

(vii) Kuandaliwa kwa Miswada mbalimbali ya Sheria ambayo inasubiri kupitishwa kuwa sheria: Miswada hiyo ilikuwa ni:-

- *The East African Community Human and Peoples' Rights Bill, 2012;*
- *The East African Legislative Assembly Elections Bill, 2011;*
- *The East African Customs Management (Amendment) Bill, 2012;*

- *The East African Community Trans-Boundary Ecosystems Management Bill, 2010;*

- *The East African Community Polythene Materials Control Bill, 2011;*

- *The East African Community Elections Bill, 2012;*

- *The Administration of the East African Legislative Assembly Bill, 2011; na*

- *The East African Parliamentary Institute Bill, 2011.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani iliona kwamba ni busara mambo haya yakawa wazi kwa Bunge letu na kwa wananchi wote pia, kwa kuwa ni maamuzi na sheria ambazo zitakuwa na athari ya moja kwa moja kwa nchi yetu kama vile kusimamia chaguzi zetu, Majeshi yetu, rasilimali zetu kama samaki wa Ziwa Viktoria, utalii, elimu yetu na maisha yetu kwa jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia uzito wa jambo hili na ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata taarifa muhimu na kushiriki kikamilifu kila hatua katika michakato mbalimbali ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kambi ya Upinzani Bungeni, ilipendekeza mambo yafuatayo:-

(i) Kuundwa kwa Kamati Mpya ya Kudumu ya Bunge ya Afrika Mashariki ambayo itakuwa inapokea na kujadili Miswada, Itifaki na mwenendo mzima wa Jumuiya na iwe na wajibu wa kutoa taarifa yake kwenye vikao vya Bunge mara kwa mara ili Bunge letu liweze kuzijadili na kuishauri Serikali kikamilifu. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilishauri Kamati hiyo iwe na jukumu la kushughulikia nidhamu ya Wabunge wa Afrika Mashariki.

(ii) Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pia ilipendekeza pawepo na vikao vya pamoja baina ya Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki wanaotoka Tanzania na Kamati ya Afrika Mashariki (itakayoanzishwa) ili kuweza

kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusiana na utendaji wao wa kazi na masuala mbalimbali ya Jumuiya.

(iii) Vilevile Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza uwepo utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na kila hatua ambayo imefikiwa kuelekea kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki ili kuepusha kuwa na Jumuiya ya viongozi peke yao na badala yake iwe ni Jumuiya ya wananchi kwani watakuwa na taarifa za kina kuhusiana na kila hatua iliyofikiwa.

(iv) Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pia ilipendekeza kuwa, kabla ya Itifaki mbalimbali kuridhiwa na Bunge la Afrika Mashariki, ni vema Wabunge wa Afrika Mashariki wakishirikiana na Wizara ya Afrika Mashariki kuziwasilisha Itifaki hizo, kwenye Bunge letu ili ziweze kujadiliwa na kupitishwa au kukataliwa na Bunge kama ambavyo tumekuwa tukifanya kwa Maazimio, Mikataba na Itifaki za Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Afrika Mashariki alikubaliana na mapendekezo haya wakati akifanya majumuisho ya hoja yake ya bajeti ya Wizara ya Afrika Mashariki 2012/2013. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inachotaka kujua sasa ni hatua gani imefikiwa katika utekelezaji wa mapendekezo hayo? Aidha, tunatambua kuwa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje ndio imekuwa na jukumu la kusimamia masuala yote yahusuyo Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Kwa mujibu wa Ibara ya 50 ya mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mabunge ya nchi wanachama wana haki ya kuchagua Wabunge wa wa Bunge la Afrika Mashariki.

Aidha, Ibara hiyo imeelezea utaratibu wa jinsi ya kuwapata Wabunge hao kuwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa Wabunge hao wanawakilisha makundi mbalimbali kama vile uwiano wa vyama vya siasa vyenye uwakilishi Bungeni, jinsia na makundi mengine maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Ibara hiyo ya 50(1) kutoa haki kwa Mabunge ya nchi wanachama kuweka utaratibu wa kufuatwa katika kuwachagua Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, jambo hili limetoa mwanya kwa kila nchi kuweka utaratibu wake wa ndani ambao hauheshimu Ibara hii kama ambavyo Tanzania na Uganda walivyofanya, kwa kuhakikisha kuwa vyama vikuu vya Upinzani katika Mabunge yao, yaani CHADEMA kwa Tanzania na *FDC* kwa Uganda hawana uwakilishi, pamoja na ukweli kuwa ndio vyama vya upinzani vyenye Wabunge wengi kwenye Mabunge ya nchi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuwasilisha mapendekezo ya mabadiliko ya vifungu vya mkataba kwenye Jumuiya na kuweka kifungu cha adhabu ya moja kwa moja kwa nchi mwananchama ambayo kwa makusudi anakiuka baadhi ya Ibara za mkataba huu ili liwe fundisho kwa kila mmoja kuheshimu mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tunataka pawepo na utaratibu wa kufanana katika Jumuiya linapokuja zoezi la kuchagua Wabunge hao katika nchi wanachama ili kuondoa udhaifu wa Mabunge husika kutokutenda haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuitaka Serikali kutekeleza mapendekezo haya, bado Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba uwakilishi wa Bunge la Afrika Mashariki kwa wananchi ni mdogo sana au pengine haupo kabisa.

Kimsingi Bunge la Afrika Mashariki linawakilisha Mabunge ya nchi wanachama ambayo ndiyo yaliwapigia kura Wabunge wa Afrika Mashariki.

Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inakubaliana na Ripoti ya Rimu ya Wataalamu ya Oktoba 2011 *(Report of the team of Experts on addressing the Fears, Concerns and Challenges of the East African Federation)* kuhusu hofu na

changamoto za kujiunga na Shirikisho la Afrika Mashariki kwamba Wabunge wa Afrika Mashariki wawe wanachaguliwa na wananchi moja kwa moja; hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri utaratibu huo ufanyike tutakapokuwa kwenye Shirikisho kamili la kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu na changamoto za kujiunga na Shirikisho la Afrika Mashariki. Kwa mujibu wa taarifa ya timu ya wataalamu juu ya kutoa ufumbuzi wa hofu na changamoto zinazozikabili nchi wanachama katika kuelekea Shirikisho la Kisisasa la Afrika Mashariki ya Oktoba, 2011, ni kwamba, pana hofu kubwa miongoni mwa wananchi wa nchi wanachama kuhusu mchakato wa kuingia kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki kwa sababu mbali mbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupoteza mamlaka ya dola kwa nchi husika. Taarifa ya wataalamu inaweka bayana kwamba ili Shirikisho la kisiasa liwepo lazima kutakuwa na kupotea kwa kiwango fulani cha mamlaka ya dola *(sovereignty)* lakini taarifa hiyo inashauri kwamba watu waangalie mbele ya pazia la "upofu wa mamlaka" *(beyond the curtain of power blindness)* na kuona faida na fursa nyingi zitakazopatikana kutokana na Shirikisho hilo. Ili kuondoa hofu hii, Jumuiya ya Afrika Mashariki inashauriwa kukamilisha kwa ufanisi Itifaki na michakato yote ya mwanzo kuelekea kwenye Shirikisho, ili nchi wanachama weweze kuona faida halisi *(tangible benefits)* za Jumuiya kwa hali ilivyo sasa, ili kuwaondolea nchi wanachama na wananchi wao woga wa kuingia katika Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili kwamba Tanzania imenufaika kwa kiasi gani kwa hatua ya sasa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuwaondolea hofu wananchi ya kuingia katika Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine yaliyotajwa kuleta hofu miongoni mwa wananchi wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kuelekea

kwenye Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki, ni pamoja na mfumo wa Utawala *(governance)* baada ya shirikisho. Taarifa hiyo ya Timu ya Wataalamu ilishauri kwamba ili kuondoa hofu hiyo kila nchi mwanachama iandae 'utaratibu wa kikatiba' wa kutambua maandalizi ya Shirikisho hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa mchakato wa kupata Katiba Mpya unaendelea ila tunasikitishwa na kitendo cha Serikali kutokuitoa ripoti hii mapema ili wananchi waweze kuelimishwa kuhusiana na pendekezo hili katika kutoa maoni yao kwa Tume ya Katiba.

Aidha, tunaitaka Wizara na Serikali kulielieleza Bunge hili, imewaelimisha wananchi kwa kiwango gani ili kutoa maoni juu ya mfumo wa utawala wa Shirikisho la Afrika Mashariki katika mchakato wa Katiba Mpya unaoendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu ya kukosa ajira kutokana na mitaala na viwango tofauti vya elimu na taaluma. Taarifa ya timu ya wataalamu imebaini kwamba tofauti ya mitaala ya elimu na viwango vya ubora wa elimu miongoni mwa nchi wanachama za Jumuiya ya Afrika Mashariki imesababisha kutokuwa na uwiano na fursa sawa za ajira hasa kwa nchi ambazo zina uwezo mdogo wa rasilimali watu, jambo ambalo linalowatia hofu wananchi wa nchi hizo kuingia katika Shirikisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondokana na hofu hiyo, Jumuiya ya Afrika Mashariki imeshauriwa kwamba ianzishe uratibu wa kuwa na mitaala ya elimu inayofanana ili kuondoa ubaguzi wa vigezo vya kielemu katika fursa za ajira katika Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ilipendekeza katika bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha unaomalizika 2012/2013 kuhusu kuanzishwa kwa mfumo mmoja wa Elimu Afrika Mashariki ili kuondoa ubaguzi kutokana na tofauti ya mitaala na viwango vya ubora wa elimu katika fursa za ajira.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza kuwa kuwe na mfumo wa pamoja wa udahili kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, ili mwanafunzi mwenye sifa ya kujiunga na chuo kikuu awe na uhuru wa kuchagua chuo chochote ndani ya Jumuiya Afrika Mashariki na adhaminiwe na Bodi ya Mikopo kutoka nchini mwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali hii ya CCM kulieleza Bunge hili kuwa imefanya jitihada zipi ikishirikiana na nchi wanachama kuanzisha mfumo mmoja wa elimu ili kuwaondolea hofu wananchi wetu kuhusu unyanyapaa katika ajira unaotokana na tofauti za kielimu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Serikali kuhimiza Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki *(The East African Universities Council)* liwezeshwe ili liweze kuendesha udahili kwa wanafunzi wanaotaka kujiunga na chuo kikuu chochote katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuwa kiungo kati ya Tume za Vyuo Vikuu na Bodi za Mikopo za nchi wanachama ili kuwawezesha wanafunzi wa vyuo vikuu katika Jumuiya kupata elimu kwa uhuru na bila bugudha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya biashara na uwekezaji. Katika jitihada za kukuza uchumi wa nchi yetu, Tanzania inajitahidi kuvutia wawekezaji wa nje. Ili kufikia malengo ya kuvutia wawekezaji wengi kadiri iwezekanavyo, Serikali inatoa motisha mbalimbali ikiwemo misamaha ya kodi. Hata nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki halikadhalika zinafanya vivyo hivyo kwa mantiki hiyo, kunakuwa na ushindani mkubwa baina ya nchi wanachama wa Afrika Mashariki kutoa misamaha ya kodi kwa wingi ili kuwavutia wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japo kanuni za uchumi wa kisasa zinaongozwa na nguvu ya soko ambayo msingi wake ni ushindani katika ubora wa bidhaa na huduma, Kambi Rasmi ya Upinzani haioni wala haishawishiki kama ushindani katika kutoa misamaha ya kodi una tija katika kujenga

uchumi imara. Hii ni kwa sababu rahisi kabisa kwamba: “ni ushindani unaopoteza mapato”.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo ni kwamba Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi kwa pamoja zinapoteza Dola za Kimarekani bilioni 2.8 kila mwaka kutokana na mashindano ya msamaha wa kodi ili kuvutia wawekezaji.

Kambi Rasmi ya Upinzani haiungi mkono jambo hili kwani ni mashindano ya kuwania nafasi ya kwanza ya kuwa maskini na fukara zaidi jambo ambalo halikubaliki kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondokana na hasara hii kubwa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuanzishwa kwa Kituo cha Uwekezaji cha Afrika Mashariki *(The East African Investment Center)* kitakachoratibu viwango vya motisha wa kodi *(tax incentives)* kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuweka uwiano wa viwango hivyo na kuepusha upotevu wa mapato kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki, ni taasisi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya zamani ambayo haikuvunjika wakati Jumuiya hiyo ilipovunjika mwaka 1977. Pamoja na kuendelea na shughuli zake kwa muda mrefu, benki hii haionekani kama ina nguvu kiuchumi na mchango wake katika maendeleo ya kiuchumi ya Afrika Mashariki hali kadhalika hauonekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ya Tanzania kuzishawishi nchi wanachama kuwekeza katika benki hii kwa kuichangia fedha na kuiombea mikopo kutoka Benki ya Dunia au Shirika la Fedha Duniani ili kuipa nguvu benki hii na kuifanya iweze kutoa mikopo ya riba nafuu kwa nchi wanachama na pia kugharamia miradi ya maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee kuhusu utalii kwa pamoja.

Kwa kuwa, kumekuwa na malalamiko mengi toka kwa makampuni ya utalii na hata kwa watalii wenyewe kutokana na kulipa pesa nyingi kwa ajili ya viza za kutoka nchi moja na kuingia nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa madhumuni ya utalii;

Na kwa kuwa, kutokana na tatizo hilo watalii wengi wanachagua kufanya utalii wao Kenya zaidi kwa kuwa kuja Tanzania kutawalazimu kulipa gharama zaidi za viza jambo ambalo linaikosesha Tanzania mapato yatokanayo na utalii;

Na kwa kuwa, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilishaanza mchakato wa kuandaa Itifaki ya Pamoja ili kuwa na Kituo Kimoja cha Utalii *(Single Tourist Destination Protocol)* na uwepo wa Hati ya Kusafiria na Viza Moja ya Utalii *(Single Tourist Visas)* kwa nchi wanachama wa Jumuiya;

Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhimiza ukamilishaji wa haraka wa mchakato huo wa kuwa na utalii wa pamoja ili kuondoa adha iliyopo sasa hivi ya watalii kutembelea nchi moja zaidi na nyingine kukosa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara haramu ya pembe za ndovu katika ukanda wa Afrika ya Mashariki inakuwa kwa kasi sana jambo ambalo linatishia kutoweka kabisa kwa wanyama hao ambao ni kivutio kikubwa cha utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa katika mtandao wa habari wa *"Annamiticus" (www.annamiticus.com)* zinasema kwamba mwaka jana 2012, makontena mawili kutoka Kenya na Tanzania yalikamatwa huko *HongKong* yakiwa yamebeba tani nne (Kilo 4,000) za pembe za ndovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa hiyo, kontena lililotoka Tanzania lilikuwa limeandikwa *"plastic*

scrap" ikimaanisha kuwa lilikuwa na vifaa ya plastiki lakini baada ya kufunguliwa kulikuwa na vipande 972 vya pembe halisi za ndovu zenye uzito wa kilogramu 1,927 pamoja na kilo moja na nusu ya unga wa pembe za ndovu zilizosagwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kontena lililotoka Kenya lilikuwa limeandikwa *"roscoco beans"* yaani maharage aina ya *roscoco,* lakini lilipofunguliwa kulikuwa na vipande 237 vya pembe za ndovu sawa na kilogramu 1,884.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa hiyo, wingi wa pembe hizi za ndovu zilizokamatwa, unadhihirisha kwamba tembo 600 kwa uchache waliuwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi uliopita kontena lingine limekamatwa lililosheheni pembe za ndovu 113 huko China zenye thamani ya Dola za Kimarekani 400,000, Kontena hili liliandikwa kwamba limebeba vipuri *(spareparts)* toka Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Burundi haina bandari, kuna uwezekano mkubwa kwamba kontena hilo lilipitia bandari ya Tanzania na hivyo kuna uwezekano pia kwamba pembe hizo zinatokana na tembo waliouwawa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua kama Serikali ya Tanzania imefanya mawasiliano na Serikali ya Burundi ili kujua ukweli kuhusu kontena lililosheheni pembe za ndovu lililokamatwa huko China. Hii ni kwa kuzingatia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(The Strategy for Regional Peace and Security)* wa kubadilishana taarifa za uhalifu na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna Watanzania walioshutumiwa na kusutwa kuhusika na mtandao huu wa biashara hii haramu ya pembe za ndovu akiwemo Katibu Mkuu wa CCM, Ndugu Abdulrahman Kinana na kwa kuwa

Serikali ya Tanzania inaonekana dhahiri kumtetea na kumlinda mtu huyu na kwa kuwa ni kiongozi mkubwa wa Chama Tawala, kama alivyofanya Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi alipokuwa anatoa mchango wake kwenye bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii mnamo tarehe 30.04.2013. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tembo wengi wa Afrika Mashariki wanazidi kupotea kila siku kutokana na biashara hii haramu ya pembe za ndovu jambo ambalo linaikosesha Jumuiya ya Afrika Mashariki mapato yatokanayo na utalii hivyo kuiweka hatarini sekta ya utalii ya Afrika Mashariki; na kwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi alipokuwa anachangia hotuba ya Maliasili na utalii na kwa mujibu wa Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)* alisema kuwa kesi Na. 3 na 4 ya mwaka 2009 kuhusu pembe za ndovu na meli iliyokamatwa *Vietnam* iliyokuwa Mahakama ya Kisutu ilifutwa kutokana na Tanzania kutokuwa na mkataba wa kubadilishana wahalifu na Vietnam na hivyo kukosekana kwa ushahidi Mahakamani, *Hansard* ya tarehe 30.04.2013, ukurasa 141.

Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inamtaka Mwendesha Mashtaka wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kumfungulia mashtaka ndugu Abdulrahman Kinana katika Mahakama ya Afrika Mashariki kwa madhumuni ya kuubaini na kuudhibiti mtandao wa majangili na wafanyabiashara haramu ya pembe za ndovu katika ukanda huu wa Afrika ya Mashariki kutokana na meli anazosimamia kama wakala wa meli mojawapo kukamatwa na shehena za pembe za ndovu huko *Vietnam* mwaka 2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tunaitaka Serikali iombe msaada kutoka nchi mwanachama ya Kenya ambayo ina Ubalozi wa *Vietnam* ili kurahisisha upatikanaji wa ushahidi badala ya kutegemea Ubalozi wetu ulioko China kama ilivyosemwa na hivyo kesi hii iweze kuendelea ili wahujumu hawa wa uchumi na washirika wao waweze kuhukumiwa kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuru wa vyombo vya habari Afrika Mashariki. Sasa hivi kumezuka wimbi la kukandamiza uhuru wa habari katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Matukio ya kuvifungia vyombo vya habari na kuwadhuru Waandishi wa Habari kwa sababu za kulinda maslahi ya watawala yanazidi kuongezeka kwa kasi kubwa katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Utangazaji la Uingereza *(BBC)* ya tarehe 20 Mei, 2013, Rais Yoweri Museveni wa Uganda ameamuru kufungiwa kwa gazeti la kila siku la nchi hiyo la *"The Daily Monitor"* na gazeti lingine la *"Red Pepper"* kwa kuchapisha habari iliyofichua njama za Rais Museveni za kumuandaa mtoto wake Muhoozi Kainerugaba ambaye ni Brigedia wa Jeshi la nchi hiyo kuwa Rais wa nchi hiyo baada ya yeye kuondoka madarakani.

Katika sakata hilo hilo, redio mbili za Dembe *FM* na *KFM* zilivamiwa na Askari Polisi zaidi ya 50 wenye silaha na kuamrisha kufungwa kwa vituo hivyo kwa madai kwamba vipo katika eneo moja na ofisi za magazeti yaliyofungiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania hakuna asiyejua jinsi tasnia ya habari inavyodhibitiwa ili kulinda maslahi ya wakubwa. Licha ya kufungia gazeti la kiuchunguzi la Mwanahalisi kwa muda usiojulikana kwa kusema ukweli, Watanzania pia wameshuhudia Waandishi wa Habari wakitekwa, kuteswa na hata kuuwawa huku Serikali ikiwaachia huru baadhi ya maafisa wake walioshiriki katika unyama huo wakiendelea na kazi katika ofisi za Serikali. Jambo hili limeichafua taswira ya nchi yetu mbele ya Jumuiya na mbele ya ulimwengu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio haya ya kufungiwa na kuumizwa na kuuwawa kwa Waandishi wa Vyombo vya Habari ndani ya Jumuiya ya Afrika yasiposhughulikiwa sasa,

yataongeza hatari na hofu ya wananchi kutoka nchi wanachama na hivyo kupinga kuingia katika Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali na Wizara hii kulieleza Bunge na Watanzania nini kauli yake na msimamo wake kuhusiana na suala la uhuru wa vyombo vya habari na usalama wa Wanahabari ndani ya Jumuiya hii ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapendekeza kuwa kutokana na tishio hili la uhuru wa habari na Wanahabari katika nchi wanachama wa Jumuiya ni vyema sasa tukawa na Itifaki ya Pamoja "*Protocol*" na sheria moja ya kusimamia uhuru na haki ya kupata habari ndani ya Jumuiya ili kuzuia Serikali na viongozi wasiopenda kukosolewa ndani ya Jumuiya kuwa na haki ya kuvifungia vyombo vya habari kwa kutumia sheria kandamizi za nchi wanachama, hii ni hatua muhimu sana katika kuelekea kwenye Shirikisho la Afrika ya Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki mbalimbali za ushirikiano wa Kikanda. Bila shaka wananchi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wanataka kuona matunda ya ushirikiano na sio kuona utitiri wa taasisi na itifaki mbalimbali zinazoanzishwa bila mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri wa Afrika Mashariki ya mwaka 2012/2013 ilitaja itifaki na mikakati kadhaa ya ushirikiano wa kikanda. Itifaki na mikakati hiyo ni pamoja na Mkakati wa Kikanda wa Kusimamia Amani na Usalama, Uwianishaji wa Shughuli za Kipolisi, Kupambana na Madawa ya Kulevya, Mapambano dhidi ya Ugaidi, Itifaki ya Amani na Usalama, Itifaki ya Ushirikiano katika Ulinzi, Mazoezi ya Pamoja ya Kijeshi na Ushirikiano katika Siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utitiri huu wa Mikakati na Itifaki, bado Afrika ya Mashariki imekuwa mhanga *(victim)* mkubwa wa matukio ya kigaidi, biashara haramu ya madawa ya kulevya, biashara haramu ya pembe za

ndovu. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua kama Itifaki na Mikakati hiyo ina nia ya dhati ya kukabiliana na matatizo yaliyotajwa au ni miradi ya ulaji ya wakubwa na kuanzisha nafasi za ajira kwa watoto wa wakubwa bila ufanisi wa vyombo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Sheria katika Jumuiya. Shirikisho la Afrika Mashariki limesababisha mwingiliano wa kijamii katika nchi wanachama kwa kiwango kikubwa ambapo raia wa nchi wanachama wana fursa ya kuoana na kuanzisha familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo linaloibuka katika mahusiano haya ni kwamba hakuna utaratibu wa utekelezaji wa hukumu iliyotolewa katika nchi moja mwanachama katika nchi nyingine mwanachama kuhusu masuala ya ndoa, talaka wala malezi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Sheria ya Utekelezaji wa Hukumu katika nchi jirani *(The Judgement Extension Act)* haihusishi hukumu zinazohusu mambo ya ndoa, talaka wala malezi ya watoto na hivyo kutoa wakati mgumu kwa wananchi wanapotaka kukazia hukumu kwenye nchi wanachama za Kenya na Uganda. Mbaya zaidi ni kwamba, sheria hiyo haina kabisa mamlaka katika nchi nyingine wanachama za Jumuiya kama vile Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, imepelekea wananchi katika nchi wanachama kukosa haki zao na hasa kuhusiana na mambo ya ndoa, malezi na hata haki za watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapotokea kuwa mzazi mmojawapo anatokea nchi nyingine na wanapokuwa ama wamekosana na kutalikiana na mmojawapo kuamua kurejea kwenye nchi yake, zile haki za mhanga zinakuwa zimepotea ama kuishia hapo, kwani hawezi kwenda kukazia hukumu huko kwa mujibu wa sheria na hii imeleta usumbufu mkubwa sana kwa wananchi wetu waliooa ama kuolewa katika nchi wanachama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwana CHADEMA inataka kujua Serikali na Wizara ina mpango gani wa kuondoa utata huu wa kisheria ili haki za kifamilia ziweze kulindwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge...

MWONGOZO WA SPIKA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Mwongozo, Mheshimiwa Lukuvi!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba radhi, nasimama kwa Kanuni ya 68. Sikutaka kumsimamisha Ndugu yangu Raya, namheshimu sana maana ningembabaisha, *speech* hii alikuwa ameandikiwa, ingemsumbua kidogo. Kwa hiyo, nilitaka amalize kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka Mwongozo wako, wasifikiri namzungumzia Kinana, simzungumzii Kinana kwa sababu hizi porojo tumeshazisikia siyo za kweli lakini nachotaka mimi kuzungumzia ni juu ya ukiukwaji wa makusudi na wa kila mara wa wa Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kanuni yetu ya 64(1)(e) inatukataza sisi Wabunge kuzungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Bunge, Jaji. Sasa leo tumekwenda zaidi kuzungumzia Rais jirani yetu Museveni kwa mambo ambayo mtu mmoja anasema...

KUHUSU UTARATIBU

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kuhusu Utaratibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE): ...amesikia kwenye *radio.*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mnyika naomba uketi chini.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha kwamba tunakatazwa kuzungumzia mwenendo wa Rais lakini pia Kanuni zetu zinatukataza vilevile kutumia majina ya viongozi kama Marais kwa dhihaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Bunge hili la Tanzania ni la watu waungwana na tunajua kwamba Rais Museveni ni Rais. Bunge hili linakataza kuzungumza mwenendo wa Rais lakini kibaya zaidi ni kwamba taarifa zenyewe ni za mtu mmoja kasikia kwenye *radio* leo tunakuja kumzungumza Rais Museveni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na zile za Kinana ambazo tulishasema tumeshajibu lakini wacha aendelee kujifurahisha lakini nataka kusemea hili, unawezaje kutumia Kiti chako, naomba utumie Kiti chako kukemea tu tabia hii iliyozoeleka ya kukiuka Kanuni kwa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Museveni anajua Kiswahili na ni Rais jirani na haya mambo yametokea kwenye *radio,* hatuna uhakika nayo lakini Kanuni zetu zinatukataza kuzungumzia Rais wa kwetu sembuse Rais wa *East Africa* jirani yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama inawezekana ukemee tu, maana tukisema afute haina maana lakini ukemee tu vitendo hivi ambavyo vinazoeleka kila mara. *(Makofi)*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu!

MWENYEKITI: Kuhusu Utaratibu, Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 63(2), nataka kumwelekeza Mnadhimu wa Serikali juu ya utaratibu kwamba Kanuni hii inatamka maneno yafuatayo:-

"Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni hatachukuliwa kuwa anasema jambo la uwongo iwapo anafanya rejea ya habari kuhusu jambo fulani lililotangazwa au lililoandikwa kwenye vyombo vya habari". (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari inayohusu Museveni iliyoandikwa kwenye hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani imenukuliwa kutoka chombo cha habari cha *BBC. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka vilevile kumwelekeza tu utaratibu wa Kanuni ya 64(d) kwamba Kanuni hii...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika kwa mujibu wa Kanuni zetu unaruhusiwa kuzungumzia jambo moja la Kikanuni unaposimama na jambo hilo moja la Kikanuni ulilotaka kulisema umeshalisema na umesema unamjibu Waziri wa Nchi, ni lile la Kanuni ya 63(2) ambayo inasema kwamba:-

"Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni hatachukuliwa kuwa anasema uwongo iwapo anafanya rejea ya habari kuhusu jambo fulani lililotangazwa ama lililoandikwa na vyombo vya habari".

Nianze tu moja kwa moja na Mwongozo wako, Mheshimiwa Mnyika, Waziri wa Nchi ameomba Mwongozo kwa Kiti, hakuomba Mwongozo kwa Mbunge. *(Makofi)*

Sasa Waziri anapoomba Mwongozo kwa Kiti halafu Mbunge anasimama anatoa Mwongozo badala ya Kiti, hiyo kwanza ni kukidharau Kiti kwamba kimeshindwa kutoa Mwongozo. *(Makofi)*

Mimi nilikuwa bado hata sijasimama hapa kujibu Mwongozo aliouomba Waziri, tayari wewe unaomba Mwongozo wa kujibu alichoulizwa Kiti.

Kwanza, nianze na utaratibu huo kwamba, unapoomba Mwongozo, wewe ungengoja mimi nitoe Mwongozo wangu na wewe ungeomba Mwongozo wa kitu kilichokiukwa kwa utaratibu ambao upo. *(Makofi)*

Pili, Waziri wa Nchi wakati akiomba Mwongozo hakusema kwamba Msomaji wa Kambi ya Upinzani amesema uongo.

Sasa wewe unapojibu, unataka kudhihirisha kwamba kile kilichosemwa na Msemaji wa Upinzani ni kweli kwa mtazamo na kwa Kikanuni, lakini Mwongozo ulioombwa na Waziri wa Nchi, hakusema kwamba kuna jambo la uongo lilosemwa. Yeye ameomba Mwongozo kwenye Kanuni nyingine kabisa katika Kanuni hizi zilizomo kwenye Kanuni zetu. *(Makofi)*

Kuhusu Mwongozo wa Mheshimiwa Mnyika hakuniomba mimi, amekiuka Mwongozo pia kwa kukijibia Kiti badala ya kusema jambo ambalo alifikiri lipatiwe majibu. *(Makofi)*

Nikirudi kwenye Mwongozo wa kwanza wa Mheshimiwa Waziri, jambo hili alilolisema ni jambo zito na lina maneno mazito ambayo yanahusu viongozi wakubwa katika nchi zetu ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sasa unaponiomba nikemee, nafikiri hata mimi nisikemee bila kujua maneno mazito ya kutumia katika kukemea hili.

Kwa hiyo, ili nipate maneno yanayolingana, ya kukemea ya Kimwongozo, naomba Mwongozo huu niuahirishe na utengenezwe kwa utaratibu unaotakiwa kwa

kuzingatia busara na hekima za wataalam wetu mbalimbali ndani ya Bunge wanaotuongoza katika mijadala yetu hapa ndani.

Basi, Mwongozo huu nitautolea majibu pale nitakapoona kwamba sasa suala hili limekaa sawasawa kwa kuzingatia haya niliyoyazungumza na Kanuni ambayo inajuhusisha na suala ulilosema. *(Makofi)*

Baada ya kumaliza kujibu miongozo hiyo, muda wetu ni mdogo, lakini naomba tu kwa heshima ya kikao hiki cha leo, Wabunge wa Afrika Mashariki wako hapa ndani, yupo Mheshimiwa Adam Kimbisa, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, Mheshimiwa Shyrose Banji, Mheshimiwa Bernard Marunya, Mheshimiwa Twaha Tasilima, Mheshimiwa Abdullah Mwinyi na Mheshimiwa Angela Kiziga. Tunawakaribisha sana katika shughuli zetu za leo. *(Makofi)*

Ninapomaliza kusema hayo, naomba sasa nitangaze rasmi kwamba sitaruhusu tena miongozo. Tunapoteza muda, muda ni mfupi kwenye Wizara hii.

Sasa naomba nimwite mchangiaji wetu wa kwanza ambaye ni Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni, atafuatiwa na mchangiaji wetu wa pili, kwa mujibu wa taarifa nilizonazo hapa Mezani atachangia Mheshimiwa Mohamed Mnyaa badala ya Mheshimiwa Haji Hatibu Kai. Kwa utaratibu huo naomba, nimwite mchangiaji wa kwanza.

MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia fursa hii ya kwanza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze na msemo wa wahenga ambao unasema, ukimwona mtu anatapatapa ujue ameshikwa pabaya.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Katibu Mkuu Kinana chapa kazi, leo hii tunaendelea kuzihirishiwa jinsi ulivyo tishio na wewe tunaamini ni jembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana falsafa na wachumi waliobobea wanaamini juu ya umuhimu wa ukubwa wa soko katika kuchangia maendeleo ya nchi. Kwa hiyo, mimi naamini kabisa kwa Mtangamano huu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao unatupatia fursa ya soko kubwa zaidi, utaweza sana kusaidia kuimarisha uchumi wa nchi yetu na kuweza kuhakikisha kwamba wajasiriamali, wawekezaji wana-*achieve economy of scale* kwenye uzalishaji, lakini pia bidhaa zetu zinashuka baadaye pamoja na kuimarika kwa ubora wa bidhaa hizo na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la msingi la kujiuliza. Je, kwa hatua ambayo tayari tumefikia, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amezungumza vizuri sana kwamba tumeshapiga hatua katika masuala mawili makubwa, Soko la Pamoja na Ushuru, wanaita *Custom Union*. Suala la msingi la kujiuliza, nchi yetu sisi kama Watanzania au kama Tanzania ni kwa kiwango gani tumeweza kufaidika na fursa za Soko hili kubwa la Pamoja la Afrika Mashariki, hasa katika maeneo matatu makubwa, eneo la biashara, eneo la uwekezaji na eneo la ajira. Changamoto gani ambazo tumekabiliana nazo na mikakati ya kuweza kuepukana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba mchango wangu uelekee katika maeneo hayo. Kwanza, eneo la Afrika Mashariki kwa ujumla wake, ni vipi Serikali yetu kupitia Wizara hii pamoja na wawikilishi wetu katika Bunge la Afrika Mashariki walivyoweza kushiriki kikamilifu kuhakikisha kwamba wanafanikisha haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja la msingi sana ambalo ningeomba kuzungumza hapa kwa msisitizo, ni suala la elimu. Katika mchakato huu, ni lazima tuhakikishe kwamba kuna uwiano wa elimu katika nchi zetu hizi za Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo huu kumekuwa na matatizo ambayo yamezoeleka, kwamba watu tunadhania kwamba kujua Kingereza ndiyo kila kitu. Lengo la mkakati

huu wa elimu, ni lazima uelekee katika kuhakikisha kwamba Kiswahili kinapewa umuhimu wa kipekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la lugha limetu-*cost* sana na linaendelea kutu-*cost*. Ni suala ambalo ningeendelea kulisisitiza kwamba lazima wawakilishi wetu kwa maana ya Serikali na wawakilishi, walitilie mkazo na walisimamie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulizungumza ni umuhimu wa kuwa na sera ya pamoja ya kuweza kuhakikisha tunapunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje. Hatuwezi kuwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo inaweza ikahamasisha uzalishaji. Unapokuwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki, miaka inayokuja tutaondoka katika kutegemea kilimo ambacho kinaajiri watu wengi sana.

Kwa hiyo, tutaelekea katika viwanda na hivyo tutakuta tunapoteza ajira nyingi sana kwa watu wa kawaida. Ajira nyingi zitakazotengenezwa zitakuwa ni za watu ambao wana uwezo wa kielimu. Kwa hiyo, moja ya mambo ambayo yataweza kusaidia ni kuhakikisha kwamba tunawezesha watu wetu kielimu lakini pia tunakuwa tunayo sera ambayo inasaidia kuzuia ili kuhamasisha ujenzi wa viwanda vyetu na bidhaa hizi ziweze kukuzwa na hatimaye kuweza kuuzwa nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema nitazungumza mambo ambayo yako ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini kuna mambo ambayo kama Tanzania tunaweza tukayafanya. Huwezi ukazungumzia mafanikio ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Tanzania bila kuizungumzia Zanzibar. Kuna upungufu mkubwa sana katika ushiriki wa Zanzibar ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunaambiwa hapa kwamba kuna miradi mingi iko katika *pipeline* na michakato inaendelea, nitoe mfano mmoja wa mradi wa Bandari ya Maruhubi, leo ukizungumza na viongozi wetu wa Afrika Mashariki watakuambia kwamba kuna matatizo kutoka

Zanzibar na ukienda Zanzibar wanakuambia vingine, kuna upungufu wa uratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze jitihada za kuanzisha ofisi, lakini ofisi iliyoanzishwa Zanzibar haina meno. Huwezi ukafungua ki-*desk* kimoja ukaweka watu wawili, watatu halafu ukasema una sehemu ya kuratibu. Upungufu mkubwa wa ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika MAshariki ni kukosekana kwa uratibu wa Wizara hii Zanzibar. Naomba kutoa wito kwa Wizara hii na Serikali, waanzishe Idara au Ofisi ya Afrika Mashariki Zanzibar ambayo itakuwa na *Commissioner* au Mkurugenzi atakayekuwa anaratibu na kuondoa migongano ambayo inajitokeza. Ukifungua kitabu hakuna hata mradi mmoja ambao umetekelezwa Zanzibar, ni miradi tu iliyoko katika michakato, sijui wako mbioni. Hili jambo linasikitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni miradi mikubwa ya nchi zetu, nitoe mfano wa suala la miundombinu ya umeme. Nilikuwa kwenye Kamati ya Afrika Mashariki ambayo ilikuwa inasimamia utekelezaji wa *East African Power Master Plan* katika miaka ya mwanzoni mwa 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana leo kusoma hotuba hii nikaona bado mradi wa kuunganisha gridi ya Taifa kutoka Arusha kwenda Nairobi, tunaambiwa ndiyo kwamba uko katika upembuzi yakinifu. Kamati yetu ya Usimamizi ya wataalam iliyokaa kwa miaka kadhaa ilishafanya upembuzi wa kutosha na tulifika hatua ya *negotiation*, leo tunarudi tena nyuma!

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni lazima wawakilishi wetu wawe *aggressive*. Kenya wamezorotesha mradi huu kwa makusudi, kwa sababu wao wameona wamepata fursa ya kuunganisha gridi yao sasa na Ethiopia. Suala la matatizo ya umeme, moja katika masuluhisho yake, ni kuhakikisha kwamba tunategemea pia kuunganisha gridi zetu na nchi nyingine. Tutakapounganisha Gridi ya Taifa Tanzania na Zambia na tukai-*connect* na *Southern African*

Powerpool na huku Nairobi itutapata fursa ya kuangalia uwezekano wa kuzalisha kwa kutumia vyanzo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunatoka kwenye kutegemea maji na tunaingia katika kutegemea gesi, *accident* iliyotokea kule Ulaya-Urusi kuhusu bomba linalokwenda Uingereza, *crisis* ambayo inatoka sasa hivi Mtwara, hatuwezi kufika mahali tukasema tumeona madhara ya kutegemea maji, sasa tunakwenda kujikita asilimia kubwa kutegemea *gas*, ni lazima kuwe na vyanzo mbadala na tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuunganisha gridi ya Taifa kutatoa fursa ya kuweza kuuza umeme nje ya nchi na hivyo nchi ya Tanzania kuweza kutumia *potential* kubwa iliyonayo katika maeneo mengi ikiwemo makaa ya mawe, maji katika maneno mbalimbali ya nchi na kadhalika. Kwa hiyo, nilitaka nimwombe Waziri maelezo, ni kwa nini tunarudi nyuma katika mradi huo wa kuunganisha gridi ya Taifa ya Tanzania na nchi nyingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kulizungumza ni suala la wawekezaji binafsi. Kuna haja ya kuhakikisha kwamba tuna-*provide incentive* kwa wawekezaji wetu wa ndani, ili waweze kushiriki kikamilifu. Katika takwimu hizi za kitabu, tunaambiwa kwamba asilimia kubwa ya wauzaji wa bidhaa katika Afrika Mashariki waliotawala ni Wakenya. Ni kwa sasababu Wakenya...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Kwa taarifa niliyopewa na Kaimu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis hatachangia na nafasi yake itachukuliwa na Mheshimiwa Leticia Nyerere na Mheshimiwa Sabreena Sungura na watachangia kwa dakika tano tano. Kwa kuwa

hawa wanagawana dakika, Mheshimiwa Mnyaa ukimaliza Mheshimiwa Leticia Nyarere na Sabreena Sungura watafuata.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nichangie Wizara hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kuchangia ukurasa wa 12 wa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri ambapo inazungumzia Umoja wa Forodha na kuna nukuu pale imetolewa kuhusu matokeo ya Umoja wa Forodha kwamba umeleta matokeo chanya. Nikiri faida zipo lakini nipende tu kwa tahadhari Mheshimiwa Waziri ajue kwamba na matokeo hasi yapo. Hili linaonekana mara nyingi sana katika bidhaa za Tanzania zinapotolewa hapa kuingizwa Kenya.

Mfano, leo ukitoka na hiliki, kama *seeds,* utaingia nazo kwa urahisi Kenya lakini ukitoka na mafuta ya hiliki, hautapita na utarudishwa nayo. Ukienda na mafuta ya alizeti katika *gallon* ya *five litres* ambayo inatengenezwa hapa Tanzania, ukifika kule wanakuambia hatutaki *five litres*, hapa mfumo wetu ni *three litres*, wanakurejesha. Ukienda na maharage unaingia kirahisi, ukienda na mahindi utapitisha kirahisi pia, lakini ukienda na unga wa mahindi hawataki. Wizara ifahamu mambo hayo mengine yapo na ni kero kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, katika ukurasa wa 12 pia, Umoja huu wa Forodha umesifiwa kwamba umeendelea kuchangia kuvutia wawekezaji. Kuna jedwali, ukurasa wa 86 kiambatanisho cha tano, kwamba mwaka 2008 miradi 77 na nchi iliyohusika kuingiza miradi hapa nchini ikatajwa, mwaka 2009 miradi 42, mwaka 2010 miradi 33, jumla mpaka mwaka 2012 kuna miradi 195. Kitu kimoja cha kuangalia hapa kwa mtu aliyeangalia jedwali hili, nchi za Kenya na Uganda ndiyo wawekezaji wakubwa hapa, lakini Mheshimiwa Waziri hakutuonyesha na sisi Watanzania katika Umoja huu wa Forodha ni kwa kiasi gani tulivyowekeza Kenya? Hakuna jedwali lolote linaloonyesha mpangilio huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna manufaa kwa Wakenya ndani ya Tanzania na manufaa ya Tanzania ndani ya Kenya hapa hatuyaoni. Katika ile *speed and standard* ya Mheshimiwa Waziri ilikuwa pia atuonyeshe Watanzania wamewekeza kiasi gani Kenya. Kwa sababu, kuwekeza kule kuna faida yake, kuna faida ya kiteknolojia, ajira na mambo mengi sana. *Speed and standard* usituonyeshe wao wamekuja Tanzania kiasi gani na miradi mingapi bali utuonyeshe na sisi Watanzania kule wamekwenda kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo, mbona miradi ya wawekezaji yote imewekezwa upande mmoja tu wa Jamhuri ya Muungano? Jumuiya ya Afrika Mashariki tumeingia Tanzania katika Muungano wa nchi mbili za Zanzibar na Tanganyika, ukitaka ita Tanzania Bara lakini sasa awekezaji wote hawa mbona wamewekeza upande mmoja tu: Je, wameelekezwa au kuna tatizo gani kule Zanzibar? Hakuna mambo ya kuwekeza? Kama yapo, naomba Mheshimiwa Waziri akija hapa kujumuisha aniambie, katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Zanzibar kumewekezwa kitu gani? Vinginevyo ndiyo ile hofu ambayo ipo siku zote ya upendeleo katika Jamhuri tutaona ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hujatutajia miradi ambayo imewekezwa, haya ndiyo malalamiko ya Wazanzibar kuhusu matatizo ya Muungano ambayo mnayafanya mpaka na mtu kama Waziri ambaye ni Mwanasheria, inabidi atueleze ni miradi mingapi katika miradi 195 imewekezwa Zanzibar na kitu gani kilichowekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maendeleo na mambo yanayochochea uchumi. Katika ukurasa wa 32 na 33, vipaumbele vya Tanzania vimeelezwa katika miradi ya bandari, mitandao ya reli, viwanja vya ndege, anga, barabara kwamba hivi ni vipaumbele vya Tanzania. Nakiri mafanikio yapo, hapa barabara ya Namanga - Arusha tayari, Mheshimiwa Rais na wakubwa wa Afrika Mashariki wanafungua. Tayari kuna Bagamoyo, Tanga na Horohoro. Reli ya Kati *feasibility study* imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona, haya ni mambo ya kiuchumi, lakini tunakuja tena palepale kwamba, uchumi huu upande mmoja? Mbona hatuoni bandari ya Mkumbuu Pemba, ambayo imetajwa mipango toka ilipoanzishwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, miaka 14 sasa,tangu mwaka 1999, hatusikii kuhusu bandari ya Mkumbuu. Imo kwenye makabrasha, hatuoni utendaji wala *feasibility study* haijawahi kukamilika. *Airport* Pemba, imetajwa mara ngapi? Maruhubi imetajwa mara ngapi? Huku tunaona upande mmoja mafanikio na ufunguzi lakini upande mwingine hakuna chochote, tueleweje au ndiyo katika mtindo uleule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hayo tu katika mafanikio, kuna *One Stop Boarder Post* ya Lunga Lunga/ Horohoro, kuna Taveta/Holili, kuna Namanga/Namanga, Sirari/Isebenia, Mutukula/ Mutukula, Rusumo/Rusumo na mbili tayari zimekamilika, ya Taveta-Holili na Sirari/Isebenia. Hayo ni maendeleo, tungetamani na sisi. *(Makofi)*

Sasa kwa upande wa Zanzibar jiulize kuna nini? Miaka 14 bandari ya Maruhubi, bandari ya Mkumbuu, *Airport* hakuna chochote kinachoendelea. Hili linatutia unyonge na haya ni mambo ya kufanyiwa marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hayo tu niliyoyataja, kuna gati namba 13 na 14, yote ni fedha ya Afrika Mashariki. Kwa nini tufanye miradi upande mmoja wa Jamhuri? Ndiyo maana Zanzibar tunataka kuingia Afrika Mashariki kama nchi kwa maonevu ya namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengi kusema kweli, mwenzangu alizungumzia ofisi, ofisi ya mambo ya Afrika Mashariki kule Zanzibar iko wapi? Hebu atuambie iko wapi? *Coordination* itakuwa wapi? Tabu iliyopo, ofisi hiyo iko Ikulu, wananchi watapata *access* vipi? Haya ni mambo ambayo yanaonesha kwamba kuna matatizo.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa ndege wa Pemba, nimeshautaja, ni matatizo mpaka leo. *Anyway*, tuje kwa upande mwingine, kuna hili Shirikisho la Kisiasa, lakini tuelewe katika hili shirikisho la kisiasa, siyo mambo pamoja na hiyo Kamati iliyoundwa kuratibu maagizo ya Wakuu wa Afrika Mashariki, haya ni mambo ya kuwa *careful* sana.

Formation ya Jumuiya hii katika Shirikisho la Kisiasa, kuna tofauti. Wakati Katiba ya Uganda inatambua Ufalme wa Baganda na Kabaka sijui, sisi huku tofauti. Kwa hiyo, hili shirikisho la siasa, muundo huu ni kitu ambacho tuwe na tahadhari, vivyo hivyo hata mambo ya fedha, hii Sarafu moja, mambo yanayoongelewa muda mrefu, lakini hii *difference* iliyopo na kila mwaka tunaikumbusha, tofauti iliyopo baina ya fedha ya Kenya, ya Tanzania na ya Uganda, na hizo nyingine za Burundi, wameshindwa *Scandinavia* ambao *Krona* ya *Norway*, ya *Sweden*, ya *Denmark*, tofauti yake ni ndogo sana, lakini miaka yote hiyo *Scandinavia* wameshindwa kuwa na Sarafu moja.

Sisi tunaotaka kuharakisha mambo haya, kabla ya kutengeneza haya mambo mengine, na tofauti ni kubwa, leo uwe na Sh. 20/= za Kitanzania, ndiyo Sh. 1/= ya Kenya, sijui na Uganda namna gani huko, halafu tunazungumza, haya mambo siyo ya kuvamia, siyo ya kufanya haraka, ni mambo ya kuangalia na yaeleweke kwa wananchi kwa upeo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba kuna vikao vya Mabaraza ya Mawaziri ambavyo vinafanyika kwa njia ya *rotation*. Pale Arusha sasa Ofisi imeshapatikana. Kwa nini visifanyike pale Arusha ili hata kipato Tanzania kingie? Kwa nini mpaka leo iendelee mtindo wa ku-*rotate* na jengo lipo sasa? *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyaa ni Kengele ya pili.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Sabreena atafuatiwa na Mheshimiwa Leticia.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mhesshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika Bajeti hii ya Wizara ya Afrika Mashariki. Kwanza kabisa, napenda kuchangia kuhusiana na mahusiano ya Bunge la Afrika Mashariki na Bunge letu la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 48 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, unaelezea ni jinsi gani Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanavyopatikana. Kwa kifupi, ninaweza nikasema tu kwamba Bunge hili ndiyo Jimbo la Wabunge wa Afrika Mashariki. Lakini Ibara ya 49(2) (a) ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, inaeleza ni jinsi gani Wabunge hawa wanatakiwa washirikiane na Bunge la Jamuhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusikitika kwamba mpaka sasa hivi tuliambiwa itaundwa Kamati ya Afrika Mashariki, lakini Kamati hiyo haijaundwa. Hawa ni Wawakilishi wa wananchi, sisi ni Wawakilishi wa wananchi ambao tumewachagua wao. Wananchi lazima wapate mrejesho nini kinaendelea katika Jumuiya yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka dakika hii, nchi ya mwisho katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa *less informed* ni Tanzania. Wabunge hawajui nini kinaendelea, wananchi hawajui nini kinaendelea, halafu tunasema tunakwenda kwenye *Monetary Union*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii, hatuwatendei haki Watanzania. Basi angalau tuambiwe ni Kamati gani ya Bunge, Wabunge hawa wa Afrika Mashariki watakuja kutoa ripoti zao kama Kamati ya Afrika Mashariki inashindwa kuundwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili napenda nizungumzie kuhusu utelezaji wa makubaliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tumeona kwamba hapa tulikuwa tuna umoja wa forodha, na suala hili linaendana moja kwa moja na masuala ya biashara, lakini ni kwa kiasi gani, sheria na kanuni zetu zina-*reflect* itifaki hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa sasa kuna haja ya kuhakikisha kwamba tunafanya *harmonization* katika sheria zetu ili tuweze kutekeleza. Wenzetu nchi za Ulaya wamekuwa wanatumia *directives;* japo na sisi tunatumia, lakini ni kwa kiwango kidogo sana. Kama tungeweza kutumia *directive*s, tunge-*issue directive*s, tungetengeneza *regulation*s, tungeweza kuhakikisha kwamba baadhi ya mambo madogo madogo kama haya yanafanyika.

La pili, ningependa tu kujua katika Jumuiya hii kuhusu *time frame.* Kwa sababu kama tungepeana *time frame*, kwamba itifaki hii mpaka kipindi hiki iwe imetengenezewa utaratibu, iwe imekuwa *harmonized* katika nchi zetu za Jumuiya, nchi wanachama ingeweza kusaidia sana kuyaondoa matatizo haya.

Kuna suala sasa hivi la kuhusu *tax incentive*s. Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinashindana, nani apate mwekezaji. Ripoti ya *IMF* inaonesha kwamba nchi za Jumuiya Mashariki zitaendelea kupoteza kodi kutokana na kutokuwa na sera ya pamoja kuhusiana na *tax incentives. (Makofi)*

Sasa sijui katika Jumuiya wenzetu wanajipangaje lakini hali itaendelea kuwa mbaya, itafikia hatua tutapata *zero balance* sasa, kwamba kila mtu anashusha, anashusha ili mwekezaji aje nchini kwake. Sasa sijui wenzetu wa Jumuiya wanajipangaje na Waziri na *team* yake wanajipangaje kuhusiana na suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, saula lingine ningependa kuongelea leo, ni kuhusu fursa. Katika madodoso tuliyopata kutoka katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, tumeona kabisa kwamba kuna fursa ambazo zinapatikana, na ni lazima

Watanzania wapate fursa hizi kwa sababu ni haki yao ya msingi. Kuna fursa ya uwekezaji, ya biashara, ya ajira, lakini tunataka kujua *Tanzania Investment Center*, ina-*play part* vipi kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata fursa za kuwekeza katika nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Isiwe tena kazi ya kuleta Wachina na watu wengine kuja kuwekeza nyumbani, lakini watu wa Tanzania, waende wakawekeze huko. Ni vipi kituo hiki kinawasaidia Watanzania kujua fursa zinazopatikana katika nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki, na watupe tu ripoti labda ni Watanzania wangapi mpaka dakika hii wamewekeza katika nchi hizo?

Suala lingine ni kuhusu *Tanzania Chamber of Commerce*, biashara. Ni jinsi gani inawasaidia wafanyabiashara wa Tanzania kuhusiana na fursa ambazo zinapatikana katika Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni ajira,...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKIKI: Mheshimiwa Sabreena muda wako umepita. Naomba nimwite Mheshimiwa Leticia.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kabla sijaendelea na mazungumzo naomba ku-*declare interest* kwamba mimi niko katika Kamati ya Mambo ya Nje.

Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kwa kazi yao nzuri ambayo wamekuwa wakifanya, na kwa taarifa ambazo wamekuwa wakizitoa katika Kamati kila wanapokuja kwenye Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile Waheshimiwa Wabunge wa Bunge letu wanaotuwakilisha, wanafanya kazi

katika mazingira magumu, na tungeomba wasaidiwe kupata Kitengo cha Utafiti ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi kupeleka taarifa ambazo zitakuwa zimefanyiwa utafiti wa kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nizungumzie suala la ajira, soko la ajira Afrika Mashariki. Ili tunufaike kama Taifa, ni lazima tuelewe kwamba elimu ya juu peke yake siyo kigezo cha kupata kazi katika soko la Afrika Mashariki. Ni lazima ujiulize; kuna maswali ya kujiuliza. Ukisema ndiyo katika maswali haya, basi unaweza ukaendelea kwenda kwenye *interview.* Ni lazima ujue *are you reliable?* Unaweza ukategemewa na mtu atakayekuajiri? *Are you dependable*? Ni mtu ambaye unaweza ukakaa ofisini muda wote bila kuomba ruhusa kila siku? *Are you responsible?* Ni mtu ambaye uko *responsible? Are accountable*? Ni mtu ambaye unawajibika? Ukishasema 'ndiyo' katika maswali haya, basi unaweza ukaendelea kwenda kufanya *interview*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *interview*, ni lazima uelewe, jipime. Siyo unakwenda pale umevaa koti upande mmoja mrefu, upande mwingine mfupi. Halafu mwingine unamkuta hata ile kola ya koti, utafikiri furushi la mchanga. Ni lazima ujiangalie wakati unakwemda kwenye *interview*, siyo elimu tu inayoangaliwa. Kuna usemi unaosema kwamba, *people don't care about how much you know, until you know how much you care. (Makofi)*

Kwa hiyo, watu hawatajali una elimu kiasi gani kama wewe mwenyewe hujali jamii, au hauko *presentable* katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima pia tujiangalie sana, unapokwenda kwenye *interview*, usipuuze baadhi ya mambo. Kuna mtu anakwenda, ndevu ziko hapa karibu kifuani. (*Kicheko*)

Cha kushangaza hizi ndevu zina rangi karibu nne tofauti. Kuna rangi nyeusi, nyeupe, *brown*, nyekundu kwenye ndevu hizo. Kweli, nani anataka kuwa na mtu wa aina hiyo ofisini kwake? Hakuna! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo kama haya ingawa ni aibu kuyazungumzia, ingawa ni aibu kuwaelewesha Watanzania wayafuatilie, ndiyo maana yamekuwa yakijirudia rudia. Tunaona aibu! Hatuwafundishi watu wetu kwamba unajua *hygiene* ni jambo zuri sana, ni jambo ambalo linatakiwa ili upate ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *hygiene,* nachelea kusema kwa mfano, *deodorants* zitumike! Watu hawana mazoea ya kutumia *deodorant.* Hawafundishwi kutumia *deodorant* kwa kuogopa kwamba, nitakuwa *offensive*. Lakini humsaidii Mtanzania! Matokeo yake anaachwa tu kwa sababu alikuwa hajatumia *deodorant*. Kwa hiyo, tuwe na elimu ya kuwaelimisha Watanzania wajiandae katika hizi ajira za kimataifa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira ya kimataifa siyo mzaha! *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Leticia.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Maneno yako mazito! Naomba nimwite Mheshimiwa Waride Jabu. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. WARIDE BAKARI JABU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kunipa fursa hii, lakini kwanza kabla sijaendelea, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kuipongeza Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kuanzisha ofisi yake pale Zanzibar. Najua kuna matatizo mengi ambayo bado hawajaiweka sawa ofisi hii, lakini kwa vile ni kilio cha muda mrefu cha Wazanzibari, tumefarijika kwa kufunguliwa ofisi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nilikuwa

nashangaa sana kwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Ndugu yetu huyu ametoka Zanzibar, na kwa kweli kwa hili, naweza kusema kuwa, yeye katika Bajeti yake alikuwa kwanza anatakiwa ayaseme yale ya Zanzibari ya kuhusiana na huu mtangamano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi hii imefunguliwa na kwa kweli haikupangiwa hata Bajeti, nimefungua randama sikuona hata *a single cent* iliyopangiwa Ofisi hii. Mambo hayo nilitarajia yangesemwa katika Bajeti aliyoisoma kama Msemaji wa Kambi ya Upinzani, lakini alichokifanya ni kumsema Mheshimiwa Kinana na CCM. Lakini haitoshi, huu mtindo wa kuanza kutukana baba zenu humu ndani, sasa hivi mnaanza kutukana baba wa wenzenu, ndiyo matokeo yake haya. *(Makofi)*

Mnaanza kumsema Mseven katika Bajeti ya Afrika Mashariki, amewakosea nini baba wa watu? Mimi nawaambia, tujihusishe na mambo yanayotuhusu kwenye Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nilikuwa naomba nichangie lingine kuhusiana na mtengamano huu. Tumeona Wizara hii ilikuwa inatoa mafunzo kwa ajili ya Watanzania ambao wanaoishi mipakani. Nilikuwa nataka kujua, Zanzibar imepangiwa vipi bajeti yake na itafundishaje? Hawa wananchi wanaofundishwa kwa kule kwetu Zanzibar, watawatoa vipi? Kama ilivyo Bara au itakuwa ya aina gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa nataka kuchangia; nimesikia katika vyombo vya habari vikieleza kuwa Tanzania imekataa kutia saini makubaliano, au mkataba wa ulinzi wa pamoja.

Nilikuwa najiuliza, kwa nini Tanzania imekataa hili? Kwa sababu kutokana na hali halisi iliyoko sasa hivi katika Maziwa Makuu au katika Bahari zetu za *Indian Ocean*, kuna haja kubwa ya kukubali kama Tanzania kuweka saini mkataba huu wa ulinzi wa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia kuwa Kenya na Rwanda wameondoleana vibali vya *work permit*. Sasa nilikuwa najiuliza, wao tayari wenzetu wameshalifanya hili, sisi Watanzania tutajitia tu kichwa kichwa au vipi? Kwa sababu huu ndiyo mwanzo, kwa sababu kama Kenya na Rwanda wamekubali, sisi Tanzania tukoje katika hatua hii?

Mimi nilikuwa naishauri Wizara hii, tulifikirie hili, tusije tukaingia kichwa kichwa, kama wenzetu walivyofanya kwa sababu pengine huu ni mtego. Wao wameanza na sisi bila kufanya utafiti yakinifu, tukajiingiza katika hili. Nilikuwa namshauri sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hili kabla hatujakwenda kukubaliana kwenye hili la *work permit* katika nchi zetu za Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kuipongeza Wizara ya Afrika Mashariki kwa kufungua Ofisi yake pale Arusha. Matarajio yetu Watanzania, Ofisi imefunguliwa, sasa hivi ile ni Ofisi kwa ajili ya Mikutano yote na shughuli zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tunaomba Wizara, kuliko ilivyokuwa huu mtindo wa zamani wa kuwa mara Mkutano ukafanyike Rwanda, mara Burundi, sisi tunaukataa. Kwa kuwa Ofisi ile ya Afrika Mashariki imefunguliwa, shughuli zote zifanyike pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa hayo machache kwa sababu ya muda, nilikuwa naunga mkono hoja tena kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tutakaporudi mchana tutamsikiliza Mheshimiwa Dalali Peter Kafumu, ndiye atakuwa mchangiaji wetu wa kwanza. Lakini hata hivyo, hapa nina tangazo kutoka Ofisi ya Mheshimiwa Spika. Ameniomba niwatangazie Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Uongozi kuwa, kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo leo Ijumaa, tarehe 24 Mei, saa 7.00 mchana, katika Ukumbi wa Spika. Kwa hiyo, ninawaomba sana.

Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge mahali popote mlipo, kuna kikao cha uongozi, na kama Mwenyekiti

wa Kamati hayupo, ningeomba sana Makamu Wenyeviti wa Kamati hizo ambazo Wenyeviti wao hawapo, washiriki kikao hicho sasa hivi.

Sasa na kwa kuwa muda tuliobaki nao ni dakika chache tu haziwezi kumtosha mchangiaji wetu huyu niliyemwita, basi naomba nisitishe shughuli hizi za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, habari za mchana!

WABUNGE FULANI: Nzuri.

MWENYEKITI: Baada ya kuwaomba mketi katika viti vyenu, basi tutaendelea na ratiba yetu ya jioni ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema wakati nasitisha shughuli za Bunge mchana wa leo, nilisema nitamwita msemaji wa kwanza Mheshimiwa Dkt. Dalali Peter Kafumu, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Mikidadi, ndiye atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

MHE. DKT. DALALI P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa kwanza kwa mchana huu. Naomba kwanza niseme kwamba ninaunga hoja hii mkono kwa sababu nikifika mwishoni naweza nikakosa muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, hoja tumeisikia na tumeielewa.

Kama kawaida, wote tunafahamu kwamba ushirikiano wa nchi nyingi katika umoja, uwe Umoja wa Afrika,

Umoja wa Ulaya, *Community* yetu hii ya Afrika Mashariki na kila aina ya umoja una malengo ni makubwa mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kuleta nguvu ya kiuchumi katika nchi hizo. Lakini pia lengo la pili ni kuhakikisha kwamba inawezekana kukawa na umoja wa kiutawala. Kwa hiyo, Afrika Mashariki sisi tunaonesha kwamba tunaweza kujiunga kama Afrika. Ni alama, ni *seed* ya kwenda kwenye Umoja wa Afrika. Kwa hiyo, ni lazima tuuenzi, tuupiganie huu umoja na tuweze kuingia huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwenda kwenye umoja huo wa nchi za Afrika ya Mashariki, kuna changamoto nyingi sana kwa sababu ya tofauti ya nchi zetu kiuchumi. Wachangiaji wa asubuhi wamesema na mimi nitarudia baadhi ya mambo kwa ufupi, kwamba changamoto hizo zinaweza kuifanya nchi nyingine ikaachwa nyuma kiuchumi badala ya kwenda mbele kiuchumi kama nyingine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni lazima tuwe wangalifu sana katika kuingia katika Umoja huu wa Afrika ya Mashariki. Sisi Tanzania ukiangalia, tafiti zinaonesha kwamba kwa namna fulani tuko nyuma ya nchi ya Kenya na hata nchi ya Uganda. Kwa hiyo, tunatakiwa kwenda kwa ungalifu na kwa kutazama vizuri miguu yetu inakanyaga wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie mambo mawili makubwa ikiwezekana na la tatu. Ushindani wa ajira kama walivyosema wachangiaji wengine, ni jambo kubwa sana katika Umoja huu, au katika *Community* hii ya Afrika ya Mashariki.

Watanzania kama Wakenya na Waganda tumesoma vizuri. Humu ndani ukihesabu *Ph.D* ziko nyingi kweli kweli, *Masters* ni nyingi kabisa kabisa! Lakini Watanzania tunalo tatizo moja kwamba tunaposhindanishwa na watu wa Kenya tunakosa uzoefu. Sijui ni kwa sababu gani. Lakini pia tunakosa *confidence,* kwa maana ya kujiamini. Dada yangu Mheshimiwa Leticia Nyerere alisema, hatujiamini kabisa tukiitwa kwenye *interview,* huwa tunababaika. Kwa hiyo,

tunahitaji sisi kama Taifa, ili tuweze kwenda vizuri huko kwenye Afrika ya Mashariki, ni lazima tuwatayarishe watu wetu; wawe na *confidence* pamoja na kusoma, lakini pia wajue lugha. Sisi tuna tatizo la lugha ya Kiingereza, ambayo ni lugha muhimu sana katika medani za Kimataifa. *(Makofi)*

Watanzania wengi tunapata taabu sana, tunapokwenda kwenye medani za kiutawala, za kibiashara katika Mataifa, Kiingereza hatukijui. Ni vizuri Wizara na Serikali tukafanya mkakati maalum kuhakikisha Watanzania tunawawezesha kwenye mambo haya. Kwenye vyuo vyetu na kwenye mambo mengi ni lazima tuwawezeshe watu wapate uzoefu.

Mimi ninakumbuka nilipopata *Ph.D* yangu mwaka 2000, niliomba kazi Afrika Mashariki, na bahati nzuri niliitiwa kwenye usaili. Lakini nilikutana na vijana wasomi wazuri wa Kenya wenye *Ph.D* zao lakini na uzoefu wa Kimataifa, na Kiingereza kilikuwa kinaongelewa utafikiri wamezaliwa London. Mimi naongea Kiingereza cha Kisukuma. Ilikuwa taabu kweli kweli. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba kwa kweli Serikali tujitayarishe kwenye jambo hilo. Tusipofanya hivyo, tutapta shida. Ukienda kwenye hoteli za Kimataifa leo hii, wahudumu wale *Receptionists* wengi wazuri ni watu wa Kenya. Sisi wa kwetu wanahangaika na Kiingereza. Ma-*Air Hostess* wako wamekwenda mpaka *Qatar Air Ways* na *Emirates Airways,* Wakenya wapo, sisi ni taabu. Kwa hiyo, inabidi tujitayrishe kwenye suala hilo la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuchangia ni suala la ardhi. Katika suala hili la ardhi kuna tofauti kubwa sana kati ya Kenya na Tanzania. Sisi sheria zetu hapa, bado ardhi inamilikiwa na Serikali, na Taifa na wananchi kwa ujumla. Kwa hiyo, ni *Custodian* ya Mheshimiwa Rais wetu ndiye anayemiliki ardhi. Mtu unapewa ardhi kwa miaka 33, 66 au 99 ufanyie kazi na Rais anaweza akakunyang'anya wakati wowote.

Kwa hiyo, jambo hili tukiingia kwenye Umoja huo wa Afrika ya Mashariki, labda tukakubali kuwa kama Kenya ambapo ardhi ni ya binafsi, ni *private land,* tutapata taabu kweli kweli. Ardhi inaweza ikachukuliwa na wenzetu kwa sababu wao wana uzoefu wa kumiliki ardhi, wana uzoefu kuwekeza katika ardhi, ardhi inaweza ikapotea na wananchi wetu wakakosa ardhi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni lazima tujitayarishe, tuchukue muda mrefu kidogo kuamua jambo hili, kwa sababu tuna watu kwenye Jimbo langu, kuna wazee na mimi mwenyewe, sisi ni wafugaji. Hata Wamasai na ndugu zangu wafugaji, tukiwapa wenzetu ardhi tutachungia wapi? Tunahangaika sasa, ikija na Afrika Mashariki ndiyo itakuwa taabu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Serikali itutayarishe, tusiharakishe. Katika mazungumza na majadiliano, lazima tujitayarishe tuwe kama wenzetu. Vinginevyo, tutapata taabu na tunaweza tukakosa baraka na kuwahudumia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho, napenda nizungumzie kidogo kuhusu suala la biashara. Biashara katika Umoja iko hivyo hivyo. Wale wanaojua biashara, wanaweza kuwashinda wenzao.

Nashukuru sasa hivi tunatengeneza Sera ya Mtangamano wa Afrika Mashariki, naomba basi Serikali katika mazungumzo na majadiliano, mtumie tafiti zilizopo zinazoonesha *gap* kati ya Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na tupeane nafasi. Inapobidi, kuwe na *quarter system* hata ya ku-*export.* Tuwape wananchi wetu kwa mfano wakulima wetu wa pamba kule Shinyanga na Igunga, wakulima wa tumbaku kule Tabora, wakulima wa alizeti na wengine, wapewe fursa ya kupeleka mazao yao Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiacha ushindani huu wa uwazi kwa sababu hatulingani kiuwezo, tutapata taabu. Wananchi wetu watashindwa kushiriki, na tutakuwa sisi ni

soko. Pamoja kwamba tumetaka liwe soko la pamoja, lakini sisi tunaweza kuwa ni soko zaidi na tukakosa huduma kwa watu wetu. Kwa hiyo, nawaomba sana, Serikali na Wizara, jambo hili mliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la biashara, suala la kodi ni jambo muhimu sana. Nimeona hotuba ya upinzani wamezungumzia kodi. Katika ukurasa wa 12 hapa, wanazungumzia kwamba nchi hizi zinashindana katika kusamehe kodi na hawataki, wanaponda jambo hilo.

Mimi naomba niwaambie kwamba misamaha ya kodi pamoja na *fees* mbalimbali ni kichocheo kikubwa sana cha kukuza uchumi katika nchi nyingi. Kodi zinasamehewa, kodi zinapunguzwa ili kuwezesha uwekezaji wa ndani na nje uweze kukua. Ni lazima uchague kodi fulani fulani uziondoe ili uhamasishe watu wako waweze kufanya biashara. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kafumu, hiyo ni kengele ya pili.

MHE. DKT. DALALI P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nakushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Dkt. Kafumu. Sasa namwita Mheshimiwa Fatuma Mikidadi.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia suala zima la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu hiki cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kina mambo kama kumi. Lakini mimi nitaje matano tu kama muda utaruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, limetajwa suala la usafirishaji. Nikianzia na Bandari; mimi nimefurahi sana

katika kitabu hiki ukurasa wa 35 kuelezea masuala ya gati namba moja mpaka saba katika Bandari ya Dar es Salaalam; Ujenzi wa gati mpya namba 13 mpaka 14, ninanukuu, katika bandari hiyo. Hapo ndiyo mwisho wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kukarabati bandari hizi, kwa sababu inasemekana kwamba baadhi ya nchi nyingine mizigo yao hushushwa bandari za jirani, kwa mfano Mombasa na kadhalika, kwa kukimbia matatizo ya bandari zetu.

Kama Serikali imeona hili, kwa kweli mimi nafurahi, nawapa pongezi kwa kuendeleza bandari yetu ya Dar es Salaam. Lakini hilo iwe kweli, isiwe katika makaratasi, kwa sababu tumesikia siku nyingi wanazungumzia masuala ya Bandari ya Dar es Salaam; gati namba fulani, gati nambari fulani; mpaka lini? Tunaomba iwe kweli kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu. Katika hizi bandari, tunazo bandari nyingine nyingi tu Tanzania. Labda tungeliweka uwiano katika Tanzania, bandari zipi nyingine ziongezeke, ukiachia zote kwenda kwa upande mmoja? Kwenda Dar es Salaam, kwenda Zanzibar, kwenda Ziwa Victoria, huko huko zinaishia huko huko. Tuangalie na bandari nyingine ambazo zina sifa kubwa zaidi ambazo zipo *naturaly,* zipo asilia zipo pale, hazitaki kuchimbwa, wala kufanywa nini, zipo tayari bandari asilia ambazo zingeweza kutumika. Kwa nini nimesema hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo kwa sababu tunazo bandari nyingine tukitawanyisha Kusini; tunayo Bandari ya Mtwara. Bandari ya Mtwara ina sifa kubwa sana.

Ningeomba sana katika suala hili la Afrika ya Mashariki nayo muiangalie. Ile Bandari nikikwambia sifa zake kwa kweli utashangaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari ile ya Mtwara ina kina kirefu, bandari ile ni ya asili, bandari ile ni ni *shortcut* ya

kutoka Malawi, Afrika ya Kusini kuja pale. Kwa mfano, kutoka Malawi hadi Mtwara ni kilomita 948, hii ni njia ya mkato. Lakini ukitoka Malawi kwenda Dar es Salaam ni kilomita 1,640 Bandari ile ya Mtwara ina sifa zote za kubeba meli zote kubwa za Kimataifa. Inaweza ikafunga gati, meli mbili kubwa za Kimataifa na meli ndogo, zinafunga pale bila matatizo, ile Bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, bandari ile ya Mtwara zinaweza kuweka meli sita zikakaa pembeni. Wenyewe wanasema zinakaa ghuba. Siyo ghuba ya Uajemi, hapana; ghuba ya Tanzania. Zinakaa kwenye ghuba. Zinakaa pembeni kusubiri wenzake. Meli sita kubwa za Kimataifa zinakaa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuangalie upya bandari zetu, tuzitawanye katika Taifa la Tanzania, kwa maana hii ya Afrika Mashariki Tanzania ipo, basi tupeleke angalau na Kusini. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la wahamiaji haramu, au njia za mpenyo mpenyo ndogo ndogo ambazo watu wanakuja kuleta bidhaa zao kwa wizi na hasa uhamiaji haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunakabiliana na watu wengi ambao wanakuja aidha kukaa au kupitiliza kwenda Afrika ya Kusini, Malawi, Zambia na kadhalika, wanapita Tanzania. Vituo vyetu vya pembeni upande wa Uganda, upande wa Kenya, Rwanda, Burundi zimewekwa vipi? Kwa maana ya kwamba, vinaangaliwa vipi ili uhamiaji haramu usiwepo? Kwa sababu kuna njia za mpenyo mpenyo nyingi ambazo hazina ofisi, hazina usalama, hazina kuangaliwa kwa vyovyote vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna eneo la Mutukula. Sehemu hii ya Mutukula watu wa Uganda ndio wanapita pale; kuna Holili, watu wa Kilimanjaro na Kenya wako pale, Kenya wanaingilia pale; Horohoro, watu wa Kenya na Tanga kule wanaingilia pale Horohoro; Rusumo,

Kagera, Rwanda Burundi, wanaingilia pale Rusumo; na Kasumula, eneo la Kyela, Mbeya mpaka Malawi wanaingilia pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nanukuu, "Tarakea, watu wa Kenya; Namanga, Kenya; Sirari, upande wa Kenya; Mwanza, ni Kenya na Uganda; Tanga, Tanga Mjini; Lindi, wanatokea Msumbiji; Kilambo, wanatokea Msumbiji; Ruvuma pale Msumbiji; Tunduma, Mbeya; Zambia na Malawi wanapitia pale; Mtambaswala, Msumbiji na Afrika ya Kusini wanapitia pale."

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo hivi vimewekwaje katika ulinzi ili tusiwe tena na watu wanaoingiza bidhaa za haramu, wanaingia wenyewe kwa wenyewe, yaani Wahamiaji haramu? Ningeliomba sana Afrika Mashariki iangalie, mipenyo yote inayoingia kwenye nchi nyingine idhibitiwe kwa usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, ni suala la Utalii. Tulipata taarifa kwamba Tanzania ni moja kati ya nchi ambazo zimepata sifa ya kuwa na Miji mikongwe, *old cities.* Miji hii mikongwe, ilikuwa imewekwa rasmi, kwamba hii itakuwa miji mikongwe na kwamba Umoja wa Mataifa na *UNICEF* watasaidia katika kuendeleza miji hii Mikongwe. Miji hii, mikongwe ipo Kenya, ipo Tanzania.

Sasa ningeliomba kujua Serikali imefutilia kwa kiasi gani suala hili? Kwa sababu *UNICEF* na nchi nyingine, kama Uingereza, Japan, na Ujerumani wanatoa fedha kwa ajili ya kuendeleza miji hii. Sisi Tanzania hii miji imeendelezwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya kuna Mombasa; Mogadishu, Somalia; Lamu, Kenya; Zanzibar, Tanzania Visiwani; Kilwa, Lindi. Naomba sana na sisi angalau kimoja tu tujue kwamba kinaendelezwa vipi katika Tanzania? Maana Tanzania nzima Kilwa ndiyo imebeba uzito huo. Katika Tanzania Bara Kilwa ndiyo iliyobeba uzito wa *heritage* hiyo, *w*anasema *old cities,* imebeba uzito ule. Tunasaidiwaje na Umoja wa Mataifa? Kwa sababu ilianza tangu mwaka 1981.

Kilwa ilitambuliwa mwaka 1982. Sasa inaendeleaje? Tunataka kufahamu.

Suala lingine ni lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili sisi Tanzania ndio walengwa wa lugha ya Kiswahili na sisi ndio hasa tulipaswa kuwafundisha nchi nyingine, na Zanzibar ndiyo kituo au Chuo cha Kiswahili kwa sababu wenzetu wameendelea vizuri sana kwa Kiswahili. Hata wakizungumza humu ndani utasikia Yakhe Yakhe! Inapendeza, mtu tunavutiwa na Kiswahili. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, Kiswahili tumekabidhi Zanzibar. Sasa Kiswahili hiki kinataka kuwa ajira Tanzania kwa sababu tunahitaji kuwafundisha watu wa Rwanda, Burundi, Uganda na Watanzania wenyewe wengine hata hawajui lugha ya Kiswahili. Hata wakizungumza wanachanganya Kiingereza na Kiswahili, basi ili mradi lakini watu wengine hawawezi kusikia. Mtu azungumze Kiswahili kile hasa Kiswahili! Tanzania ina dhamana hiyo ya kuwa na Waswahili wengi na Chuo cha Kiswahili. Tanzania tunajiandaa vipi katika ajira hiyo ya kufundisha Kiswahili katika mataifa mengine ya Rwanda, Burundi, Kenya na Uganda? Mheshimiwa Waziri hilo katika majumuisho yako naomba utuambie kwamba Tanzania inajiandaa vipi?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, hiyo ni kengele yako ya pili!

MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana na nakushukuru sana Mheshimiwa Fatma Mikidadi na hasa katika ile radha ya yakhe yakhe! Kwa kweli nafikiri hata wenzetu wa Zanzibar itabidi muwe mnatufundisha hii habari ya yakhe yakhe! Nakushukuru Mheshimiwa Mikidadi. *(Kicheko)*

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kuwasilisha Hotuba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo ningependa kupatiwa ufafanuzi katika Wizara hii. La kwanza ni mafao ya Wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nilipochangia Hotuba ya Waziri wa Uchukuzi, niliulizia kuhusu malipo ya wastaafu wa iliyokuwa *East African Railways* imefikia wapi? Wapo wazee wengi sana bado wanahangaika kupata mafao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira; kwa kuwa kuna utofauti wa mitaala ya elimu katika nchi zetu, pengine Wizara ingetuondolea wasiwasi au utaratibu utakaotumika endapo zitatolewa nafasi za ajira katika jumuiya yetu au vigezo vitakavyotumika kuwa na nafasi sawa za ajira kwa nchi zote ili kujiondolea wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa napenda kujua ni lugha gani Jumuiya hii imepanga kuitumia, kwa sababu naona Bunge la Afrika Mashariki bado linatumia Lugha ya Kiingereza. Je, ni lini Bunge hili litabadili Lugha ya Kiingereza kutumia Kiswahili ili Wananchi wa nchi zote zilizo katika Jumuiya hiyo wapate haki ya kujua mambo yanayoendelea katika Jumuiya yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna Sheria tofauti za umiliki wa ardhi kati ya nchi zilizo Mwanachama wa Jumuiya hii; je, suala hilo limekuwa vipi? Mfano, umiliki wa ardhi kwa nchi yetu ya Tanzania unapatiwa muda wa umiliki wa Serikali inaweza kufuta umiliki wakati wowote na wenzetu Kenya ukipatiwa umiliki wa ardhi ni wa moja kwa moja; je, Wananchi wana uelewa kiasi gani juu ya jambo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali ni vyema mambo mengine tusiende haraka au umoja huu

uchague baadhi ya mambo ya kuungana, mengine kila nchi ibaki kama ulivyo katika nchi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya chini ya Waziri na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufafanuzi wa mambo yafuatayo:-

Kwanza, nashukuru sana kwamba, ndani ya Jimbo letu tunayo masoko matatu ya mipakani; Mnanila, Nyamugali pamoja na Kilelema. Tatizo lililopo ni kwamba, tumeanza kujenga Soko la Nyamugali Wilaya mpya ya Buhigwe, ambalo litahitaji daraja la kuunganisha Tanzania na Burundi ili biashara iweze kufanyika kwa ufanisi zaidi. Nilitaka kujua Wizara hii imejipanga vipi kufanikisha tatizo linalotukabili? Pia tutakapoanza kujenga Soko la Mipakani la Kilelema; Wizara imejipanga vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpaka wa Tanzania – Mnanila – Manyovu na Burundi ni lini utatumika kikamilifu kupitisha mizigo kwenda Burundi, magari *(IT)?* Tunaomba mpaka huu ambao una miundombinu uanze kutumika kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujirani mwema; sisi Jimbo la Manyovu tuko mpakani na Burundi na Wananchi wote wanafanya biashara ndogo na kubwa, lakini Polisi wamekuwa wanakwamisha juhudi nzuri za Wananchi kujipatia kipato kwa kuwakamata mara kwa mara. Ninaomba Wizara itoe tamko juu ya biashara hii inavyotakiwa kufanyika katika Jumuiya hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Je, watu wanatakiwa kuvuka? Je, watu wanatakiwa kufanya Biashara? Je, Polisi wanatakiwa kukamata maharage, ndizi na kadhalika? Je, watu wa Burundi wanatakiwa kuja Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hasa Mkoa wa Kigoma, tumehifadhi Wakimbizi wengi toka Burundi, Jamhuri ya Kongo na Rwanda, lakini nini faida ndani ya Mikoa ambayo tumefaidi; hata lami hakuna, mashule hakuna, vyote hata faida hakuna. Nini faida ya Wizara yako kusaidia ili Mkoa na Wananchi waone manufaa yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalizo; Wananchi wa Tanzania na Kigoma hawajui Jumuiya ya Afrika Mashariki na faida zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema sasa Kiswahili kikatumika katika Bunge la Afrika Mashariki, kwani tulishapitisha Azimio la Kiswahili kutumika Afrika Mashariki. Sambamba na hilo ni lazima sasa kufanya kila hali na kufanya utafiti juu ya kuwepo kwa nafasi za kazi ya kusomesha Kiswahili *EALA*. Muhimu zaidi, kusomesha Vijana wa Kitanzania ili wawe na upeo na waweze kuajirika na kufanya kazi hizo kwa uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kuwa, tuwe makini sana kwa suala la kuanzisha sarafu ya pamoja, kwani tumeshuhudia tafrani kubwa iliyowakumba wenzetu waliotumia *Euro Zone* huko Ulaya. Pesa yetu inashuka mara kwa mara tofauti na wenzetu Kenya; ni vipi tutaendesha nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji katika Ziwa Victoria yanapungua siku hadi siku, ningependa kujua *EALA* ina mkakati gani kwa hili? Tunashuhudia maji hayo yakiendelea kupungua kwa kasi, ni vyema mkaja na mkakati na kutufahamisha kuwa nchi ambazo haziguswi na Ziwa hili itakuwaje na itasaidiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wengi bado wana malalamiko na Umoja wa Forodha na baadhi yao hawajafahamu ilivyo; basi hili ninyi kama Viongozi kuna nafasi yoyote mnachukua kuwaelimisha wafanyabiashara hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta za Huduma ya Jamii zinahitaji uratibu wa karibu wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano ya kutunga Sheria mpya ya Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki *(Inter – University Council of East Africa – IUCEA),* yahusishe siyo tu Serikali na Viongozi wa Vyuo Vikuu bali pia Vyama vya Wahadhiri na vya Wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada ukishaandaliwa, Wizara iratibu mjadala katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(UDSM)* na Vyuo Vikuu vingine kuhusu Muswada huo. Aidha, naomba maelezo zaidi juu ya vigezo na hatua za ziada zinazohitajika kufanikisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(UDSM),* kinaingia katika orodha ya taasisi zilizobobea katika kuratibu Mpango wa *Open Health Initiative (OHI),* wenye kulenga kuchangia katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia 485, yenye kulenga kuboresha afya ya mama na mtoto wafikie Halmashauri ikiwemo ya Kinondoni. Udhamini wa *NORAD* kupitia *Clinton Health Initiatives* wapaswa kufuatilia kwa karibu na Wizara husika ili kuhakikisha malengo *(Targets),* kwa mujibu wa andiko la awali ya mradi yanafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama, nakala ya Rasimu ya Pamoja ya Nchi Wanachama wa Afrika ya Mashariki ya Hati ya Makubaliano *(MoU)* ya kukabiliana na ugaidi inapaswa kuwasilishwa kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama kabla ya Serikali kuendelea na hatua nyingine za majadiliano na kusaini. Hii ni kwa sababu

ya Al Shabab. Tanzania inapaswa kuwa na tahadhari katika masuala ya mapambano dhidi ya ugaidi ili kuepusha Nchi na Wananchi wasiathirike au kuathiriwa. Maandalizi ya Itifaki za Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Itifaki ya Utawala Bora. Aidha, itifaki zingine ziandaliwe kuhusu chaguzi na juu ya Uhuru wa Vyombo vya Habari pia, michakato ianzishwe ya kuunda Mabaraza ya Vijana na Wanawake ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la Afrika Mashariki; pamoja na Wizara kuleta orodha ya Miswada iliyopitishwa na Maazimio, ifanye utaratibu wa kutoa nakala za Sheria na Maazimio yote yaliyopitishwa wakati huu wa Bunge la Kumi kwa Wabunge. Aidha, Wizara iweke mfumo na Miswada kabla ya kupitishwa na Bunge hilo, orodha itolewe kwa Wabunge wote na nakala ziwe katika Ofisi na Maktaba ya Bunge ili Wabunge wanaotaka kuipitia na kutoa maoni wafanye hivyo.

Pia, Miswada hiyo ipitiwe na Kamati za Kisekta za Bunge la Tanzania ili Wabunge wetu waende wakiwa na maoni ya Wabunge wa Tanzania, ambao kimsingi ndiyo wapiga kura na wawakilishi kwa niaba ya Wananchi wote kwa kuzingatia Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Nchi. Mahakama ya Afrika Mashariki, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, itoe elimu kwa Umma kujua haki zao kwa msingi wa Mkataba wa Afrika Mashariki, Itifaki na Sheria za Afrika Mashariki, waweze kuitumia Mahakama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji kwa mwaka 2012/2013 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2013/2014 yanaonesha bado kuna changamoto nyingi katika kuhakikisha ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kujenga Jumuiya iliyoshamiri na wenye tija na unaolinda masilahi ya Taifa. Katika muktadha huo, naomba kutoa mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa hatua za mtangamano: Wizara ieleze sababu ya kuchelewa kwa marekebisho ya sheria zote ambazo zinahitajika kuiwezesha

Tanzania kunufaika na fursa za Soko la Pamoja. Katika majumuisho, Wizara itaje orodha ya sheria zinazohitaji kurekebishwa na kutoa ahadi ya kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali, wenye kulenga kuwezesha Tanzania kunufaika na soko la pamoja badala ya kusubiri kuingiza vifungu kidogo kidogo kupitia njia nyingine za marekebisho. Kwa upande wa Umoja wa Fedha, Serikali kupitia Wizara ya Fedha ieleze sababu za Tanzania kushindwa kufikia vigezo vya muunganisho wa uchumi mpana *(macro economic convergence)* na mkakati wa kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mkakati gani umewekwa kulinda uchumi wa ndani kabla ya kuanza kwa Umoja wa Fedha ili kuepusha madhara kama yanayotokea kwa sasa katika eneo la Umoja wa Fedha wa Wilaya. Juu ya Shirikisho la Kisiasa, wakati Serikali kwa upande wake ikiendelea na uchambuzi wa rasimu ya mapendekezo ya muundo na modeli ya shirikisho, Wabunge tupewe nakala ya rasimu hiyo. Hali ya soko la pamoja na mwelekeo wa majadiliano ya Umoja wa Fedha na Shirikisho la Kisiasa inahitaji mchakato wa kukamilisha Sera ya Utengamano uharakishwe na kukamilika katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014. Hatua hiyo iambatane na kuanzisha Kitengo cha Utafiti katika Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na kushirikisha Idara za Sera na Mipango za Wizara za Kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa miundombinu ya kiuchumi; naomba katika majumuisho nipewe majibu wa masuala niliyoyahoji mwaka 2012 wakati wa mjadala wa Bajeti ya 2012/2013, juu ya Miradi inayogusa Jimbo la Ubungo na Jiji la Dar es Salaam, ambayo Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ina nafasi yake katika uratibu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara iratibu kwa karibu zaidi miradi kipaumbele iliyoidhinishwa na wakuu wa nchi hususani kuongeza kina cha Gati Namba 1 – 7 katika Bandari ya Dar es Salaam, miradi ya uendelezaji wa barabara za kupunguza msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam ambazo ni Banana – Tangi Bovu na upanuzi wa Barabara ya Morogoro, miradi ya uendelezaji wa nishati na uzalishaji wa

umeme hasa katika maporomoko ya Mto Rusumo kwa kuwa miradi mingine kama ya Kinyerezi na Kiwira ina vyanzo vingine vya fedha.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa moyo wa dhati, kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na Mawaziri wote wanaohusika na masuala ya Afrika Mashariki, kwa namna ambavyo nchi zetu hizi zinavyozidi kuelewa na kuendeleza mtangamano huu wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya changamoto ambazo hata Wizara husika imekiri kuwa ni tatizo kwao ni elimu kwa Umma.

Naiomba Wizara pamoja na Wabunge wetu wa Jumuiya, kutumia nyenzo zake zote ili kutoa elimu kwa Wananchi wetu, kwani hali halisi inaonesha bado uelewa wa Wananchi katika mtangamano huu ni mdogo sana na hii inasababisha Wananchi walio wengi kutokuchangamkia fursa nyingi ambazo tayari zinapatikana kwa kuwepo utengamano huu. Kukosekana na uelewa huo bado vijana wetu hawajatayarishwa au kuelimishwa kuingia katika soko la ajira. Hata baadhi ya wafanyabiashara wetu wanaogopa kutumia fursa hii katika Sekta ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa lengo la Jumuiya hii ni kufikia katika Shirikisho. Ninaiomba Wizara kutofanya haraka kuwa na sarafu moja hadi pale Sera zetu za Fedha zitakapowiana.

Naiomba Wizara kuangalia mfano wa Nchi au Jumuiya *ya Scandinavian Countries (*Norway, Sweden na Denmark), ambazo zinatumia sarafu moja ya *Coron,* ambapo thamani ya fedha hiyo haina tofauti kubwa baina ya nchi moja na nyingine, bali hadi leo hii bado hawajafanikiwa katika hilo. Utofauti uliopo wa thamani ya fedha katika Nchi

za Afrika Mashariki bado ni mkubwa mno, naiomba Serikali isifanye pupa kuingia au kuunda Umoja wa Sarafu hadi pale Sera zetu za Fedha zitakapowiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Jumuiya kwa kuweka Ofisi za Jumuiya pale Zanzibar. Hali halisi inayojionesha ni kwamba, bado Miradi ya Maendeleo kwa Zanzibar haijawa kipaumbele kwa miradi hiyo ila mradi mmoja tu wa Bandari ya Maruhubi, ambao umekuwa kama hadithi tu ya kupamba Ripoti za Wizara, bali hakuna hatua zozote za dhati ambazo zinaonekana. Kwa hakika tumechoshwa kusikia Mradi huo uko katika upembuzi yakinifu kila mwaka; ni vyema Waziri atupe maelezo ya kina ni kwa namna gani upembuzi huu yakinifu umekuwa wa muda mrefu bila majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili iliyopita Wizara iliainisha ujenzi na utanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Karume kule Pemba. Je, ni hatua gani zimefikiwa hadi sasa kuhusu utanuzi wa Uwanja huo? Utanuzi wa Uwanja huo wa Ndege si tu utasaidia kukua kwa Uchumi wa Visiwani bali itakuwa ni kiungo katika nchi zetu za Jumuiya hii.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa Hotuba nzuri na kwa kazi ngumu wanayofanya pamoja na bajeti finyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninayo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamekuwa na utaratibu ambao haufuatiliwi wa kwamba, Sheria zinazopitishwa na *EALA* zina *supersede* Sheria zote za *Partner States*; je, ni Sheria ngapi au maamuzi mangapi yaliyopitishwa na kuletwa kwenye Nchi zote za Jumuiya na kufanyiwa kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamekuwa na malalamiko mengi kuhusu utendaji wa baadhi ya Wabunge wetu wa *EALA* hasa Kamati ya *TRADE,* kwani *East Africa is all about*

Trade. Mwenyekiti analalamikiwa kuwa hafifu sana na kuonesha kuwa Tanzania ina uwezo mdogo sana, mbali na malalamiko ya wao kuvutana wao kwa wao. Wizara inachukua hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna haja ya kuelimisha zaidi na zaidi Wananchi wetu ili waendane na kasi ya *East Africa* kwa maana ya maendeleo. Tuendelee kushirikiana kwa kutumia mbinu mbalimbali ili kuelimisha watu au Wananchi wetu.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Sitta, Naibu Waziri na Timu nzima ya Wizara, kwa kazi nzuri mnayoifanya katika kuisimamia Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote, mahusiano ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, naomba chonde chonde majirani zetu tusiwaruhusu hata kidogo kuwamilikisha ardhi yetu. Mengine yote tufanye, lakini kwenye ardhi yetu hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiruhusu umilikishaji ardhi tumekwisha, nchi itajaa watu wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara ambayo imeboresha kuleta umoja na mshikamano mkubwa baina ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, uhuru mkubwa uliotolewa katika uingiaji wa raia ambao ni wa Nchi Wanachama wa Jumuiya, unatia shaka kutokana na uaminifu mdogo walionao baadhi ya raia hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivi kutokana na wasiwasi wangu kwamba, mipaka ya nchi yetu haipo salama kama ambavyo tunaamini, kiasi ambacho uhuru huu unawezesha kuingizwa kwa silaha nchini mwetu kinyume cha Sheria. Jambo ambalo linaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa

maisha ya Watanzania ambao hawana hatia, lakini vilevile kukaribisha ujambazi kutoka miongoni mwa raia wanaotoka miongoni mwa Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama wa Jumuiya zilikubaliana kuwa na soko la pamoja la biashara. Mwaka jana katika kujadili Hotuba ya Waziri hii, kulitokea malalamiko dhidi ya chupa ambazo zilikubaliwa na Nchi ya Kenya kuhusiana na ukubwa na viwango, lakini Viwanda vya Tanzania vilipofuata viwango vilivyowekwa na Kenya, Nchi ya Kenya ilibadilisha Sheria ya Viwanda vipya na kusababisha chupa zilizotolewa Tanzania kuonekana hazifai na hivyo kusababisha hasara kwa Viwanda vya Tanzania. Je, hatuoni kwamba tatizo hili limefikia wapi? Hatua gani iliyochukuliwa na Serikali juu ya suala hili; kama hakuna hatua zilizochukuliwa hatuoni kwamba hili linaanza kuitia doa Jumuiya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni miongoni mwa Nchi Waasisi wa Jumuiya hii ya Afrika Mashariki. Katika Jumuiya kuna nafasi za ajira ambazo zinatolewa kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya. Mheshimiwa Waziri anaweza kutueleza Jumuiya ina waajiriwa wangapi? Na je, ni wangapi kutoka kila Nchi Wanachama wa Jumuiya? Kwa kuwa Tanzania ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar; kuna wafanya kazi wangapi kutoka Tanzania Bara na Watanzania Zanzibar wangapi walioajiriwa katika Jumuiya hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina Sekta nyingi za Utalii zikiwemo Mbuga za Wanyama kama vile Serengeti, Ngorongoro, Manyara na Mikumi. Vilevile Milima Kilimanjaro, Majengo ya Kale na Bandari zenye fukwe zenye kuvutia, jambo ambalo linaweza kuiingizia nchi yetu mapato makubwa. Je, Wizara hii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imechukua hatua gani katika kuitangaza Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi katika kujibu suala zima la ujenzi wa Bandari ya Micheweni kama Mradi uliopendekezwa na Jumuiya, ilisemwa kwamba, Bandari hiyo haimo katika vipaumbele vya Jumuiya. Vilevile ikasemwa kwamba, eneo hilo halifai; je, hakuna sehemu yoyote katika

bandari zote zilizomo katika Wilaya hiyo ambayo inaweza kupewa kipaumbele cha kujengwa Bandari hasa ikitiliwa maanani kwamba Wilaya hiyo imepakana na Nchi ya Kenya?

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kutoa pongezi kwa kuwa na Jengo la Afrika Mashariki na hivi sasa vikao vyote vitafanyika Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwendo wa bidhaa kutoka nchi moja kwenda nyingine kutokana na udhaifu wa miundombinu hasa barabara na reli kwa upande wa Tanzania, bidhaa hizo kupeleka nchi jirani, lakini pia mlolongo mrefu wa magari kwenye mizani yetu, ni kikwazo cha pili. Namwomba Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauru wa Zanzibar ndani ya *EAC*. Zanzibar inashikirishwaje katika kuhakikisha michakato ya kuwa nayo inufaike na uwepo wake ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki? Pia Zanzibar huwa kuna Miradi na mingine inaibuliwa; je, ni sifa gani hasa Mradi inabidi uwe unazo? Mheshimiwa pia atueleze njia ya kupita hiyo Miradi ipate ufadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili hivi sasa kinatumika karibu nusu nzima ya Bara la Afrika Mashariki na hata Nje ya Bara la Afrika. Chanzo cha Kiswahili hasa ni Tanzania, jitihada za ziada zitumike ili kiweze kuwa cha fasaha na hatua za makusudi zifanyike kulitaka Bunge la Afrika Mashariki litumie Kiswahili na hasa hawa Wabunge wetu kutoka Tanzania; kwa nini hawapeleki yenye manufaa ya nchi yetu kwa Lugha ya Kiswahili? Tunawaambia sisi wapiga kura wenu Bunge la Afrika Mashariki mwakani liwe limeshapitisha Muswada wa kutumia Kiswahili Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hatua inayofuata ni kuwepo na sarafu moja, Wananchi wana wasiwasi wa jambo hilo; ni vyema elimu ya kutosha itolewe kwa Wananchi na ipewe muda wa kutosha. Kwa kuwa hatua ya mwisho ni ya siasa ya pamoja, mambo hayo yajadiliwe baada ya miaka 20.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa Nchi za Afrika Mashariki zimeridhia itifaki ya kuanzishwa kwa ajira katika nchi husika; ni kwa namna gani Tanzania imewandaa vijana wake katika ushindani huu? Hakuna asiyefahamu kwamba ili kijana aweze kushindana vyema ni lazima awe ameandaliwa vizuri kielimu katika ngazi zote. Hali ilivyo sasa kwa Tanzania ni kwamba, Elimu hasa ya Juu imekuwa haiwafikii au kuwapa nafasi vijana wengine wanaoitamani kupata. Hii inatokana na ubaguzi unaofanywa kwenye utoaji wa mikopo katika baadhi ya kozi. Mfano, Serikali inatilia mkazo kwenye masomo ya Sayansi na Uchumi pekee katika utoaji mikopo.

Je, imeshajiridhisha kwamba ina wanataaluma kama wanauchumi, wahasibu, wakaguzi wa mahesabu, Sekta ya Utalii, wana mzigo waliosomea na kadhalika wa kutosha? Ni kwa nini isione kwamba inapokuja kutika suala zima la ajira mbalimbali vijana wengi wa Kitanzania wataachwa nyuma?

Je, Serikali imeweka mkakati gani wa makusudi wa kutenga ajira ambazo zitakuwa ni pekee kwa Vijana wa Kitanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu sasa Serikali kupitia Wizara hii, imekuwa ikishauriwa kuanzisha Kitengo cha Utafiti katika Wizara hii, lakini mapaka sasa bado hatujasikia chochote kuhusu uanzishwaji wake. Sote tunafahamu kwamba, *no research, no right to speak* au kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba, bila utafiti huwezi kulizungumzia jambo kwa ufasaha. Sasa kama Wizara haina Kitengo cha Utafiti mpaka sasa ni kwa namna gani inaweza kutambua mambo muhimu ambayo yanatakiwa kuwepo kwenye ushirikiano huu? Ni kitu gani kinakwamisha uanzishwaji wa Kitengo hiki muhimu sana kwa mustakabali wa ushirikiano wa Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wanaowakilisha Bunge la Afrika Mashariki wameonekana kutokuwa na mahusiano mazuri na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania hasa ya kiutendaji na kimaamuzi. Ni vyema Wabunge wa Afrika Mashariki kabla ya kuingia mkataba, kutungwe Sheria, Itifaki na kadhalika, wakiwasiliana na Bunge letu ili kitakachoamuliwa kiwe na baraka kwa Wananchi wa Tanzania kupitia wawakilishi wao ambao ni Wabunge. Kufanya maamuzi bila kushirikisha Wananchi wa Tanzania ni suala ambalo hapo baadaye linaweza kuleta migogoro isiyo na mwisho na kuathiri ushirikiano huu ambao una tija kubwa kwa nchi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna malalamiko mengi kwamba, Wizara ya Afrika Mashariki haina mahusiano mazuri na Wabunge wake na hivyo kufikia hatua ya kutupiana maneno yasiyokuwa na staha kati ya Wabunge na Mawaziri husika. Hii ni aibu kwa nchi yetu na haileti afya ya ushirikiano na nchi nyingine kama suala hili litaendelea bila kukomeshwa wazi kwamba, itafika mahali hata Wabunge wengeni wasio waaminifu kuisema nchi yetu vibaya mbele ya wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara ifanye jitihada ya kutatua tatizo hili haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mungu, kwa kunipa nafasi ya kutoa mawazo yangu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kupendekeza kwa matumizi ya Lugha ya Kiswahili kama Lugha Rasmi ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuona Wizara hii inachukua hatua za haraka na za makusudi kama kweli nchi yetu inataka kufaidika na fursa ni vizuri kuitangaza kwa kutumia ushawishi wake wa uzoefu wa matumizi ya lugha hii ili iwe rasmi na Watanzania ambao ndiyo watumiaji na wafundishaji wa lugha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama tukifanikiwa katika hili hasa kwa kuwapa jukumu la kuhakikisha haya, Wabunge wetu wa Afrika Mashariki kulipa kipaumbele kwenye vikao vyao, ninao uhakika kazi itakuwa kubwa sana na mafanikio yataonekena kwa kipindi cha muda mfupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea kuyasikia majibu ya kina kutoka kwa Waziri ili basi angalau tujue ni namna gani watu wetu wanajiandaa na fursa iliyopo hasa katika ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuungana na kauli ya Waziri kulaani kitendo cha Gazeti la Nchi jirani kwa kuchora kikaragosi cha udhalilishaji wa Bunge la Tanzania. Hicho ni kitendo cha dharau iliyopitiliza siyo tu kwa Bunge bali pia kwa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukumbushia ujenzi wa reli na Bandari ya Musoma. Jambo hili limeongelewa sana na sasa limeanza kuonekana ni kama blah blah za Jumuiya. Akijibu hoja za baadhi ya Wabunge, Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi alisema, Bandari ya Musoma ipo kwenye mipango ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Napenda sasa kuchukua fursa hii kuuliza ni lini Reli ya Tanga na Bandari ya Musoma itaanza kujengwa rasmi ili kuanza kufungua rasmi fursa za kiuchumi zilizopo na zitakazojitokeza watu wetu waanze kunufaika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nitapata fursa ya kuchangia kwa maandishi, basi nitasisitiza ujenzi wa Reli ya Tanga na Bandari ya Musoma na pia katika ufafanuzi wa Wizara nitapenda kulisikia hilo.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelewa Zanzibar siyo mwanachama wa moja kwa moja wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, kwa sababu ushirikiano wa Kimataifa ni suala la Muungano. Hali hiyo inasababisha kutokuwa na Wajumbe tisa kama zilivyo Nchi Wanachama na pia Zanzibar haiwezi moja kwa moja kuomba Miradi ya Maendeleo kwenye Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Kwa mtazamo wangu, Zanzibar kukosa nafasi hiyo, tumekosa nguvu za kura kwenye Jumuiya hiyo, ingekuwa Tanzania tuna kura 18 pia tumejiwezesha nafasi pana ya kuomba Miradi kwenye Jumuiya. Leo Miradi inayoidhinishwa kwa Tanzania Bara na Zanzibar inahesabiwa ni Miradi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki sehemu kubwa kwa wakati huu inashughulikia mambo ya kiuchumi na Miradi ya Maendeleo. Je, Wizara haioni haja ya kufanya marekebisho ya mazingira inayofanya Zanzibar kutumiwa ujumbe wa moja kwa moja ili iwe Mjumbe kamili kama ilivyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ya mwanzo iliyoundwa mwaka 1967.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgao wa soko *(market share)* miongoni mwa nchi za Afrika ya Mashariki, Kenya wanaongoza kwa kuwa na asilimia 36 wakati Tanzania ni asilimia 24. Je, nchi yetu imekosa mambo gani ikapitwa na Kenya wakati Tanzania ni kubwa ina watu wengi? Ni vipi Tanzania au wafanyabiashara wa Tanzania wamekosa soko mgao wake ukawa mdogo kuliko Kenya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inavyoonekana kuna fursa nyingi za uwepo mtengamano katika Afrika ya Mashariki hususan kwenye eneo la biashara, lakini uelewa wa wafanyabiashara wetu bado ni mdogo. Je, Wizara ina mkakati gani wa kutoa elimu kwa Wafanyabiashara wa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Waziri, ukurasa wa 23, kifungu cha 33, pamoja na maelezo mengine pia imeelezwa kuwa, suala au changamoto ya biashara ya magendo ya Karafuu kutoka Zanzibar imeondolewa. Ninamwomba Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake, anipatie maelezo ya kina changamoto hiyo imeondolewa vipi ili na sisi tujue? Je, hakuna vipenyo vingine ambavyo vinaweza kusababisha biashara ya magendo ya karafuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali na Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, kwa hotuba nzuri, yenye mipango mizuri kwa Wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali pamoja na mambo yetu, ijipange kupambana na Soko la Jumuiya. Sababu za kusema hivyo ni kutokana na hali yetu halisi kama Watanzania kutoweza kubadilika kiutendaji na hasa kufanya kazi kwa haraka na bidii kubwa yenye mafanikio makubwa.

Ushauri wangu; elimu itolewe kwa vijana wetu waelewe tunakotoka na tunakoenda na jinsi ya kupambana na Soko la Afrika Mashariki.

Mhe
shimiwa Mwenyekiti, nashukuru Tanzania na Watanzania, baadhi yao wameamka wanafanya biashara katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa kupeleka mizigo Rwanda, Burundi na Kongo. Haya ni maendeleo makubwa sana japo wanapata changamoto kubwa ya vituo vya ukaguzi na *TANROADS*, hali hiyo inawapunguzia faida ya biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Walimu wa Tanzania kutofundisha shule za nchi za jumuiya lakini wao wanakuja kufundisha kwetu; Serikali imegundua tatizo ni nini na ushirikiano mzuri si Wanajumuiya wote kuchanganyika; inakuwaje wao wanakuja sisi hatuendi?

Gharama za Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki ni vyema Serikali ikasimamia umoja katika elimu kwa kuangalia uwiano wa gharama za Vyuo Vikuu. Wanafunzi wetu wanaenda wengi sana na wanapata elimu; je, Serikali inawasaidiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki imeisaidiaje Bandari yetu ya Dar es Salaam kuongeza wateja kupitia Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri.

MHE. SELEMANI SAIDI JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mapendekezo yafuatayo:-

Kuongeza wigo wa elimu kwa Wakazi wa Tanzania ili kunufaika zaidi na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Uelewa mpana utawawezesha Watanzania kushiriki vyema katika kuchangamkia fursa za kimaendeleo katika soko la pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iweke mkakati mpana wa kuwajengea uwezo vijana wasomi wa Kitanzania ili waweze kushindana vyema katika fursa za ajira katika nchi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kutopupia mambo mpaka pale inapoona yana maslahi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali au Jumuiya ya Afrika Mashariki kuimarisha Lugha ya Kiswahili kama njia kuu ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu *(S.W.)*, kwa neema na rehema zake nyingi kwangu, familia yangu na Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina umuhimu wa kipekee katika mustakabali wa nchi yetu kwani umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Umoja wenye nguvu ni ule wenye nia na dhamira iliyo njema kabisa miongoni mwa wanaounda umoja huo. Kwa mantiki hiyo, naiomba na kuisihi sana Serikali yetu iwe makini sana katika mchakato huu wa kuunda umoja huu ili tufaidike na fursa zitakazopatikana na tusifisidike.

Sina wasiwasi na uwezo na umakini walionao Waziri na Naibu wake wa Wizara hii. Wasiwasi wangu ni kwa wataalamu wetu wasije wakashawishiwa vibaya kwa kufuata tamaa zao binafsi za kimaslahi na kutupeleka pabaya. Nashauri na kusisitiza juu ya hili kutokana na matukio mengi ya kimaslahi ya nchi kama mikataba ya madini; misamaha ya kodi kwa makampuni makubwa ya kigeni na hata mikataba ya ukandarasi wa miradi mikubwa ya ujenzi kutoleta tija inayostahili kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba kuwasilisha. Mungu ibariki Tanzania.

MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano huu ni kitu muhimu sana hasa katika kukuza maendeleo katika nchi zote wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na suala la ulinzi; naiomba Wizara hii ifanye mazungumzo ya pamoja hasa katika kulinda mipaka ya nchi. Ulinzi uimarishwe kwani nchi nyingi hivi sasa zimekuwa zikikumbwa na migogoro inayosababisha machafuko na kuvuruga amani iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni elimu. Kumekuwa na ufundishaji ambao unaleta utengano katika nchi hizi; mfano, wanafunzi wanaokwenda kusoma nje wanatumia Kiingereza zaidi na kusababisha imani potofu kuwa elimu bora ni kujua Kiingereza na kudharau Kiswahili.

Naiomba Serikali kupitia nchi hizi za Afrika Mashariki, ikae pamoja na kuona sasa ni wakati wa kukitangaza Kiswahili na kukipa kipaumbele ili kuokoa Kiswahili fasaha ambacho kinapotea sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya maeneo ambayo Watanzania wanatakiwa kunufaika nalo ni Soko la Ajira ndani ya Jumuiya. Hadi kufika sasa bado Nchi Wanachama hawana Sera zinazowiana katika elimu. Ikiwa Tanzania haijaweza kujipanga kulinda ajira, basi nchi itajiweka pabaya na haitakuwa na manufaa yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhuru wa kila Mwananchi katika nchi Wanachama kuweza kuishi popote bila sharti, utanyima fursa kwa Watanzania kwani bado nchi kama Kenya na Uganda wanabagua sana Watanzania ambao huwa wanafika kutafuta fursa za ajira na uwekezaji. Wizara ifanye jitihada ya makusudi kuelimisha fursa za kiuchumi zinazoweza kupatikana katika Soko la Pamoja la Jumuiya. Tanzania ni nchi pekee katika Jumuiya ambayo imebakiwa na ardhi ya kutosha. Tusipochukua hatua madhubuti, itasababisha Wananchi wa Tanzania kuvamiwa na kukosa ardhi. Ardhi yetu ilindwe.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kwanza, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, kwa kuniwezesha kuchangia Bajeti hii ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ya Mwaka 2013/2014. Pia nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Watumishi wote wa Wizara hii na kuweka mikakati mizuri ya kuendeleza ushirikiano uliopo uzidi kukua, pamoja na nchi zote zilizopo katika Ukanda wa Afrika Mashariki. Bajeti hii imezingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kuhakikisha ushirikiano wa Nchi za Afrika Mashariki unaendelea kudumishwa na kukua katika sekta mbalimbali. Tuendelee kuuenzi ushirikiano huu kwani unatupa fursa nyingi za kimaendeleo baina ya nchi zetu na kusaidia kupunguza umaskini uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kujipongeza kwa kuweza kudumisha ushirikiano na Muungano wetu tangu hapo awali mpaka hivi sasa. Jambo la kipekee na la kujivunia ni kwa Muungano wetu kuzidi kuwa imara kwani hivi sasa

Nchi za Rwanda na Burundi zimeshaingia katika Muungano na kufanya Muungano kuwa wa nchi zipatazo tano hivi sasa. Hili siyo jambo la kubezwa hata kidogo; ni jambo la kujisifu na kujivunia kwa ujasili tulionao kwa kuchukua maamuzi ya kuwa na Muungano huu na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kwani sisi siyo wa kwanza kufanya jambo hili na mifano ipo mingi kwa nchi zilizotangulia ambazo ziliungana na kupata mafanikio makubwa ya kimaendeleo na kiuchumi. Ushirikiano wa Afrika Mashariki umefanya tuwe na nguvu, kauli moja na kushirikiana katika nyanja mbalimbali za kibiashara, elimu, siasa na maendeleo kwa ujumla, lakini kuna baadhi ya changamoto ndogondogo ambazo kama Serikali zetu hazina budi kuzifanyia kazi.

Watanzania wengi hawana elimu ya kutosha kuhusu Muungano huu. Upungufu huo wa kutokuwa na elimu ya kutosha unafanya Wananchi kuwa na maswali na uwoga pia, kwani wanakumbuka jumuiya ya awali ambayo ilivunjika na baadhi ya Wananchi kuathirika kwa kiasi kikubwa, kwani walikuwa wamewekeza maeneo mbalimbali katika nchi zilizokuwa katika Muungano. Naiomba Serikali katika mchakato mzima wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaoendelea hivi sasa, watoe elimu ya kutosha kwa Wananchi ili kuwatoa uwoga waliokuwa nao wa kutokujua faida za Jumuiya na kuainisha mambo yote yatakayoleta faida katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi sana ya kuzingatia ili Muungano huu uendelee kutunufaisha nchi zote. Kila nchi ina sheria zake, kwa mamlaka zilizopo katika Muungano huu lazima sheria ziangaliwe ili zilete usawa kwa watu wote wa nchi shiriki bila kufanya wengine kuona hawajatendewa haki. Vilevile katika sheria hizo lazima suala la kuingia na kutoka katika Nchi Mwanachama bila kupata bugudha yoyote lizingatiwe ili kuwapa fursa Wananchi wote wanachama wa Jumuiya hii kuweza kuwa huru kuamua ni wapi wanaweza kufanya uwekezaji. Pia liangaliwe suala la Sera za Kodi na Ushuru wa Forodha kuwa na viwango sawa na kuhakikisha kuwa na soko huru la pamoja la mazao na bidhaa zinazotoka katika nchi hizi. Kuhakikisha Jumuiya ya

Afrika Mashariki kuwa na mipango mizuri kuhusu masuala muhimu yanayozikabili nchi hizi kama suala la Forodha, Usalama na Ulinzi, pamoja na Uhamiaji, viwango vya elimu na usawa wa kupanga bei ili kuwa na bei moja. Naishauri Serikali kufanyia kazi mikakati hiyo ili kuleta manufaa kwa Jumuiya nzima pamoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuikumbusha Serikali kuliangalia kwa mapana suala zima la ardhi katika Muungano huu, kwani nchi yetu imebarikiwa kuwa na ardhi kubwa na ya wazi. Kwa kuwa tunaingia kwenye Jumuiya, basi Serikali iangalie suala hilo katika makubaliano; hivyo, kusitoe mwanya katika suala la ardhi kuwa katika makubaliano na kufanya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuweza kumilikishwa ardhi yetu. Masuala ya ardhi yabakie katika mamlaka ya nchi husika. Naishauri Serikali suala la ardhi libakie kwa Taifa lenyewe ili kuweza kuwanufaisha Wananchi na kama ikitokea uwekezaji wowote, basi mzawa abaki na asilimia nyingi ili kuweza kulinda ardhi yetu na si mgeni kumilikishwa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na uwoga na wasiwasi baina ya Watanzania kuhofia kupoteza ajira zao pindi Jumuiya hii itakapoanza kufanya kazi, kwa kuwa nchi shiriki kama Kenya, kielimu na kiutendaji kwa raia wake wametuzidi kidogo. Naiomba Serikali itoe elimu ya kutosha kwa Wananchi jinsi ya kukabiliana na changamoto hiyo, kwani kumekuwa na matatizo katika hili. Jambo hili siyo geni kwani pale utakapoenda mahali kupata huduma yoyote na kumkuta Mkenya ndiyo mtoa huduma hiyo na jinsi atakavyokuhudumia ni tofauti kabisa na watu wetu, kwani wenzetu wamekuwa wako makini sana katika kazi, tofauti na sisi tumekuwa hatujali na kufanya kazi kwa mazoea. Ndiyo maana kumetawala uwoga huo, ila kwa kuwaelimisha basi wataweza kukabiliana na changamoto hizo ili na sisi tujijengee kufanya kazi kwa moyo na nguvu zote na si kwa mazoea kama ilivyozoeleka baina ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Mheshimiwa Waziri Samuel Sitta na Naibu wake, kwa kusimamia Jumuiya ya Afrika Mashariki huku wakihakikisha kuwa maslahi yetu kama nchi yanalindwa na kuendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirikisho la Kisiasa *EAC* liandaliwe bila ya kuharakishwa hadi hapo tutakapokuwa tayari. Shirikisho la Kisiasa lije baada ya kukamilishwa kwa Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja na Sarafu ya Pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi iendelee kutawaliwa na kusimamiwa na Sheria ya Nchi husika. Ardhi isiwe kamwe ni shughuli ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itoe msukumo wa ujenzi wa Masoko ya Mazao na Mifugo Namanga, Sirari, Holili, Mutukula Rusumo na Kigoma.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia njia ya maandishi, nichangie Bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hoja yangu ni fursa ya Wizara yetu katika kukaribisha na kuwezesha kujiunga wanachama wapya. Moja ya manufaa ya sisi kuwa katika Afrika Mashariki ni kuwa na uhakika wa soko kubwa. Ni ushauri wangu kuwa, jitihada zifanyike ili Nchi ya DR-Congo iwe sehemu ya Jumuiya. Hii ni nchi inayojengwa upya, yapo mahitaji makubwa ya vifaa vya ujenzi kama saruji ambavyo vinapatikana hapa. Kufuatia matumizi ya gasi asilia katika uzalishaji, mwakani bidhaa zetu zitakuwa na bei shindani kulingana na nchi zilizotuzunguka. Eneo tajwa pia linayo mahitaji makubwa ya chakula, fursa nyingine kwa Wakulima wa Tanzania.

Kwa uhakika wa soko kubwa, Watanzania wanaweza kupewa bei ya mazao kabla hata ya msimu wa kulima. Jitihada hizi ziende sambamba na kuendesha shughuli za mauzo nchi za nje kwa kutumia mfumo rasmi, yaani mauzo yote yawekwe wazi, mapato katika fedha za kigeni yatumike na kuwekwa benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwingine katika Wizara hii ni kuhamasisha Wananchi na Makampuni ya Kitanzania kujasiria Masoko ya Afrika Mashariki. Tunapaswa kuwa na makampuni na Wananchi wanaoendesha shughuli katika nchi zote za Jumuiya. Serikali kupitia Wizara ibebe jukumu la uhamasishaji kama nilivyodokeza. Fursa za kiforodha zinazotoa faida ya kiushindani kwa Kampuni za Kitanzania, itumike mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo Makampuni ya Mafuta ya Kitanzania yanayoendesha biashara nchi za DRC, Zambia Rwanda Burundi na hata Uganda. Muhimu kueleza kuwa, kampuni hizi zilikwenda huko kwa msukumo wa kukwepa sheria zisizo rafiki za *TRA.* Hoja hapa ni kuwa, tuwawezeshe Watanzania kujasiria fursa za soko kubwa na kutumia faida ya eneo tulipo *(Tanzania Location Advantage)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano ni pamoja na mahusiano mema. Naendelea kuomba na kuishauri kwa namna ya pekee, Wizara iwatake watendaji wenzao katika Jumuiya ili watu na Wananchi wao wawe na ushirikiano na uhusiano mwema na Watanzania. Ushirikiano wa Nchi za Afrika Mashariki siyo neno zuri kwa masikio ya baadhi ya Wananchi katika sehemu za mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa ni kuzitaka nchi jirani kuhakikisha watu wao wanapokuja nchini kwetu wanakuwa watu wema. Sambamba na hilo, Wizara nayo kwa kushirikiana na Wizara husika, wahakikishe Watanzania nao wanaendesha shughuli kwa kujenga mahusiano mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majukumu ambayo ni vyema Wizara ikayafuatilia ni kupunguza vikwazo vinavyochelewesha mizigo inayopitia bandari zetu kwenda nchi jirani, lakini pia wizi wa mizigo au bughudha yoyote kwa Wananchi wa Mataifa yaliyotuzunguka. Ni imani kuwa, kwa kuonesha imani na wema kwa wenzetu, nao taratibu watajifunza na kujenga mahusiano mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SALUM KHALFAN BARWANY: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu kwa maendeleo ya nchi tano za Afrika Mashariki; kuna umuhimu wa kutengewa pesa za kutosha hasa kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ni dhaifu hasa kwa upande wa Tanzania. Watanzania tuna kila sababu ya kuboresha miundombinu hasa ukizingatia kuwa, tumezungukwa na nchi ambazo hazina bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli yetu ni mbovu na ni ya viwango vya kizamani; hivyo, ni vyema Wizara ikafanya juhudi za makusudi ili tuwe na reli yenye ubora na ya viwango vya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatakiwa kuwa makini kwa lengo la kudhibiti uzito wa magari yanayosafirsha bidhaa kuelekea nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahusiano na nchi jirani yanaendelea vyema, ni vizuri Wizara ikaendeleza umakini katika ulinzi wa mipaka yetu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani na Nje ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kila sababu ya kuendeleza michezo mashuleni ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Ni vyema ikumbukwe kuwa, hapo nyuma kulikuwa na mashindano ya mpira wa miguu kwa shule za sekondari Tanzania na Zambia (UMISETA). Mashindano hayo yalikoma mwaka 1977; hivyo, ni vyema mashindano hayo yakaboreshwa kwenye Ukanda huu wa Afrika Mashariki. Michezo hiyo itawezesha kupatikana timu bora za Taifa za michezo yote ambayo tunashiriki Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiridhike na nafasi ya pili ya mashindano ya wanavyuo, ni vyema tukaboresha elimu yetu ili tufanye vizuri zaidi.

MHE.HAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa dira kuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kukuza kipato, kuinua maisha ya Wananchi wa Afrika Mashariki, kukuza uchumi na kujenga ushindani wa kanda katika ngazi ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma hii, Nchi Wanachama zinanufaika kutokana na mahusiano mazuri ya kibiashara na uwekezaji. Aidha, Nchi Wanachama zinanufaika na programu mbalimbali ikiwa ni pamoja na programu za kuendeleza mitandao ya barabara, reli, bandari, umeme, elimu, afya, usalama na utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na dira hiyo, tunatarajia Tanzania inauza bidhaa kwa wingi katika Nchi za Afrika Mashariki, ikiwa ni pamoja na bidhaa za chumvi, umeme na vifaa vya umeme, mafuta ya kupikia, vifaa vya *plastic,* kahawa iliyosindikwa na nondo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na ushindani ndani ya Soko la Afrika Mashariki; je, Serikali imeweka mikakati gani madhubuti na ya muda mrefu, ili kuhakikisha kuwa bidhaa zetu zinakuwa zenye ubora zaidi ili kukidhi vigezo vya kimataifa na ziweze kukabiliana na ushindani huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalizo ni kuwa, Serikali ina maneno mengi mazuri sana ya matumaini, lakini kiutendaji mara nyingi siyo watendaji tofauti na wenzetu katika Nchi Wanachama, wao wako kikazi zaidi na wana maandalizi barabara; kwa hiyo, Serikali ifanye kazi ya ziada juu ya hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, inabidi kuwepo na tathmini kwa kila mwaka ili tuweze kujitathmini sisi wenyewe kuwa tumefikia wapi katika ushiriki wetu na bidhaa zetu za hapa nchini zimeuzika kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto za Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, Mheshimiwa Waziri Sitta alisema, Serikali ipo katika mchakato wa kujenga masoko kwenye mipaka inayopakana na nchi

hizo ili Wananchi waweze kuuza bidhaa zao katika utaratibu unaoleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Pemba ni moja ya sehemu iliyopakana na Shimoni Kenya, basi ni vyema Serikali kati ya masoko hayo ambayo inatarajia kujenga mipakani, soko moja likajengwa Pemba hasa kule Kaskazini ili Wananchi wa Pemba wasiendelee kusumbuliwa na kudhulumiwa wanapopeleka bidhaa zao Nchini Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Serikali itafanikisha ujenzi wa soko moja katika Kisiwa cha Pemba, basi hata malalamiko ya Wananchi wa Pemba yatakuwa yameisha kwa jinsi wanavyoonewa na kunyanyaswa na wenzetu wa Kenya, kwani wenzetu hawa muda wote wanajiona wao wako juu zaidi kuliko wengine na wakati mwingine hujifananisha na kujiona miungu watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhusu elimu ya biashara, ni lazima Serikali kupitia Wizara hii ya Afrika Mashariki, ifikishe elimu kwa wafanyabiashara wa Kisiwa cha Pemba hasa kule Kaskazini ili Wananchi hao wajue haki zao mara wanapopeleka bidhaa zao Nchini Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira ni vyema Serikali ikaona umuhimu wa kuajiri watendaji wa Wizara hii ya Afrika Mashariki katika Kisiwa cha Pemba ili Wananchi wa Pemba mara wanapokuwa na shida au malalamiko yanayohusu Afrika Mashariki, iwe rahisi kupata maelekezo au msaada wa haraka kwa Wizara yao ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamwomba Mheshimiwa Waziri wakati akifanya majumuisho, aniambie ni lini Wizara itaajiri watendaji Kisiwa cha Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nimwombe Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri, wasiache kufanya ziara katika Bandari ya Shimoni Kenya, kwani Mheshimiwa Naibu Waziri, alipofanya ziara katika Bandari hiyo, Wananchi wa Pemba ambao ndiyo wadau wakubwa

wa Bandari hiyo, faida ya kwenda Naibu Waziri kwa kipindi kile waliiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nilizonazo tayari hali ya zamani katika bandari hiyo inaanza kujirudia; hivyo, ni vyema Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri, wawe wanapanga ratiba ya kupitia kwenye bandari hiyo ili kuwasaidia wafanyabiashara wadogowadogo wanaotoka katika Kisiwa cha Pemba, kwani kufika kwao kwenye Bandari hiyo faraja huwa inapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru. Ahsante sana.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba, Ushirikiano wa Afrika Mashariki wa awamu ya kwanza uliovunjika mwaka 1977, sababu mojawapo iliyopelekea kuvunjika kwa Ushirikiano huo kama ilivyoelezewa katika dibaji ya Kitabu cha *MEAC Communication Strategy;* ni ushiriki mdogo wa Wananchi wa nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali za Nchi za Ushirikiano wa Afrika Mashariki, zinafanya juhudi zipi ili Wananchi wauelewe vizuri ushirikiano uliopo sasa wa Afrika Mashariki na hivyo kupunguza athari zinazoweza kujitokeza na hivyo kuvunjika tena kwa Ushirikiano uliopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, bado haieleweki kwa Watanzania walio wengi. Wananchi wapatiwe elimu ya kutosha ili maandalizi yatakapokamilika, Wananchi na hasa Watanzania, wasiachwe nyuma katika kuelewa ni nini kinachoendelea kuhusiana na Soko la Pamoja na Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Sitta inaainisha maandalizi kadhaa yanayoendelea katika Wizara yake ya Ushirikiano wa Nchi za Afrika Mashariki; kwa mfano, maandalizi ya Sera ya Mifugo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Pia uratibu unaoendelea wa uanzishwaji

wa Umoja wa Fedha wa Jumuiya na Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo hayo yote ni Watanzania wachache wana uelewa wa nini kinachoandaliwa na kufanyika katika Wizara hii. Wananchi wapatiwe taarifa mara kwa mara kupitia Vyombo vya Habari ili wasiwe gizani kwa yale yote yanayowahusu, yanayoendelea katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 18, inaelezea mafanikio yaliyopatikana katika uwekezaji, idadi na thamani ya miradi inayowekezwa hapa nchini na wawekezaji kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni katika maeneo ya ujenzi, utalii, usafirishaji na usindikaji viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, hali ya uwekezaji ikoje katika Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki kutoka Tanzania? Nini mwamko wa Watanzania kuwekeza katika Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki ukilinganisha na Kiambatanisho Namba 5 na Namba 6, kinachoonesha Nchi nyingine za Afrika Mashariki zinazowekeza Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Wizara kwa kazi wanayoendelea kufanya. Hata hivyo, bado kuna changamoto nyingi kuhusu Ushirikiano huu wa Afrika Mashariki, ikiwemo suala la Elimu kwa Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wengi bado hawaelewi ushirikiano huu wa Afrika Mashariki upo katika nyanja zipi na bado hawajui fursa zilizopo kutokana na ushirikiano huo. Uelewa na juu ya jinsi fursa hizo zitakavyosaidia ukuaji wa uchumi wa mtu kwa mtu na Taifa kwa ujumla bado hazieleweki kwa ufasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara hii kutoa elimu ya kutosha kwa Watanzania kuzielewa fursa zilizopo

kutokana na ushirikiano huu wa Afrika Mashariki ili tuweze kwa pamoja kufaidika na ushirikiano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano huu kwa kuwa na sarafu moja bado ni changamoto ambayo Wizara na Serikali kwa pamoja mtahitajika kujipanga, kwa kuwa suala hili ni gumu hasa tukiangalia matumizi na thamani ya fedha ya nchi yetu na nchi zingine. Hata hivyo, Serikali bado haijajipanga vyema kwa suala hili kwa kuwa pia Sera za Fedha kwa nchi hizo zinapishana. Je, ni kwa kiasi gani Wizara na Serikali imejipanga kwa suala hili la kuwa na sarafu moja ya Afrika Mashariki? Je, changamoto ya Sera za Fedha kwa nchi hizo itatatuliwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kamisheni ya Kiswahili Makao yake Makuu yapo Tanzania (Zanzibar), nashauri tutumie fursa hii kukuza Lugha hii hasa kwa lengo kuu la kuimarisha Umoja wa Jumuiya kama tulivyofanikiwa Tanzania kuunganisha zaidi ya makabila 120 kwa kutumia Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Utafiti kianzishwe au kiimarishwe kwa ajili ya kutafiti kwa mapana mbinu za wenzetu katika Jumuiya ambazo hazina tija kwa upande wetu hasa intelijensia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wa Afrika Mashariki wapewe Ofisi za kuwawezesha kuhudumia Watanzania kwa urahisi na pia kupata mawazo kutoka kwa Watanzania kuhusu namna bora zaidi ya kushiriki katika Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msisitizo wa kufanyia Vikao vya Bunge la Afrika Mashariki Arusha uzingatiwe kwa masilahi mapana ya Wanajumuiya. Na kama mzunguko unaendelea ndani ya Nchi Wanachama, basi uwepo uwezekano kwa upande wa Tanzania wafanyie Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afrika Mashariki ifanye kazi kwa ukaribu na Wizara ya Ujenzi au Uchukuzi kuimarisha miundombinu ya Bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Zanzibar na Reli zote zinazounganisha Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kiswahili ni kati ya Lugha zinazotumika katika Bunge la Afrika, pia kitumike katika Bunge la Afrika Mashariki.

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kuhitimisha hoja yake, aliambie Bunge lako Tukufu ni Miradi mingapi ambayo imesaidiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Development Bank*) kwa Tanzania; kati ya hiyo, Zanzibar imefadhiliwa miradi mingapi. Maelezo ya Mheshimiwa Waziri, yatasaidia kuondoa hofu kwa upande wa Zanzibar kwamba, Zanzibar ni msindikizaji tu na hainufaiki chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Mheshimiwa Waziri, aliambie Bunge lako Tukufu namna ambayo Tanzania imenufaika katika fursa za Masoko ya Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki. Ni Watanzania wangapi wameajiriwa katika Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki kwani kwa sasa tunaona Wakenya na Waganda wamefaidika na ajira hapa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba, makampuni mengi ya Kenya yamefanya biashara hapa Tanzania. Je, ni makampuni mangapi yanayomilikiwa na wafanyabiashara wa Kitanzania yanafanya biashara huko katika Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Samwel Sitta, Naibu wake na watendaji wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kulinda na kusimamia maslahi ya nchi yetu kwenye Jumuiya na mchakato unavyoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo kubwa moja ninaloomba mlifanyie kazi nalo linahusu deni la pango la Jumuiya ya Afrika Mashriki kwa Shirika la *AICC.* Shirika linasita kwenda Mahakamani kwa sababu za kidiplomasia, lakini sasa litalazimika kwenda huko baada ya Wanasheria wao kushindwa kujibu hoja za Wanasheria wa *AICC.* Ili tusifike kubaya, tunaomba jambo hili lishughulikiwe kulinda mahusiano yetu ya kidiplomasia.

Nawapongeza sana, washike msimamo huo huo kwenye suala la ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imeamua kujenga masoko mawili ya kimataifa katika Mji wa Himo; na kwa kuwa masoko haya ya mbogamboga, ndizi na nafaka, yatavutia Wananchi wa Kenya, Uganda, Sudani ya Kusini na Somalia; na kwa kuwa Mji wa Himo utakuwa kituo kikubwa kwa watalii wanaopanda Mlima Kilimanjaro; naomba kujua sera ya Wizara ya Ushirikiano kuhusu:-

(i) Kupanua Barabara ya Arusha – Holili hasa maeneo ya Vunjo inakopitia barabara hiyo. Barabara hii ni muhimu sana, kwani inatumiwa na watalii wengi wanaotaka kupanda Mlima Kilimanjaro kupitia Lango la Himo.

(ii) Kutengeneza upya Reli ya Kahe – Taveta ambayo sasa imechakaa. Reli hii ni muhimu hasa wakati huu, baada ya uamuzi wa Serikali wa kujenga Masoko ya Kimataifa Himo ambayo yatawaleta wafanyabiashara wengi wanaotoka Kenya, Uganda, Sudani ya Kusini na Somalia.

(iii) Kwa kuwa ipo mizani moja tu ya kupima uzito wa magari pale njiapanda Himo; na kwa kuwa mizani hiyo husababisha foleni kubwa ya magari; Wizara ya Afrika ya Mashariki ina mpango gani wa kuweka mizani ya pili?

(iv) Ikiwa Jumuiya ya Afrika Mashariki itajenga barabara kupitia Mji wa Himo na tayari nyumba nyingi pale zimewekewa alama ya X; nani atagharimia fidia ya nyumba hizo ni Serikali ya Tanzania au Jumuiya ya Afrika Mashariki?

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu kwa sababu ya Ushirikiano wa Nchi za Afrika Mashariki, Tanzania ikiwa nchi mojawapo. Ili nchi hii uchumi uendelee, ni vyema Wizara (Serikali) hii, iwe makini katika programu zote zinazoainishwa katika Ushirikiano huu; mfano, kuwa makini na Miswada inayowasilishwa katika Bunge la Afrika Mashariki, Miradi inayoainishwa na Sekretarieti inayohusu ushirikiano katika Nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo changamoto ya ajira zinazotoka katika nchi nyingine. Soko la ajira linaelekea limefunguliwa, lakini bado kuna vikwazo, nchi hizi bado zinahitaji vibali vya kufanya kazi hasa katika maeneo machache mfano *Hotel Managers*. Wananchi wa Kenya mfano, wanatumia Lugha ya Kiingereza na Kiswahili, usaili mwingi katika nchi zetu za Afrika Mashariki unafanyika kwa Kiingereza na mahali pengine Rwanda na Burundi Kifaransa. Watanzania wana tatizo la kuongea Lugha ya Kiingereza na Kifaransa, jambo ambalo linawanyima fursa nyingi za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado maeneo mengi Watanzania hawana uelewa au kuwepo kwa Soko la Afrika Mashariki, hata wale waishio majirani na nchi kama Kenya, Uganda, Burundi na kadhalika. Elimu zaidi inatakiwa ili kuelimisha Watanzania katika fursa zilizopo katika Soko la Afrika la Mashariki. Fursa za wanawake wajasiriamali zipo nyingi, ila elimu inatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi iliyopangwa ya maendeleo kutekelezwa katika nchi za Afrika Mashariki

(Tanzania), inatakiwa isimamiwe kwa makini na uadilifu ili ilete tija kwa Taifa. Mfano, ni Ujenzi wa Barabara, *Airports,* Umeme, Reli na Bandari na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kujenga Vituo vya *One Stop Post* katika Miji ya Namanga, Sirari, Holili na kadhalika. Vituo hivi vitasaidia sana Watanzania au Watalii wanaotembelea nchi zetu au kwenda kuuza bidhaa katika nchi nyingine za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa masoko ya mipakani nayo ni muhimu; mfano, Soko la Lokolova la Makuyuni Mkoani Kilimanjaro. Masoko haya yatazuia uuzaji wa mali katika njia za kificho (*black market*), hususan mazao ya nafaka, sukari na kadhalika. Wanunuzi kutoka nje ya Tanzania watakuja Tanzania, watanunua bidhaa na italeta tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Sera ya Mtangamano wa Afrika Mashariki inatakiwa itatuliwe. Wizara hii na Wizara ya Mambo ya Nje, zikutane, Sera itengenezwe iletwe Bungeni. Bila Sera yetu wenyewe, utekelezaji wa yale tunayotaka yatekelezwe itakuwa vigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, wanapaswa kutoka kwenda katika Mikoa ya Tanzania, waombe wapangiwe mikutano na Wakuu wa Mikoa, ili waongee na hadhara za mikoani, kusaidia kutoa elimu kuhusu soko la fursa za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ya sarafu ya pamoja haina tija kwa Taifa hili kwa wakati huu. Tumeshuhudia Muungano wa Ulaya Uholanzi ikitamani kutumia *guilder,* Denmark na Uingereza kutumia sarafu yao, badala ya sarafu ya pamoja ya Umoja wa Ulaya, yaani *Euro.* Naishauri Serikali tusiharakishe kwenda kwenye sarafu ya pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kuhamahama kwa Vikao Bunge la Afrika Mashariki kunaharibu dhana ya Makao Makuu ya Umoja wa Afrika Mashariki. Naelewa kukaa Bunge

hilo Mjini Arusha, kunaongeza pato la Wakazi wa Arusha *(hotel, guest houses, family resorts, restaurants, banks, bureau de changes* na kadhalika). Kuiweka dhana ya Makao Makuu ya Afrika Mashariki vyema, Serikali ya Tanzania iweke msimamo katika hili, Bunge likae Arusha na si vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, kwa juhudi kubwa anayoifanya ili kuhakikisha kwamba, Shirikisho hili la Afrika Mashariki linafanikiwa, akishirikiana na Naibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Watanzania wana wasiwasi mkubwa juu ya uundwaji wa Shirikisho la Siasa pamoja na kuwa na sarafu ya pamoja. Naiomba Serikali kuchukua tahadhari kubwa katika kufikia suala la kuwa na sarafu moja. Baada ya soko la pamoja, kinachofuata ni kuwa na sarafu moja; hivyo, ni vyema kabla kufikia lengo hili, Wananchi wapewe elimu ya kutosha na pia washirikishwe kutoa maoni yao, kwani hofu zaidi ni kwamba uchumi wa wenzetu unakua kwa kasi kila mwaka ukilinganisha na sisi ambao uchumi wetu unakua polepole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uundwaji wa siasa ni bora jambo hili lipewe muda mrefu, kwani Wananchi wengi jambo hili wana mashaka nalo. Hivyo, pamoja na Serikali kutia sahihi lakini ni bora kwanza Watanzania wapewe taaluma ya kutosha ili waelewe wanakoelekea na pia waweze kushiriki kikamilifu wakati ukifika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na soko la pamoja kuanza; je, Tanzania tunafanya vizuri kwa kuwa bado tuna tatizo la miundombinu mibovu na pia hatuna viwanda vya kutosha kama vile nchi za wenzetu ambao tunaungana nao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nipatiwe taarifa sahihi; je, tunafanya vizuri katika ushuru wa forodha isiwe sisi ni watu wa kufaidisha wengine tu?

MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 86 ya Hotuba ya Wizara ya Afrika Mashariki inaonesha kuwa Mto Umba umeanzia Jimbo la Mlalo na sehemu kubwa unategemewa na Watu wa Mlalo. Je, upo uwezekano wa kunipatia nakala ya Programu iliyopitishwa kuhusu ikolojia ya Mto Umba?

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa maana ya michango ya jumla tumemaliza. Sasa nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri ili aanze kuja kujibu hoja na baadaye tutamwita Mtoa hoja Waziri Mwenyewe na yeye atakuja kuhitimisha hoja hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa unatoka Zanzibar, basi yakhe yakhe uziseme sana kwenye hotuba yako hapa.

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sote hapa kukaa salama salimini na kujadili mambo haya muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nawashukuru na kuwapongeza wananchi na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki wote kwa ujumla Watanzania na wasio Watanzania kwa ushirikiano wao mkubwa wanaoutoa kwangu mimi pamoja na Mheshimiwa Waziri wangu ili kufanikisha majukumu yetu yawe salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingi sana zimechangiwa, lakini na mimi nafurahi sana kwa kunipa nafasi angalau niweze kuchangia machache na niweze kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo zitakuwa na faida kwa Watanzania kwa ujumla.

Nitajitahidi kwa ukomo wa uwezo wangu kujibu hoja hizo na pale nitakaposhindwa, basi Mheshimiwa Waziri naye atakuja kuendelea na kama nyingine tutakuta hatujazijibu,

siyo kwa sababu tumedharau lakini ni kupitiwa kibinadamu na tutazijibu kimaandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya kuwa Wizara ina mpango gani wa kuendeleza Bandari ya Mfumbuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ruhusa kwanza nianze Pemba. Kwa kauli fupi tu ni kwamba Bandari ya Mfumbuu haikuwasilishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa iwemo katika mchakato wa kutafuta ufadhili na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kwa hiyo, tutashindwa kuelezea lolote kuhusu bandari hii. Lakini kwa ukaribu wa bandari hii na umuhimu wake kama ilivyo ile ya Wete, naamini kwamba kama jambo hili Mheshimiwa Mbunge atalipa kipaumbele kwenye Serikali ya Mapinduzi, basi Tume ya Mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar watatuletea sisi na tupo tayari kulishughulikia ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kulikuwa na hoja nyingine ya kwamba uwanja wa ndege wa Pemba umeshughulikiwa vipi na Jumuiya ya Afrika Mashariki? Uwanja wa ndege wa Pemba ni miongoni mwa vipaumbele ambavyo vimeshatiwa saini na Waheshimiwa Wakuu wa Nchi katika mipango ya miundombinu kuhusiana na mambo ya anga ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Jumuiya ya Afrika Mashariki imepokea na nina furaha kusema kwamba tumeshatafuta mpaka mfadhili, yaani *African Development Bank* ili waweze kusaidia ukarabati wa uwanja wa ndege wa Pemba. Lakini kilichotokea na baada ya ufuatiliaji wa kina, kuanzia mwaka 2012 mwezi Aprili na Novemba pia tulikwenda Pemba; Januari katika Mkutano wa kikao cha pamoja cha *SMZ* na *SMT* tulilijadili jambo hilo na mwezi wa Aprili mimi nilikwenda pamoja na timu yangu kutaka kujua kwa kina kwa nini uwanja wa ndege ule haujajengwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi tu kwa sababu muda wenyewe ni mfupi, taarifa nilizozipata kutoka kwa mamlaka yanayoshughulikia uwanja wa ndege ule kwa maana ya Wakurugenzi na Waziri ni kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshaweka kiasi cha fedha za Kitanzania Shilingi milioni 500 kwa ajili ya kufanya *feasibility study* ya ile sehemu. Hiki ndiyo kitu ambacho kilikuwa kinasubiriwa kwa sababu ikishafanyika *feasibility study,* mkataba uliokuwepo baina ya Afrika Mashariki na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kwamba ikishafanyika *feasibility study,* basi yatakayofuatia yote yatashughulikiwa na *African Development Bank*. Hii ndiyo taarifa ambayo tunayo mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lililobaki kwa hapa ni kwamba, Wizara yetu ya Afrika Mashariki inasubiri hiyo *feasibility study* na ikishamalizika tu tuliambiwa anatafutwa *consultant* na baada ya kupatikana *consultant* utafanyika utaratibu wa kuanza kufanya hiyo *study* katika miezi 18 hivi kwa kauli niliyopata kutoka kwa Naibu Waziri, amesema inaweza ikakamilika na italetwa kwetu sisi, tutaiendeleza katika mchakato unaoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kulikuwa na suala la Bandari ya Micheweni. Lilikuja suala hilo na likaulizwa tena kimaandishi. Lakini nirejee tena kusema kwamba kuhusu Bandari ya Micheweni hakuna taarifa yoyote ambayo kama ilivyokuwa ya Mfumbuu, basi na Micheweni ndiyo hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika ziara tuliyoifanya pale Micheweni na tukakutana na mamlaka zilizopo pale, zimesema kwamba Micheweni haipo hata katika *concept paper,* yaani katika Wizara ya Miundombinu ya Zanzibar hawakuitia kabisa na wala mawazo ya kupeleka bandari pale. Lakini kilichotokea ni kwamba wananchi wenyewe na hilo hata mimi mwenyewe nalikubali na hata tulipofanya ziara tulikubali na *DC* alikubali kwamba wanahitaji *jet,* yaani egesho tu. Tumeshamwambia Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na mwakilishi wake kupeleka pendekezo hili katika *SMZ* ili pale pawekwe egesho na wananchi baada ya

kuonana nao sisi wenyewe ana kwa ana wamesema inatosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda Zanzibar, pana Bandari ya Maruhubi. Katika maelewano ambayo tumekutana katika harakati za makusudi tulizokwenda kuzifanya pale, tumeambiwa kwamba Bandari ya Maruhubi ilikuwa ina *feasibility study* siyo chini ya tatu. Lakini nitoe angalizo kwamba Wizara yetu ya Afrika Mashariki ilikuwa inasubiri ile *feasibility study* ifanyiwe *project unpacking* yaani kwa Kiswahili imeng'enyuliwe, ipate *project unpacking* ili kile kipande kiletwe katika Afrika Mashariki ambayo tupo tayari na ilishatolewa kipaumbele kupitia Marais wetu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, kumeng'enyua nacho ni Kiswahili eh! *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Kwa hiyo, tunasubiri hilo na tulipofika sisi tulitoa tu taarifa kwamba ikiwa *project* ile ambayo ilifanywa na *GIPS* au ile ambayo ilifanywa na China kwa Dola milioni 400 au ile ya Dola milioni 700, yoyote ile kati ya hizo tuletewe ili tuweze kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waride na Mheshimiwa Mohamed Mnyaa waliulizia kuhusu Ofisi kwani hawakuwa na uhakika kama ipo. Ni kweli Ofisi ya Mwanzo ilikuwa Ikulu. Iliulizwa katika Bunge hili kwamba hii Ofisi kuwepo Ikulu, kweli wafanyabiashara na watu wengine waliokuwa namna gani vipi watakwenda Ikulu?

Kwa hiyo, nina furaha kuelezea kwamba Ofisi ile imeshafunguliwa, ipo Kinazini kwenye jumba la *ZSTC*, Ofisa yupo, vitendea kazi vipo na iliyobaki tu sasa hivi ni kuboresha tu na kuifanya bajeti yake iwe mahususi, basi. Lakini ipo na ninatoa wito kwa Wazanzibar waliopo kule, wanaweza kumtumia huyu Ofisa mahiri kabisa ili kuweza kupata maelekezo juu ya namna gani wanaweza kutumia fursa ya kufaidika na mtangamano huu wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waride alipendekeza tu na wengi walipendekeza, kwanza alipongeza na ninamshukuru sana kwa kutupongeza kwani ni moja ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kuwepo kwa jengo lile pale Arusha. Tayari sisi tumeshalikubali kwa sababu Baraza la Mawaziri limeshaamua kwamba 50% ya vikao vya Mawaziri vikutane Arusha na hilo limeshapita wala halina mjadala. Sasa Wabunge wetu wa Afrika Mashariki wapo, na wao wana *commission* yao katika Bunge, watalipendekeza hili kwa maslahi ya Tanzania na sisi tutasaidia katika kushajihisha ili na vikao vya Bunge la Afrika Mashariki navyo angalau 50% vikutane Arusha na vingine viwe vinazunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lilikuja la kuulizwa kwamba hivi Zanzibar inashirikishwa vipi katika maamuzi ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki? Ikiwa jambo halipo kimaandishi, kisheria au kikanuni, basi kuna desturi na miongozo na mambo mengine hutumika. Utamadumi ambao umejitokeza sasa hivi na ndiyo ambao tunautumia na tunaona unafaa sana, ni kwamba Zanzibar hushirikishwa katika vikao vyote vya Jumuiya ya Afrika Mashariki, tangu vikao ambavyo ni vya Watendaji wadogo, kuna vya *Senior Official,* kuna vya Makatibu Wakuu, kuna vya Mabaraza ya Kisekta na Baraza la Mawaziri.

Bahati inakuwa nzuri wakati mwingine, anayeshika bendera katika majadiliano anakuwa ni Mzanzibari. Hilo limejitokeza siyo mara moja na wala siyo mara mbili, na hasa katika majadiliano ya *SADC*, *EAC* na *COMESA*, Mheshimiwa Mazrui ambaye anatoka katika Chama cha *CUF,* yeye ndio mashuhuri kwa kukiongoza kikao kile. Kwa hiyo, ni wazi kwamba Zanzibar tunashirikishwa. Hii hitilafu ndogo tu ya ya kuwa labda katika mambo ambayo siyo ya muungano na ya muungano, lakini katika masuala yote kabisa wanashirikishwa na hakuna matatizo yoyote yanayojitokeza mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la juu ya sera. Kwa ufupi tu, katika hotuba yetu ya mwaka 2012

tulizungumzia kwamba kutakuwa na sera inayohusiana na Mtangamano wa Afrika Mashariki. Nakubaliana sana na Mheshimiwa Masauni na Waheshimiwa Wengine waliozungumza kwamba bila ya sera maana yake ni kwamba hatutakuwa na mwelekezo, lakini kwa hivi sasa siyo kwamba hatuna mwelekeo, tunatumia sera ya mambo ya nchi za nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina furaha kusema kwamba rasimu ya sera hii imeshakamilika na hivi sasa tumeshaikabidhi kwa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ambayo ndiyo *instrument* ya mambo hayo na kwa kushirikiana pamoja kupitia nyenzo za Serikali, basi hii sera kwa muda mfupi sana tunategemea itakuwa tayari na tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuonyesha undani wa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine ya kuhusiana na Wabunge wa Afrika Mashariki kwamba Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao ni Wabunge wetu kule na Jimbo lao ndiyo hili, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwamba tunawashirikishaje? Je, tunawahamasisha vipi na tunawapa taaluma vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna furaha tu kusema kwamba Wizara yetu siyo katika Bunge hili, lakini hata Bunge lililopita, tuligundua kwamba kuna ukosefu fulani wa mawasiliano na hawa Wabunge wetu. Tuna furaha kusema kwamba Wizara yetu imeshatengeneza utaratibu wa kukutana nao hao Wabunge kila kabla ya kukutana katika Bunge lolote lile ambalo litakutana, nchi yoyote ile.

Aidha, tunakutana hapa Tanzania au ikishindikana, tunakutana katika nchi ambayo wanakutana. Lakini kama hili halitoshi, kuna wakati mwingine wao huwa na mahitaji ya kutaka kutuona sisi kutokana na hoja ambazo wanazo, sisi tunakuwa tayari pamoja na wataalamu wetu na wataalamu wengine kutoka nje kuwaweka na kuwapa taaluma namna gani ya kuweza kuendelea na majadiliano katika Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nilikuwa napenda kutoa angalizo muhimu sana kwamba kukutana na Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki na kuwapa taaluma, siyo kwamba tunawashawishi au tunafanya *lobbing* kwamba *Excutive Arm* ya Bunge la Afrika Mashariki iwe ndiyo mihimili yao, hapana! Ni taaluma za kisera na ni taaluma za kitaalamu ambazo wao wanataka kujua na kupata ufahamu wa masuala tofauti ya kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili ambalo limezungumzwa kuhusu kuwawezesha Watanzania na Watanzania wako vipi katika ajira za nchi jirani za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nakubaliana na kusema kwamba kwa kweli taarifa za nchi jirani au taarifa za Watanzania kwenye nchi jirani ziko finyu kidogo kwa sisi kuyajua. Lakini kama utakwenda, basi nadhani wewe mwenyewe utaweza kufurahia na kuweza kuona kwamba ni namna gani uthubutu wa Watanzania umejitokeza katika nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulitokea jambo dogo tu, ziara ndogo ya wanamichezo wa *Bunge Sports Club,* nami nilibahatika kuwa nao Kenya, tuliwaona Watanzania jinsi walivyokuwa wanafanya kazi. Wapo wengi sana, yaani wapo Watanzania tuliowakuta katika sehemu moja tu ambao ni wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati karibu 500.

Kwa hiyo, siyo kusema kwamba hawaendi, bali wanakwenda, lakini sema taarifa kuja kutoka kwetu sisi huwa kidogo ni finyu, na hili nalikubali. Siyo Kenya tu, bali Uganda wapo, Burundi wapo wengi tu, wanatuuzia mpaka mchele na vitu vingine vingi sana na tunakutana nao. Kwa hiyo, hili nilikuwa napenda kusema kwamba ufinyu wa taarifa kweli upo na tutazidi kutoa taarifa kwa kushirikiana na Balozi zetu ili kuweza kujua ni namna gani wananchi wana-*enjoy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiacha jambo hilo pia, kwa taarifa tu hivi sasa, Benki ya *CRDB* imeshafunguliwa Burundi na inafanya kazi *full operation.* Hata sisi wenyewe tukienda kule huwa tunaitumia Benki yetu ile. Rwanda tumeshakutana na Azam, anafanya kazi nzuri sana tu,

Bakhresa. Kwa hiyo, vilevile palepale Rwanda kwa yale macho ya mwanzo mwanzo tumekutana na watoto wa Kitanzania, maana siwezi kuwaita watu wazima; ni vijana shababi wame-*apply tender pale* ya kupaka rangi uwanja wa ndege wa Rwanda. Ni fahari yetu sisi hiyo!

Kwa hivyo, siyo kwamba hakuna, lakini narejea tena kusema kwamba, kidogo taarifa zimekuwa finyu kutufikia na Wizara itafanya kila liwezekanalo kuzipata zile taarifa ili na Watanzania tuwe tunasema wapo wanaothubutu; kwenye redio ya Kiswahili Rwanda, Walimu na kadhalika. Mmoja kati ya Mawaziri kule Rwanda ana asili ya Kitanzania, nilimkuta akaniambia mimi *passport* yangu sijarejesha. Ni Profesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na wazo la kuwepo kitengo cha utafiti katika Wizara yetu. Hili jambo siyo baya, tunalikubali. Lakini kulikuwa na hoja ndogo tu ambayo ilibidi lazima tuielezee ya kusema kwamba, kitengo chetu tunategemea sana kuwa na uratibu wa utafiti kwa kushirikiana na sekta nyingine. Mheshimiwa John Mnyika amelielezea vizuri sana hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwaelezea Waheshimiwa Wabunge kwamba hili jambo lipo Wizarani kwetu na tunataka tulishajihishe kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi na Ajira, ili tushirikiane na Wizara nyingine za kisekta kuweza kujua masuala tofauti. Ni wazi kwamba, hata kama tutakuwa na kitengo cha utafiti cha watu watano, sita, saba, lakini siyo rahisi kumkuta mtu pale ambaye huyo ataingia katika viwanda, huyo huyo forodha, huyo huyo mambo ya kijeshi na huyo huyo katika elimu. Hivyo, inabidi kutafuta uratibu pale kwa kushirikiana na vitengo vingine katika Wizara za kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la ushiriki wa *SADC*. Mheshimiwa Masauni alisema kwamba, ni lazima Serikali ilieleze Bunge manufaa ambayo Tanzania inayapata katika mambo ya mtangamano. Manufaa yako mengi sana. Kuna manufaa ya kiuchumi. Kama tulivyosema kwamba mauzo ya ndani ya Tanzania yameongezeka karibu mara

tatu au nne, ukilinganisha na mauzo ya zamani ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hili ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunapata uwekezaji ndani ya nchi. Mheshimiwa Habib Juma Mnyaa, kidogo alihoji kwamba wenzetu wanakuja, sisi tutapona vipi? Nimeshaelezea sisi nje tunaingia vipi. Lakini na wao kuja siyo jambo baya. Kuja kwao wao sisi kupata taaluma, tunauza, na tunapata mambo mengi sana humu ndani ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, pamoja na sisi kwamba tunakwenda, lakini na wao kuja vilevile wakifuata taratibu zinazohusika, siyo jambo baya hata kidogo. Tunawakubali hata waishi kati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa sana ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi hawakuliona, kuna mambo kama ya kiuchumi na kijamii tunashirikiana sasa hivi. Kwa mfano, kuna kitu kinaitwa *bulk procurement* ya *drugs*, yaani manunuzi ya dawa katika kima kikubwa. Ukinunua dawa kwa kima kikubwa, basi hata fedha unayotoa inakuwa ni ndogo na inanufaisha watu wengi. Haya ni miongoni mwa manufaa ambayo tunayapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, masuala ya ujirani mwema, ulinzi na usalama, katika kutokomeza maangamizi ya silaha ndogo ndogo, yote haya tunashirikiana. Kwa hiyo, faida ipo kubwa sana, siyo zile tunazoweza kuziona kwa macho tu, lakini hata zile za kinadharia ambazo wanaita *soft copy advantages.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi ninaloweza kulizungumza kuhusiana na faida ambayo tunaweza kuipata ni kwamba, sasa hivi Tanzania inaingia kwenye majadiliano ya kiuchumi na *EPA*. Vilevile imetoka nafasi sasa tunaingia katika majadiliano ya kiuchumi na *COMESA, SADC* na *EAC*. Maana tumefungua dirisha lingine la kuweza kwenda kujadiliana kiuchumi. Katika mambo mengi kama haya tunaita *bilateral negotiations* zinaweza kujitokeza. Kwa hiyo, faida za kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ni nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo limejitokeza limeulizwa kuhusiana na kwamba, kuna utaratibu gani wa kuweza kuoanisha mifumo ya elimu ndani ya Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni lazima nikubali na nikiri kwamba mtangamano wa Afrika Mashariki hivi sasa pamoja na kwamba upo kwa zaidi ya miaka 10, haya ni mambo ambayo yanajitokeza na kuendelea hatua kwa hatua. Sasa hivi siyo rahisi kusema tuagize mitihani kutoka Uganda na Uganda waagize kutoka kwetu, lakini kumeshafanyika utaratibu hivi sasa na ni mpango wa utekelezaji wa kuimarisha mifumo ya elimu na mitaala. Kamati imeshatengenezwa, Baraza la Mawaziri lilipendekeza hilo, imeshatengenezwa.

Vilevile Baraza la Mawaziri limeidhinisha maandalizi na mikakati inayolenga kuhuisha au kuainisha mifumo na mitaala katika elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Ualimu, Elimu yenye Mahitaji Maalum, Elimu ya Watu Wazima, Elimu ya Ufundi na kadhalika. Tayari hili jambo limeshafikiriwa na hivi sasa watu wako kazini wanatazama ni namna gani tunaweza tukaainisha mfumo wa elimu katika *level* ya Afrika Mashariki na ni namna gani itahuishwa na kukubalika katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la elimu kidogo liko nyuma, lakini kwa upande wa afya wako mbali sana. Yaani sasa hivi kuna kitu kinaitwa *reciprocal recognition.* Yaani daktari anayesomea Chuo Kikuu cha Moi, Kenya ana haki ya kuja kufanya kazi hapa kutokana tu na kwamba taaluma na *syllabus* zao wameshaziweka pamoja. Haikuishia hapo tu, hata vile vyuo vyao sasa hivi vinafanyiwa *inspection* ya pamoja katika Afrika Mashariki. Ukifeli *IMTU* basi ndiyo umefeli *Nairobi University.* Kwa hiyo, hii ni hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Nyerere hili ulilipendekeza na hivi ndivyo hali ilivyo, tunakwenda huko. Mambo ni hatua kwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni lile ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Augustino Mrema, aliulizia kuhusu upanuzi wa barabara ya Arusha – Holili ukoje? Katika bajeti yetu iliyopita tulizungumzia hili kwamba *feasibility study* ilikuwa inafanywa. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, *feasibility study* imeshafanywa. Sasa hivi kuna *detailed designs* ambazo watu wanata kuzifanya, kuna *consultants* wanachukuliwa kazini na baada ya hapo upanuzi na ujenzi utaendelea na Wizara yetu inalisimamia suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Mrema alikuwa na suala moja zuri la kuchomekea kidogo juu ya ile reli inayotoka Kahe kwenda Taveta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wetu na katika mipango ya miundombinu ya reli ambayo Waheshimiwa Marais wameishaipitisha, hiyo reli imo. Isipokuwa tu ni kwamba katika mipango, kwa sababu ilivyo baada ya kupitishwa, ile mipango inakuja inahuishwa inakuwa *adopted* na mipango ya nchi. Kwa hiyo, kwa upande wa Tanzania na Afrika Mashariki kwa kikanda hivi sasa, *priority* iliyopo ni kujenga reli inayotoka Tanga - Arusha – Musoma. Sasa hii reli anayoizungumza Mheshimiwa Mbunge, itajengwa kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Amina Amour, pia alizungumzia kwamba Zanzibar inashirikishwaje katika mchakato wa uendelezaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki? Hili nimeshalizungumza kwamba, kuna hatua kwa hatua tangu waanzishe vikosi kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Habib Mnyaa, anauliza ni sifa gani ambazo *project* inatakiwa iwe inazo ili ikubalike? Maana yake hizi ni *special:* Je, nyingine zikoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa ni ndogo tu kwamba, ile *project* mnayoiibua iwe ni *project* yenye sifa za kikanda, halafu vile vile yenye kipaumbele ndani ya nchi husika. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza tu kwamba ili kuwa kipaumbele inatakiwa itoke katika Tume ya mipango ya nchi ambayo

upo halafu inaletwa. Hili ni jambo ambalo ni la kawaida kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja hii ya lugha ya Kiswahili. Kwanza, niseme kwamba Kiswahili ni lugha ambayo sasa hivi inafundishwa karibu katika nusu ya Bara la Afrika. Vilevile, katika Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2012 kulikuwa na mchakato wa kutoa Tume tatu. Tume ya Kiswahili imethibitishwa kwamba ibakie Tanzania na Makao Makuu yake yako pale Krotana Zanzibar. Kwa hiyo, hili ni jambo la mwanzo la kufurahia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kulikuwa na hoja kwamba, kwanini hii lugha ya Kiswahili haitumiki katika Bunge la Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hoja nzuri na ambayo itatutangaza sana Watanzania na kutuunganisha Wana-Afrika Mashariki. Lakini, labda kazi hii Waheshimiwa Wabunge wa Afrika Mashariki, niliwahi kusikia fununu kwamba kuna Mbunge mmoja anataka kupeleka Muswada wa Sheria kwamba Kiswahili kitumike katika Bunge la Afrika Mashariki. Wizara inasema, itamsaidia sana na iko pamoja naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hata Bunge lako Tukufu litakuwa pamoja na huyu Mheshimiwa Mbunge ambaye anataka kupeleka pendekezo kwamba Kiswahili kitumike katika Bunge la Afrika Mashariki, kama vile kinavyotumika katika Bunge la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *visa* moja katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Suala hili ni la mjadala mkubwa sana baina ya nchi tano za Afrika Mashariki. Suala hili kwa upande wa Tanzania mara nyingi huonekana kama Tanzania inalipinga. Lakini siyo kwamba Tanzania tunapinga kuwa na *Visa* moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuelezea kwamba, sababu za msingi za Tanzania kukataa kwa muda huu kuingia katika mchakato wa *Visa* moja ni kwamba,

inalazimisha uwepo wa mfumo wa kimuundo na kisheria juu ya aina ya *Visa* na namna zitakavyotolewa na Balozi zetu nchi za nje. Hili ni jambo la lazima. Lazima kuwe na mfumo wa kisheria na kimuundo. Pia kuwepo na mtandao makini wa mawasiliano mpakani ambao utajulisha nani ameingia wapi, lini na kwa madhumuni gani. Hili ni lazima lijulikane. Kama halikujulikana hivyo, itakuwa tunaingia kiholela tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo mtandao huo tu, vile vile kuwe na mtandao wa mawasiliano baina ya Balozi zetu zote za nchi tano hizi huko nje zinakotoa *Visa* hizi. Bila ya kuwa na uhakika wa kuwepo hilo, sasa tukiingia sisi tutasema tunaingia bila kujipanga.

Mwisho kabisa, *Visa* ni mkusanyiko wa pato. Sasa je, haya mapato yatakusanywa vipi? Vilevile ni suala ambalo kwanza tunataka tujipange halafu ndiyo tuingie. Maana yake Watanzania tumekuwa tukiambiwa kwamba ni kama *road blockers*. Siyo *road blockers* lakini tunataka tuwe na mambo thabiti na lile tunalolifanya tuwe na uhakika nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine ambayo Mheshimiwa Amina Amour aliiuliza kuhusiana na hii *issue* ya *work permit* kwamba, kwanini baadhi ya nchi katika Afrika Mashariki zimepeana misamaha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna mambo mawili, kuna kupeana msamaha wa tozo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunakushukuru hasa kwa kuwakumbusha vijana wa Tanzania wawe mashababu na wajitahidi kuwa mashababu katika miradi mingine mingi ya Afrika Mashariki. Hicho ni Kiswahili

kipya kabisa, nadhani nitatafuta nafasi utusaidie kujua maana ya ushababu. Mimi hapa nimeishaipata tayari. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Waziri mtoa hoja ili na yeye aweze kujibu hoja zake. *(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitangulie kama ilivyo ada kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha sote kuwa hapa na kuchangia kuhusu maendeleo ya nchi yetu.

Pili, niwashukuru wachangiaji 10 waliopata nafasi ya kuchangia kwa kuongea na Waheshimiwa Wabunge 32 waliopata nafasi ya kutuandikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zote ni darasa kwetu, zinatusaidia kuelewa kwa upana zaidi mafanikio na udhaifu katika Wizara yetu. Kwa hiyo, nawashukuru sana nyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda kwa haraka sana kwa sababu muda niliobaki nao ni nusu saa, dakika 30, tumegawana sawia na Naibu Waziri. Kwa hiyo, zaidi nitatamka maeneo na majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ni malipo kwa wale waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Watani zetu CHADEMA tunaendelea kuwazoea tu kwa sababu kutumia sana hoja za nguvu hivi, au kwa Kiswahili cha mjini hoja za ku-*force*, kwa hiyo, jambo linaweza kuwa limekaa hivi wao wakalipamba likawa gumu, matatizo, wanazungumza kwa kumnukuu Mwalimu Nyerere ambaye sio mwanachama wao, basi ilimradi wamegeuza... *(Kicheko)*

Huwa nawashangaa! Hawa rafiki zangu ambao wanashirikiana na vyama vya kibwanyenye huko nje, ndiyo vinavyowapa fedha kama vile *Conservative Party* ya *UK, CDU* ya Ujerumani, ndio marafiki zao. Sera za hao marafiki zao wa nje zote ni za mlengo wa kulia, lakini wakifika hapa, ni

wajamaa utadhani wakomunisti. Lakini ndivyo mambo yalivyo, unapotafuta kushika madaraka, nyenzo zote zinaruhusiwa, ila silaha tu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wafanyakazi wa Afrika Mashariki ni kama ifuatavyo:-

Tulitiliana sahihi, yaani Serikali na hawa wafanyakazi kwa uwakilishi wao, tarehe 21 mwezi Septemba, 2005. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitiliana sahihi na wale waliokuwa wanaongoza majadiliano na ikakubalika kwamba, wafanyakazi hao walipwe Shilingi bilioni 117 na makubaliano haya yameandikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wake ni kwamba hadi kufikia tarehe 30 mwezi uliopita wa Aprili, idadi ya wastaafu 31,779 wamelipwa madai yao kwa kiwango cha Sh. 116,855,650,012.75. Kwa hiyo, kufikia tarehe hiyo, jumla ya wastaafu ambao bado hawajalipwa ni 52 tu katika wale 31,700. Kwa hiyo, Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani alipoliweka kama watu hawa wameteseka sana, ni kweli ilichukua muda na urasimu kuweza kulitatua hili jambo, lakini siyo kwa kiwango kilichosemwa na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bakaa ya fedha ya kuwalipa wale 52 ni Sh. 144,349,987.25, zipo Hazina lakini tuna habari kwamba jamaa hawa 52 baadhi yao sasa wamechochewa, wanaanza kufungua madai mapya. Sasa jambo hili haliwezi kwisha, ikiwa kila tunapofika mwisho watu wanarudi nyuma wanashawishika kwamba wanaweza kupata zaidi na wanakwenda Mahakamani tena. Basi tutasubiri tuone tutafika wapi na hilo, lakini asilimia 98 ya wafanyakazi hawa wamelipwa hizo Shilingi bilioni 116.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa umeme Singida – Arusha – Namanga – Nairobi, kazi ya upembuzi yakinifu ilikwishakamilika ya kuunganisha gridi ya Tanzania kwa kutokea Singida hadi Isinya kule Kenya. Njia hii ni kubwa sana, ni njia ya umeme wa Msongo wa kV 400 na inategemea sana

kukamilika kwa kuunganisha umeme kutoka Zambia. Kazi hii inaendelea pande zote mbili, kusini na kaskazini mwa Tanzania. Tumekwishapata miadi ya kupata fedha za kujenga mradi huu kwa pande zote mbili, kusini na kaskazini kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Dunia. Gharama za Mradi ni Dola milioni 242.09 na tumefikia hatua nzuri sana ya kuweza kukamilisha upatikanaji wa fedha ili mradi uweze kujengwa ndani ya muda wa miaka miwili, waliokadiria wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, amejibu masuala Ofisi ya Zanzibar na kwamba sasa imetoka pale Ikulu na ipo mahali pake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ya kushughulikia Sera ya Ushirikiano tunakwenda vizuri, tunatarajia kwamba mapema katika mwaka ujao wa fedha Julai/Agosti tuwe na machapisho kamili ya Sera ya Mtangamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilihusu tafadhali tulizopewa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali kuhusu hatua mbalimbali za Mtangamano. Ni hakika mambo ya Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja ni magumu, lakini magumu zaidi ni mambo ya Umoja wa Fedha na hatimaye shirikisho la kisiasa. Lakini wale ambao tafadhari yao inatokana tu na kutuambia kwamba Umoja wa Ulaya ulipata taabu, tuache hayo mawazo kwamba Wazungu wakishindwa kitu, basi na sisi hatukiwezi. Waache Wazungu washindwe, lakini sisi tunakwenda hatua kwa hatua kuhakikisha kwamba umoja wa fedha tunaoujenga, utakuwa imara na utadumu. *(Makofi)*

Katika hili, kuna baadhi ya wachangiaji walikuwa wakisema kwamba Tanzania ndiyo ipo chini zaidi. Katika vile vigezo vilivyowekwa vya nakisi ya bajeti, kiwango cha mfumuko wa bei na kadhalika, sisi Tanzania ni imara zaidi kuliko nchi zote ukiacha Kenya. Lazima uvisome hivyo vigezo, usitazame tu ubadilishanaji wa fedha. Kuna vigezo vya mfumuko wa bei, vigezo vya nakisi ya bajeti, kuna kigezo cha

ukopaji, ni asilimia ngapi ya pato la Taifa. Katika hivyo, sisi ni namba mbili na kuna uwezekano kabisa wa kufikia vigezo hivyo kabla ya miaka mitano. Lakini msiwe na wasiwasi, tumepeana miaka kumi ili mambo yote yakienda vizuri, basi mwaka 2023 ndiyo tunatarajiwa kuwa na sarafu ya pamoja. Mwaka 2023! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru hili suala la kuwawezesha Watanzania kupata ajira tunaendelea nalo kwa njia mbalimbali. Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki linasimamia mitaala ili viwango vya elimu kwa shahada ama stashahada, shahada ya pili na kadhalika vilingane, na hilo litakuwa ndiyo jambo nzuri la kutuwezesha kuwaweka katika uwanda mmoja wasomi wetu wanapotafuta ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishauriwa kwamba muundo wa Wizara uboreshwe na kuongeza Idara ya Utafiti. Hata Kamati yetu, tunawashukuru sana Kamati ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wamependekeza hili. Ndiyo maana kunakuwa na udhaifu kiasi fulani kuhusu baadhi ya takwimu. Kwa sababu hatuna Idara mahsusi au Kitengo cha Utafiti. Tukikipata hicho, nadhani itakuwa ni vyema. Tunafanya kazi ili tuweze kuwa na Kitengo cha Utafiti na itatusaidia katika kubaini fursa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Serikali kujipanga vizuri kuingia Umoja wa Fedha, hili tumeshalizungumza. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya kushughulikia Afrika Mashariki ndiyo lilikuwa ombi la awali, lakini sasa kilichokubalika ni kwamba Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ndiyo ishughulikie suala la Mtangamano wa Afrika Mashariki. Wizara imekwishawasilisha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki mapendekezo ya kuboresha utungaji wa Sheria za Jumuiya kupitia Miswada Binafsi ili kuwezesha nchi wanachama ikiwemo Mabunge ya nchi hizo kushiriki kikamilifu katika utungaji wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lililozungumzwa sana, hata Msemaji wa Kamati ya Mambo ya Nje amelizungumzia, ni kuhoji Serikali imefanya jitihada zipi kushirikiana na nchi

Wanachama kuanzisha Mfumo mmoja wa Elimu. Sasa Wizara imeendelea kuratibu kama nilivyoeleza katika aya ya 72 ya hotuba yangu.

Aidha, Baraza la Mawaziri wa Jumuiya limeidhinisha maandalizi ya mikakati saba inayolenga kuhuisha mifumo na mitaala ya elimu katika nchi zetu. Kwa hiyo, hiyo ni kazi ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai kwamba tuanzishe Kituo cha Uwekezaji cha Afrika Mashariki, linaweza kuwa ni jambo nzuri, lakini hadi sasa tunachokifanya ni kila nchi na Kituo chake kushirikiana na kila kituo ili taratibu zetu za kuwavutia wawekezaji ziwe sawia. Hapo niseme tu kwamba, siyo kweli kwamba tunashindana kuelekea kwenye umaskini. Siyo kweli hata kidogo! Vivutio vinavyotolewa ni vivutio vya kawaida kabisa na tunakuwa waangalifu sana kuvipunguza kila sekta inapofanikiwa.

Kwa hiyo, hatutazami kwamba Kenya wanafanya nini au Uganda wanafanya nini halafu kuwaiga, hapana. Tunaangalia vipaumbele. Bahati nzuri nchi hizi, kila mojawapo nchi mwanachama ina vipaumbele vyake ambavyo siyo vinavyoshindana. Utakuta kwa mfano, nchi ya Tanzania kuna gesi, kuna maeneo makubwa ya kilimo, lakini Kenya ingawa wanashughulika na kilimo, zaidi ni kilimo ambacho kinahusu mazao ya kuuza nje kama vile maua, mboga mboga na kadhalika. Huku tungeweza kabisa kuwa ghala la Afrika Mashariki hapa Tanzania la kuuza vitu kama mchele, sukari na kadhalika, na ndivyo ambavyo tumejipanga kimkakati kuwa hivyo. Tuwe sisi ndiyo ghala la kuuzia wenzetu mazao muhimu ya nafaka kwa sababu ardhi tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo kuhusiana na uhuru wa Vyombo vya Habari; hapa nashangaa kidogo. Tanzania ndiyo ina magazeti mengi kuliko nchi yoyote ya Afrika Mashariki. Hapa Tanzania ndiyo tuna uhuru wa kuchora jambo lolote kuhusu kiongozi. Ukimchora Mheshimiwa Rais Kikwete ana miguu kama vijiti vya kiberiti, hakuna mtu anakusumbua asubuhi. Hebu jaribu ufanye hivyo Rwanda;

jaribu ufanye hivyo Kenya, jaribu kufanya hivyo popote katika nchi hizi za Afrika Mashariki. Kwa hiyo, nchi yetu ina uhuru mpana.

Sasa haya mambo yaliyoingia ya ugaidi, kwa watu ambao wanataka kuyatazama mambo haya kwa ushahidi, kuisema Serikali ya CCM kwamba inaua watu, ndiyo hizo hizo nasema hoja za nguvu tu. Maana yake unajaribu kulifanya tukio moja lionekane ndiyo tabia ya mtu. Yaliyotokea Nyororo, sasa yamefanywa ni wimbo kwa baadhi ya Vyama. Ndiyo Tanzania iko hivyo, wakatili sana! Inashangaza kweli kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu mimi, aliyekamatwa kuhusiana na mambo kama ya ugaidi gaidi ni kiongozi wa Chama fulani hivi.

Sasa kama magaidi wangekuwa upande huu wa pili, wangekuwa wanashughulikiwa. Lakini mpaka leo mtu yupo ndani na ni vyombo vya sheria vinamshughulikia. Kwa hiyo, isije ikawa ni kilio cha mamba hapa, unalia huku kumbe wewe ndiyo unamtafuna mtu huku unatoka machozi. Kwa hiyo, bado historia itatuelekeza tunakokwenda. *(Makofi)*

TAARIFA

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Ehe, taarifa!

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni taarifa ndogo tu kwa Mheshimiwa Waziri kwamba kiongozi wa Chama fulani aliyeshtakiwa kwa ugaidi, Mashtaka ya Ugaidi yalifutwa na Mahakama Kuu ya Tanzania. Kwa hiyo, kwa sasa hakuna kiongozi yeyote anayekabiliwa na mashtaka ya ugaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu. *(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikutaja Chama. Inaelekea huyu ni kiongozi wa CHADEMA basi. Watu hawa ndio taabu yao. Kwa nini CHADEMA hamuwi wastahimilivu kama wenzenu wa *CUF?* Huyo kiongozi aliyepo ndani, bado shtaka la njama... (*Makofi/Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Yupo nje!

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Yupo nje wapi? Ipo rufani. Hata tukitaka kueleza tu, alah! *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri endelea! *(Kicheko)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Chama gani ambacho mikutano yake inaandamwa na fujo kila wakati? Chama gani? *(Kicheko/Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tuendelee. Naomba tuwe watulivu. *(Kicheko)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Nadhani hoja yangu imeeleweka.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hebu tuwe watulivu, mwacheni Mheshimiwa Waziri aendelee. Huu ni utaratibu wa kuwa na ngozi ngumu. *(Kicheko/Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wamekwenda kikosi kimoja kule Jimboni kwangu Urambo eti wanasema mwaka 2015 watachukua Kiti cha Urambo. Unajua ndoto, siyo hoja! *Style* yenu hiyo, wamezomewa, wameondoka katika hali ya aibu tu. Uchukue Urambo kwa kuwa una mtu anajua kutukana? Ni ndoto hiyo! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea. Mheshimiwa Salum Barwany na wengine wameulizia kuhusu barabara

zenye sura ya kikanda. Sasa hizi tumeziorodhesha kwenye eneo *2B5* na ni mtandao ambayo unashughulikia wakati hadi wakati na unakwenda vizuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wamezungumzia juu ya Shirikisho la Kisiasa, na kwamba lije baada ya kuimarisha sarafu ya pamoja. Huo ndiyo utaratibu na ndivyo tunavyokwenda. Niwahakikishie kwamba sisi pale Wizarani kwa shughuli ya uratibu, pia na Wakuu wa Nchi wanakwenda vizuri sana katika kuyatazama mambo haya kwa mujibu wa maslahi ya kila nchi. Maamuzi yetu katika majadiliano kuhusu Umoja huu ni maamuzi ambayo yanazingatiwa kwa kuridhiana, yaani *consensus.* Kwa hiyo, tunakwenda vizuri na tunajifunza kutokana na siku za nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna swali limeulizwa: Je, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo inaweza kuwa sehemu ya Jumuiya? Sasa hivi tuna maombi kutoka Sudan ya Kusini na Somalia. Ombi la Sudani Kusini nadhani litakubaliwa hivi karibuni, lakini Somalia hatuoni kwamba mpaka sasa inakidhi vigezo vya nchi ambayo imetulia kuweza kujiunga katika Jumuiya.

Kwa hiyo, hilo litasubiri kidogo. Kuhusu *DRC* hatujapata ombi lolote, lakini ni nchi kubwa sana. Mfahamu kwamba *DRC* ina kilomita za mraba zaidi milioni mbili. Kwa hiyo, inatoka Mashariki inakuwa sehemu ya Afrika ya Kati na pia inapakana na Bahari ya Atlantiki.

Mwelekeo ninaouona hivi sasa kutoka kwa Wakuu wa Nchi, ambao ndiyo unaotuongoza ule mwelekeo ni kwamba bora ikishaingia Sudan ya Kusini, tuimarishe eneo hilo kwanza tutulie. Tusikubali wanachama wapya hadi hapo tutakapoweza kuimarisha kwa miaka kadhaa nchi zile sita. Zinawezekana, zinabebeka, unaweza kwenda nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa reli ya Tanga, Bandari ya Musoma utaanza lini? Mradi huu ni miongoni mwa miradi iliyopo katika Mpango Kabambe wa Reli ya Afrika Mashariki na upembuzi yakinifu wa mradi

unatazamiwa ukamilishwe katika mwaka ujao wa fedha 2013/2014 ni mradi mkubwa sana, mabilioni ya Dola, kwa hiyo, bado kidogo, hatuwezi kusema unaweza kuanza sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na swali kwamba kuna mkakati gani wa kuzingatia changamoto zinazojitokeza katika Umoja wa Forodha? Je, kuna mikakati gani katika kutekeleza changamoto hizo? Changamoto kubwa katika kutekeleza Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja unatokana na vile tunavyoviita vikwazo visivyo vya kiforodha *(Non Tariff Barriers - NTBs)*. Viwango vya bidhaa vinahitilafiana, na kwa hiyo, ukifika mpakani unaweza kucheleweshewa kupitishiwa bidhaa zako kwa sababu ya mambo kama hayo ya viwango na kadhalika. Lakini timu za viwango zinashirikiana, mambo ya uzito wa magari tunasaidiana.

Kwa hiyo, nadhani hatua kwa hatua yale tunayoweza kuyapunguza tunaweza. Ni kweli kwamba katika upande wa Tanzania kwa sababu barabara zetu ndiyo zina masafa marefu, basi inaonekana sehemu zile za kupima mizigo zinakuwa ni nyingi ambazo zinapitiwa na magari yanayopeleka bidhaa kwa majirani na kupitisha bidhaa kuja kwetu. Lakini tunafanya utaratibu kwa mfumo wa *electronic* wa kisasa ili magari ya mizigo yasishurutishwe kusimama kwenye kila kituo cha mizani na badala yake iwe ni vituo vitatu, mwanzoni, katikati na mwisho, mpakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine naona zimejibiwa. Kuna hoja hapa kwamba miradi mingapi imefadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki? Miradi kadhaa, mifano ni Shirika la Ndege la *Precision*, Mahoteli ya Kitalii, ikiwa ni pamoja na hoteli ya Ngurdoto na hivi vimechangiwa na mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya jinsi *TIC* na *TCCIA* wanavyosaidia katika Mtangamano, haya nayo tumekwishayaelezea. *TIC* ni chombo cha kuvutia wawekezaji na *TCCIA* inaungana katika umoja wa vyombo hivi vya *Chamber of Commerce,* kipo kimoja cha Afrika Mashariki.

Kwa hiyo, nchi wanachama vyombo vyake vya wafanyabiashara vinakutana katika chombo kimoja. Hili la kufanyika vikao vya Jumuiya Arusha, nadhani Naibu Waziri amelielezea vizuri tu. Tulichokubaliana ni kwamba angalau asilimia 50 ya vikao vitafanyika Mjini Arusha na asilimia 50 viwe kwa mzunguko. Hii pia inatoa hamasa ya wananchi wa Afrika Mashariki katika maeneo yao kuweza kufahamu shughuli zinazofanyika za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru kipekee Mheshimiwa Athumani Mfutakamba, alituandikia kuhusu athari za *aflatoxin* ambayo tayari imekwishaingia katika nchi yetu. Hii ni aina ya mdudu ambaye anatema sumu ambayo inaitwa sumu kuvu na ina athari kubwa katika mazao ya nafaka. Jitihada za pamoja zinaendelea kuweza kuwadhibiti wadudu hao ambao wanaitwa *aphids* na *trips*. Athari za chakula chochote ambacho kina hii sumu kuvu inaharibu sana viungo ndani na inasadikika pia inaleta ugonjwa wa saratani. Kwa hiyo, tunafanya bidii ili kuweza kudhibiti hali hiyo.

Mwisho, nisingependa kusema tena kuhusu Rais Museveni, ni siasa za Uganda na isingekuwa vyema tuzijadili. Lakini kuhusu Mheshimiwa Abdurahman Kinana, naona mwanasiasia huyu anawakera sana Chama fulani, maana yake hatoki midomoni mwao. Kinana, Kinana! Ukitaka kutenda haki, kuwa mtu ambaye anahusika na chombo cha usafirishaji, umhusishe na yaliyopatikana ndani ya chombo, kwa kweli mara nyingine tena tunaona ile ile hali ya watu wakipata jambo, basi lazima walivute kwa nguvu mpaka liweze kulingana na kile wanachotaka, na zaidi ni kuonesha tu kwamba watu fulani sijui sio waadilifu! Hivi hawa watu mathalan wanaojikopesha ruzuku ya Chama ni waadilifu! Hawa ni waadilifu eeh!

Kwa hiyo, mimi nadhani mambo haya tuyaache tu. Mwacheni Kinana afanye kazi yake tutapambana majukwaani na mwisho ya yote majibu mtayapata kwa wananchi mwaka 2015. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa hayo na tuache tu maana yake tutaendelea kusikia wengine wahuni wanajiita *Reverend,* lakini wahuni kabisa wa kawaida. Yaani ni raha ya kuwa humu, lakini sasa mnatufikisha mahali ambapo, nadhani wananchi wanaanza kuwaelewa vizuri sasa kwamba ni watu wa aina hiyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 97 - Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea majibu ya hoja mbalimbali, sasa naomba tuingie katika Kamati ya Matumizi. Katibu naomba utuongoze.

Kif. 1001 – *Administration and General*...Tshs. 3,883,407,000/=

MWENYEKITI: Kwa mujibu wa utaratibu wa sera, nimepata taarifa hapa, Chama cha *CUF* atauliza Mheshimiwa Sanya, halafu tutakuwa na Mheshimiwa Wenje (*CHADEMA)*; Mheshimiwa Juma Njwayo (CCM), Mheshimiwa Waride Jabu (CCM) na Mheshimiwa Masauni (CCM). Kama muda utaturuhusu, basi tutaongeza wawili, watatu wengine. Tuna dakika 25 tu. Kama muda utaturuhusu, tutaongeza wengine, usipoturuhusu tunaendelea na kanuni.

Naomba Mheshimiwa Waziri myachukue maswali yote, halafu mtayajibu kwa pamoja. Mheshimiwa Sanya.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nataka ufafanuzi tu kidogo.

Kwa kuwa katika *treaty* ya Afrika Mashariki zilikubaliana nchi zote wanachama kwamba kila nchi iwe na Wizara ya Mambo ya Afrika Mashariki, lakini baada ya uchaguzi wa Kenya, imeonekana kwamba katika kubana na kutengeneza Serikali ndogo, wameichukua Wizara ya Afrika Mashariki kuiunganisha na Wizara ya Utalii ya Kenya. Hatuoni kwamba Kenya hapa imekiuka taratibu na *treaty* ambayo imekubaliwa na nchi zote wanachama wa Afrika Mashariki? *(Makofi)*

MHE. EZEKIEL D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani tulitoa takwimu ni jinsi gani Serikali za Jumuiya ya Afrika Mashariki inavyopoteza mapato kwa lugha ya misamaha ya kodi, yaani *Tax Incentives.* Takwimu inaonyesha karibu kila mwaka fedha inayopotea ni karibu 2.8 *US Dollars* kutokana na misamaha mbalimbali ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatoa misamaha ya kodi katika nchi za Jumuiya kwa Makampuni makubwa yanayokuja kuwekeza kutoka nje, halafu tunarudi tena kuomba misaada kwenye hiyo nchi ambayo Makampuni yao ndiyo tunawapa misamaha ya kodi. Kutokana na upotevu wa fedha kiasi hiki Kambi Rasmi ya Upinzani ikapendekeza kwamba Serikali kupitia Wizara hii iende ikapeleke hoja kwenye nchi nyingine za Jumuiya ya Kuanzishwa kwa *East African Investment Centre* itakayofanya kazi kubwa ya ku-*regulate* sera za wawekezaji wanaokuja ili misamaha hii mikubwa ya kodi inayopelekea fedha nyingi kupotea kwenye Jumuiya ipungue. Mheshimiwa Waziri alitoa maelezo mepesi sana alipokuwa anatoa majibu kwenye hoja ya msingi inayoleta hasara kubwa kwenye nchi za Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba nisipopata majibu ya kuridhisha, basi nitashika Shilingi kwenye mshahara wa Waziri.

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Waride.

MHE. WARIBE BAKAR JABU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 65 alisema kufungua Ofisi ya Masuala ya Afrika Mashariki kwa upande wa Zanzibar. Lakini nimepitia randama kifungu kwa kifungu pamoja na vitabu vingine vya bajeti vyote kwenye Wizara hii, sikuona hata mahali pamoja palipopangiwa matumizi kwa ajili ya Ofisi hii. Nilikuwa nataka kujua: Je, Ofisi hii itatumia fedha kutoka kwenye kifungu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Njwayo!

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 34 mpaka 35 analieleza Bunge namna Viongozi Wakuu wa Jumuiya walivyokutana na kuidhinisha baadhi ya miradi ambayo ni muhimu sana, mojawapo ikiwa ni ujenzi wa reli inayotoka Mtwara, Songea hadi Mbambabay.

Kwanza, nataka niipongeze Serikali yetu kwa sababu jana nimeona kwenye gazeti la Mwananchi tangazo linalohitaji *expression of interest* kwa ajili ya mchakato wa ujenzi wa reli hii. Lakini swali langu dogo nililonalo, hivi Jumuiya imejipangaje kuhakikisha ujenzi huu unakamilika katika muda mfupi? Kama tujuavyo kwamba kukamilika kwa miradi hii ndiyo itatupeleka Tanzania kwenye ule uchumi wa kati katika muda mfupi ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Masauni!

MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu nilizungumzia kuhusiana na ubutu wa Ofisi ambayo ipo Zanzibar na nikapendekeza kwamba ili kukabiliana na matatizo yoyote ambayo tumeona yanajitokeza ya kutokuwa

na ufuatiliaji pamoja na uratibu mzuri, ni vyema Ofisi ile ikaongezewa meno kwa kuanzisha Idara pale Zanzibar ambayo itakuwa chini ya Katibu Mkuu moja kwa moja. Lakini katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri halikuzungumzwa hivyo. Naomba majibu ya hoja hiyo.

MWENYEKITI: Ahsante. Nilimwona Mheshimiwa Msabaha!

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa kuna miradi mingi ambayo imepangwa katika Afrika Mashariki, kwa upande wa Zanzibar ni miradi mingapi ambayo imetekelezwa mpaka sasa hivi?

MWENYEKITI: Ahsante. Nilimwona Mheshimiwa Lekule Laizer!

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu hoja za Wabunge alisema kwamba Tanzania ndiyo tumefanya ghala la chakula ili kuwauzia nchi nyingine. Lakini ukiangalia Watanzania bado wananyanyasika sana wakiuza chakula nje na hasa pale Namanga, kwa sababu Namanga ni lango la nchi. Lakini ukiangalia sana, watu wa Namanga, Watanzania, wanapata shida sana kuliko Wakenya na hasa urasimu mkubwa, vituo vingi vya kuuzuia mazao. Wakishavuka hao wenzetu wamelegeza sheria, kwa hiyo, wanafanya biashara vizuri, hakuna hizo sheria ambazo zinawaghasi wafanyabiashara kufanya biashara. Hasa pale Namanga tunaona tofauti kubwa sana kati ya wafanyabiashara wa Kenya na wafanyabiashara wa Tanzania, wa kwetu wanazuiwa sana pale mpakani. Lakini wanapoleta bidhaa kutoka Kenya hawana kizuizi. Tatizo ni hapa kwetu.

Je, Serikali haiwezi ikaweka utaratibu mzuri ili Watanzania nao wafanye biashara waone umuhimu wa Soko la Pamoja kuliko wao kunyanyasika kila siku na kulia? Kwa hiyo, naomba nipate ufafanuzi, kwa nini huku kwetu wafanyabiashara wanafanya biashara kwa ugumu na

vikwazo tofauti na Wakenya ambao wanakuja Tanzania kuingia, wanakwenda na hawana kizuizi katika nchi yao na hawa wananyanyasika; hasa wafanyabiashara wa Namanga, wana kero kubwa sana ambao wanalalamika sana kila wakati.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri!

WAZIRI WA USHIRIKIANO AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Majibu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Sanya, kuundwa kwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, biashara na utalii Kenya hakuathiri chochote katika mkataba wetu. Kulikuwa na hisia mnamo mwaka 2004 kwamba Mawaziri wanapokuwa wanachanganya shughuli nyingi, basi ile ambayo inakuwa ni ya Afrika Mashariki inapata athari. Kwa hiyo, kukawa na maelekezo tu ya jumla ambayo hayamo katika mkataba, kwamba pengine ni vizuri sasa nchi ziteue Mawaziri wa Afrika Mashariki iwe mahsusi. Lakini ukitazama kwenye mkataba wetu, ibara ile ya 8(3) inasema kwa Kiingereza: *"each partner state will designate a Minister to deal with East African Affairs."*

Kwa hiyo, wenzetu wamepitisha Katiba ambayo wameweka ukomo wa idadi ya Mawaziri. Kule Mawaziri ni 18 na wanaitwa *Cabinet Secretariats,* hawahudhurii Bunge. Ni viongozi pale, hawatakiwi kushughulika na siasa. Sasa huu ni utaratibu mpya kabisa. Imebidi sasa Serikali ya Kenya ipunguze kutoka Wizara kama 40 ziwe 18 na kutokana na hiyo wakachanganya. Unasema lifanyike hapa? Bado hiyo, toa maoni kwenye Katiba.

Mheshimiwa Wenje anasema kwamba misamaha ya kodi inapoteza fedha nyingi, hili ni wazo potofu, watu wengi wanafikiria hivi. Mimi nimefanya *TIC* miaka tisa na nusu. Misamaha siyo kupoteza fedha, hata kidogo! Unajua unapovutia kitu, ni lazima uweke kitu. Huwezi kuwa huchangii halafu wewe unasema tu watu watakuja.

Mazingira ya nchi zetu hizi ni magumu kwa wawekezaji na *formula* hii ya kuweka misamaha tumeiga kutoka nchi zilizofanikiwa kabisa za Mashariki ya Kusini ya Asia, Malaysia, Korea ya Kusini wote wamefanikiwa kwa kuzingatia kuvutia wawekezaji kwa kutumia misamaha. Dawa haiwezi sasa kuwa tuunganishe eti *TIC* na *Kenya Investment Authority* na hivi halafu tupate kitu kimoja. Bado haisaidii. Kwa sababu kiasi fulani cha ile misamaha itaendelea kuwepo.

Mimi hapa sizungumzii misamaha ya Mashirika ya Dini, siku hizi imezuka na *NGO* na kadhalika, sasa hayo ni mambo mengine. Lakini misamaha inayohusu kuvutia wawekezaji, ni kitu ambacho kimetumika katika kila nchi, mpaka nchi zilizoendelea kama *Ireland* imeweza kuvutia Makampuni kama *IBM*, Makampuni kama *SAMSUNG* yamekwenda kuweka Makao Makuu *Ireland* kwa sababu iliweza kuweka nafuu fulani za kodi kwa ajili ya uwekezaji.

Kwa hiyo, dawa anayopendekeza Mheshimiwa Wenje, nasikitika haisaidii sana, hatuna haja ya kuunda *East African Investment Centre;* na kisheria litafanya kazi vipi? Lazima tuje karibu tuwe labda sasa na Umoja wa Fedha na tuwe tumekamilisha Soko la Pamoja, ndiyo tunaweza kuunda Taasisi moja ya kusimamia mambo haya kama tulivyoanza kwenye upande wa ushuru wa forodha ambao hatujaunganisha mpaka hivi sasa, ndiyo tunafikia hatua za mwisho.

Mheshimiwa Njwayo reli ya Mtwara, Songea, Mbambabay imeombewa fedha kwa nguvu wa Wakuu wa Nchi za Afrika Mashariki na mimi nina hakika kwamba itakwenda kwa kasi. Nimeshuhudia vikao hivi vya Wakuu wa Nchi na uzuri ni kwamba wanapokutana, wanakuwa wamealikwa pia wale ambao wana teknolojia na fedha za mitaji kuweza kusikiliza kinachotokea pale. Reli hii ilipata uzito mkubwa sana kwa sababu wenzetu wa Msumbiji wanatuunga mkono, kwa sababu kama mnavyofahamu Kusini ya Tanzania ambapo ndiyo inaanza Kaskazini ya Msumbiji ni mbali sana, ni kilomita 2000 kwenda Maputo. Kwa hiyo, miradi ya umeme ya usafirishaji, kuboresha ile *Mtwara*

Corridor yatakuwa na faida kubwa sana kwa sababu pia yatasaidia nchi jirani ya Mtwara. Kwa hiyo, naamini tutakwenda haraka.

Mwisho, kwa yale ambayo nitayashughulikia, Mheshimiwa Lekule Laizer nilipofika pale Longido mwaka juzi na nikaenda tena mwaka 2012 tumekubaliana na Mkuu wa Mkoa wa Arusha pale Namanga kwamba soko kubwa kabisa lijengwe upande wetu. Udhaifu wa Watanzania imekuwa ni kwamba tunapeleka bidhaa kwa mnunuzi. Lazima atakulalia tu! Ukijichukua wewe ndiyo ng'ombe, sijui mahindi unapeleka mpaka kule anakwambia haya hayakufikia kiwango. Kurejea na mali, huwezi; basi anakwambia bei yoyote na hilo ndilo limekuwa likiwapata. Sasa tunataka pale Arusha na ardhi imetafutwa tuweke na maji kwa ajili ya mifugo, maji kwa ajili ya matumizi ya watu, huduma za jamii ili biashara yoyote ya pale mpakani iweze kufanyika upande wa pili yaani Tanzania. Kwa hiyo, watu wanaotaka vitu hivi watakuwa wanakuja kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza hapa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, amekwishaanza shughuli hiyo na ameshirikisha Benki binafsi kuweza kujenga soko la kisasa pale Holili kwa madhumuni hayo hayo. Tunataka iwe hivyo Horohoro, Sirari, Mtukula na Kabanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa hayo yaliyobaki, Mheshimiwa Naibu Waziri atayashughulikia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kulikuwa na suala la Mheshimiwa Waride juu ya kwamba ametazama randama, hamna kasma ya Ofisi ya Zanzibar. Namwarifu tu kwamba Ofisi ya Zanzibar kasma yake imo katika kasma ya Utawala. Sasa hivi Ofisi ile hatujaikweza na kuipa nafasi ya Kitengo. Kuikweza kwake kunatokana na wingi wa kazi na uzito wa kazi. Nafasi hiyo vilevile itatupa mtazamo wa nafasi gani ya yule Ofisa anayekaa pale awenayo. Kwa hiyo jibu ni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Msabaha aliulizia ni miradi mingapi imetekelezwa Zanzibar? Mheshimiwa Msabaha kwa hivi sasa kuna miradi miwili imeshakamilika. Kuna mradi wa kukuza mazao Zanzibar, tayari umeshakamilika; mradi ambao mwanzo ulikuwa unasimamiwa na Afrika Mashariki na baadaye ukasimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya *Taxi* ya Airport ya pale Zanzibar tayari umeshakamilika; na kwa kasma ndogo sana vilevile mradi wa kuondoa ndorobo nao ulishakamilika. Lakini pamoja na yote hayo, hivi sasa kuna Kamisheni nzima pale ya Taasisi ya Kiswahili ambayo iko Gymkhana nayo imeshakamilika na sasa hivi iko katika taratibu za kuanza kufanya kazi.

Kwa hiyo, iko miradi ambayo Jumuiya ya Afrika Mashariki imeshughulikia pale na imeshakamilika. Miradi mingine ambayo unaijua ya Pemba *Airport*, Roro, Bandari ya Maruhubi nayo vilevile tupo njiani kwa kushirikiana na SMZ ili kuikamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Masauni aliulizia kwamba ile Ofisi ina uzito gani? Kwanini kusiwe na Katibu Mkuu au Mkurugenzi? Mheshimiwa Masauni swali lako kwa kasma moja inaweza ikawa inakubalika kwamba apande daraja kwa kiasi gani. Lakini hii Ofisi tangu ifunguliwe ina karibu kama miezi mitatu tu sasa hivi. Kulingana na uzito wa kazi, huyo Afisa ni Afisa mwanzilishi na hili jambo halikuwepo sasa hivi. Kwa hiyo, hatua kwa hatua hayo mawazo yako tutayachukua na kwa kusema kima cha utendaji wa kazi tutamwongeza cheo yule mtendaji aliyeko pale.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - *Finance and Account* ... ... Shs 366,411,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 - *Policy and Planning* ... ...Shs13,281,579,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cheyo na Mheshimiwa Mnyika. Haya, Mheshimiwa Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nazungumzia kasma 270200 - *current grant to international organization* ambacho ndiyo kifungu cha Wizara hii kulipia michango ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kimeongezeka kutoka Shilingi bilioni 8.8 mpaka Shilingi bilioni 12.5 mwaka huu sawasawa na ongezeko la asilimia 41. Yaani mwaka huu ukiondoa michango tuliyolipa mwaka 2012 ambayo tutalipa tena mwaka huu tunalipa Shilingi bilioni 3.6 ya ziada sawasawa na zaidi ya Shilingi milioni 3,600 kama michango kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni fedha nyingi sana za umma, ni muhimu ziendane na manufaa kwa maana ya *value for money*. Ningependa Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi, ongezeko hili la ada na michango ambayo tunalipia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki linaambatana na maslahi gani ya ziada ambayo kama nchi tunapata baada ya ongezeko kubwa hili la Shilingi bilioni 3.6 kama michango kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba mwaka 2012 Shilingi bilioni nane zilikuwa ni fedha ambazo ni chache tulizopewa kwa kulipia *fee* ya Afrika Mashariki. Pesa hizi zimetufanya tuwe na deni kubwa na tulipata *contingency* kwa sababu zilitakiwa zilipwe karibu Dola milioni 11.1. Hizi zinalipwa kwenye *contingency*. Sasa kutoka Dola milioni 11 kwenda milioni 12 ndiyo hali ambayo ipo sasa hivi. Kwa hiyo, ongezeko lifahamike kwamba ni kutoka milioni 11.1 kwenda milioni 12. Kwa hiyo, ni milioni moja tu ndiyo ambayo imeongezeka, na zote hizi zimo katika *documentation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cheyo!

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Waziri, amejibu swali langu.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1004 - *Trade, Finance and Investment* ...Shs 641,534,000/=

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Rashid Abdallah. Kuna mwingine? Mheshimiwa Rashid!

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kwenye kasma ya 220300. Kitengo hiki cha *Trade, Finance and Investment* ni muhimu sana. Mwaka 2012 kilitengewa Sh. 4,400,000/= lakini mwaka huu hakuna fedha yoyote. Sijui kwanini hakikutengewa fedha hata moja?

MWENYEKITI: Ehe, Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, manunuzi yote hayo yamepelekwa katika Utawala.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma 221100 - *Travel out of country* mwaka 2012 kilitengewa Shilingi milioni 278, mwaka huu imetengewa Shilingi milioni 228 ikiwa imeshuka kwa kiwango cha Shilingi milioni 54.6...

MWENYEKITI: Ni 224 Mheshimiwa Mnyika, siyo 228.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mwaka huu imetengwa Shilingi milioni 224, ikiwa imeshuka kwa kiwango cha Shilingi milioni 54.6 kwa mahesabu ya haraka. Sasa hii ndiyo Idara inayohusika na biashara, fedha na uwekezaji. Ni Idara ambayo inaisaidia nchi yetu kwenye masuala yanayohusiana

majadiliano ya Umoja wa Fedha, masuala ya majadiliano ya Umoja wa Forodha na masuala ya Soko la Pamoja. Kwa hiyo, ni Idara muhimu sana.

Napenda kupata maelezo, kwa sababu kimsingi kazi ya Wizara hii ni kwenda kufanikisha masuala kama hayo ya majadiliano. Ni kwanini kuna kushuka kwa kiwango cha mgao wa fedha kwenye Idara hii muhimu?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la swali la Mheshimiwa Mnyika, kwanza ni kutokana na *ceiling* ufinyu wa bajeti, lakini vilevile sasa hivi tunatumia *electronic means* na *teleconferences* kwa ajili ya Mikutano katika Wizara yetu. *(Makofi)*

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1005 - *Economic and Social Infrastr.*... ...Shs. 650,217,000/=

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma 221100 kuna *contradiction*. Hii ni Idara ya *Economic and Social Infrastructure* kwa maana ya miundombinu ya kiuchumi na kijamii. Kwenye kifungu cha *travel out of country,* kifungu kile kile kama kwenye Idara nyingine muhimu. Idara hii kiwango cha fedha kimeongezeka kutoka Shilingi milioni 180.8 mpaka Shilingi milioni 202 ambayo ni sawa na ongezeko la Shilingi milioni 20.

Sasa kama kifungu cha masuala ya majadiliano yanayohusu biashara, uchumi na kadhalika kwa kisingizio cha *teleconferences,* kiwango cha fedha kimepungua. Ni kwanini kifungu hiki cha masuala ya miundombinu ya kiuchumi na kadhalika, ambacho chenyewe hakina safari nyingi kama kifungu hiki cha majadiliano, kimeongezewa Shilingi milioni 20?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la Mheshimiwa Mnyika ni kwamba, kama alivyosema yeye mwenyewe kitengo hiki

kinahusiana na masuala ya *social promotion* na *infrastructures,* ni kusema kwamba sasa hivi maonyesho mengi yanafanyika, maonyesho ya Juakali, maonyesho ya NaneNane na Wizara imeanza mpango wa kuchukua wajasiliamali wadogo wadogo kwenda kule kuwakutanisha na wajasiliamali wenzao ili waweze kuongeza *capacity*. Kwa hiyo, kifungu hiki kimeongezeka hela kwa kuwasaidia wananchi na siyo kwa Maafisa kusafiri.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1006 - *Political, Defence and Security*...Shs 391,108,000/=

MWENYEKITI: Nimewaona Mheshimiwa Mnyika na Mheshimiwa Leticia. Nakupa nafasi Mheshimiwa Leticia.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 1006 - *Political defence and security* kasma 221000 - *travel in country*. Kifungu hiki kimeongezeka kwa takriban Shilingi milioni 50 ukilinganisha na mwaka 2012. Napenda ufafanuzi tufahamu ni shughuli gani zaidi ambazo zimeongezeka mwaka huu ambazo pengine mwaka 2012 hazikufanyika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, safari hii kilichoongezeka ni suala la mazoezi ya kijeshi ambayo tunayafanya kwa mzunguko kwa nchi. Sasa mkiwa ndiyo *host*, yaani zamu yenu sasa matumizi yanakuwa makubwa. Mwaka 2012 tulifanya Kigali Rwanda, mwaka huu tunatarajia kufanya Tanzania. Kwa hiyo, itakuwa gharama zaidi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 102(1) ya kufanya mabadiliko kwamba katika Kamati ya Matumizi

Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja ya kutaka kufanya mabadiliko katika makadirio ya matumizi ya Serikali iwapo mabadiliko hayo hayatabadili madhumuni ya fungu.

MWENYEKITI: Hayo mabadiliko yako yanasemaje?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mabadiliko kwenye kifungu cha 221000 - *travel in country* ambacho kimeongezewa kiwango cha fedha kutoka Shilingi milioni 29.5 za mwaka 2012 mpaka Shilingi milioni 80.8 za mwaka huu. Maelezo ambayo yametolewa na Mheshimiwa Waziri...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika, hicho ni kufungu ambacho amekihoji Mheshimiwa Letecia Nyerere?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Yeye amehoji ufafanuzi. Mimi nataka kutoa hoja.

MWENYEKITI: Kwa utaratibu ni kwamba kifungu hicho kikishahojiwa na kutolewa maelekezo.**..**

MHE. JOHN J. MNYIKA: Yeye amehoji, mimi nataka kutoa hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika, naomba uketi. Utaratibu wa uendeshaji wa shughuli zetu ndani ya Bunge wote tunafahamu, na ni utaratibu unaotumika. Kifungu kimoja kikishahojiwa na Mheshimiwa Mbunge aliyetangulia, hayo yote mkitaka tuyabadilishe, tutayabadilisha kwa utaratibu utakaotakiwa na tutafanya kwa utaratibu ambao utaruhusu wote kutendewa haki. Tumefanya hivyo toka Bunge hili limeanza, hata mimi mwenyewe Mheshimiwa Spika, alishanikatalia kurudia kutoa hoja katika kifungu ambacho kilishahojiwa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1007 - *Procurement Management unit*.. Shs 182,132,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1008 – *Government Comm. Unit*…… Shs. 383,594,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rukia, *Microphone* yako haisikiki.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kwenye kifungu 221300 - *educational material, supplies and services*. Kifungu hiki kimepungua kwa kiasi kikubwa sana. Mwaka uliopita kulikuwa na Shilingi milioni 55, mwaka 2011 kulikuwa na Shilingi milioni 28 na mwaka huu kuna Shilingi milioni 10. Je, haya matumizi hayapo tena au kuna kitu gani hapa? Naomba ufafanuzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la Mheshimiwa Rukia ni kwamba manunuzi mengi tulifanya mwaka 2012, na mwaka huu yamepungua. Kwa hiyo, ndiyo maana kifungu kimebakia kuwa hivyo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1009 - *Mgt Information Syst* …. …. ….. ….Shs 337,318,000/=
Kif. 1010 - *Internal Audit Unit*... …. …. …. …. .Shs 167,321,000/=

(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1011 - *Legal Services Unit* . …. …. ….. …Shs 185,486,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyaa!

MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kasma 410600 - *acquisition of Office and General Equipment*; ni ununuzi wa vifaa vya Ofisi, na katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba kumeshafunguliwa Ofisi pale, iko Zanzibar, jengo lile la *ZSTC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri na inawezekana Ofisi imefunguliwa inataka kuingizwa vifaa vipya. Lakini mimi nataka ufafanuzi kwamba Ofisi hiyo itakuwa pale Unguja tu? Kwa sababu nature ya vile visiwa Unguja na Pemba na wafanyabiashara maarufu Kenya ni Wapemba kule na wako karibu zaidi na Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Ofisi itafunguliwa kwenye kisiwa kimoja tu au itafunguliwa na Pemba na fedha hizi zitatumika ili kwenda ku-*furnish* hiyo Ofisi itakayokwenda kufunguliwa Pemba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka maelezo, kwa sababu ya muundo wenyewe na ili wananchi wawe huru wapate na wapate kuuliza mambo ya Afrika Mashariki. Sasa haiwezekani katika maumbile ya vile visiwa ukafungua Ofisi Unguja tu, usifungue Ofisi Pemba. Naomba ufafanuzi. *(Kicheko/Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la swali la Mheshimiwa Mnyaa la kuchomekea ni kwamba hizi Sh. 4,240,212/=ni kwa ajili ya *Legal office* pale Zanzibar na vilevile zitatumika kwa ajili za harakati za kuimarisha Mtangamano wa Afrika Mashariki kwa ajili ya Pemba na Unguja. *(Makofi)*

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hatuna *development budget*. Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja, taarifa.

TAARIFA

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashiriki kwa Mwaka 2013/2014 yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Spika na viongozi wengine wote wa Bunge, kuwatakiwa kila la kheri Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki - Mheshimiwa Samuel Sitta na Naibu wako.

Waheshimiwa Wabunge, tunaamini kabisa Jumuiya hii kama tutaitumia vizuri, Watanzania tutanufaika kiasi

kikubwa na kiasi cha kutosha. Wahenga walisema umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. Kwa hiyo, naomba niwashukuru na niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango na mawazo.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha Bunge, naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Nchi aweze kutoa hoja ili kesho tuweze kuendelea na shughuli za Bunge.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (BUNGE, SERA NA URATIBU): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja chini ya kifungu cha 153(1) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013 kama ifuatavyo:-

KWA KUWA, Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge wa kushughulikia Bajeti ya Serikali pamoja na Shughuli nyingine za Bunge zilizopangwa, zimepangwa kumalizika tarehe 28 Juni, 2013;

NA KWA KUWA, ratiba ya shughuli zote zilizopangwa kufanyika katika Mkutano huu wa Kumi na Moja, zimepangwa kwa kwa kuzingatia Kanuni ya 99(1) cha kanuni za kudumu za Bunge, toleo la 2013;

NA KWA KUWA, tarehe 22 Mei, 2013 Mheshimiwa Spika alilazimika kusitisha mjadala wa Hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini kufuatia vurugu zilizotokea Mkoani Mtwara ili kutoa nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge kutafakari jambo hili;

NA KWA KUWA, siku ya Alhamisi tarehe 23 Mei, 2013 ambayo ndiyo ilipangwa kuhitimisha hoja ya Wizara ya Nishati na Madini, Bunge liliahirishwa mapema mara tu baada ya Serikali kutoa taarifa juu ya hali halisi ya matukio yaliyotokea Mtwara na Spika kuagiza Kamati ya Uongozi ya Bunge kukaa na kuzingatia jambo hilo, pamoja na kupanga siku ya kuhitimisha hoja ya Wizara hiyo;

NA KWA KUWA, katika kikao cha Kamati ya Uongozi ya Bunge kilichofanyika kwenye ukumbi wa Spika tarehe 23 Mei, 2013 Wajumbe wa Kamati hiyo waliazimia kuliomba

Bunge likubali kufanya kazi siku ya Jumamosi, yaani kesho tarehe 25 Mei, 2013 ili kujadili na kuhitimisha hoja ya bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2013/2014;

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2013 Bunge haliwezi kufanya kazi siku ya Jumamosi, Jumapili au siku za mapumziko;

NA KWA KUWA, ili kuliwezesha Bunge kuweza kukutana siku ya Jumamosi tarehe 25 Mei, 2013 ni lazima Bunge litengue Kanuni ya 28(15) cha Kanuni za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 153(1).

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Kumi na Moja, Kanuni ya 28(15) itenguliwe kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 28(15) ambayo kwa ujumla wake inaelezea kwamba Bunge halitakutana siku ya Jumamosi, Jumapili na siku za mapumziko, itenguliwe na badala yake Bunge likutane siku ya Jumamosi tarehe 25 Mei, 2013, kesho kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa nane mchana isipokuwa kwamba kwa siku hiyo hakutakuwa na kipindi cha maswali kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo ina mantiki kabisa na ni hoja ya msingi. Basi kwa mujibu wa taratibu za Bunge ili iweze kuhalalishwa, ni lazima nilihoji Bunge na kupata ridhaa ya Bunge.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Hoja ya Kutengua Kanuni ya 28(15) ili Bunge liweze kukaa Siku ya Jumamosi ilikubaliwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa Tatu Asubuhi.

(Saa 1.00 jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumamosi, Tarehe 25 Mei, 2013 Saa Tatu Asubuhi)